Kikao cha Tatu - Tarehe 20 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 47

Bugudha na Masumbulizi kwa Diaspora wa Zanzibar

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma)- Aliuliza:-

Wazanzibari walio wengi wakiwemo Wapemba na Waunguja wamekuwa wakiishi nje ya Zanzibar, kama wawakilishi nje ya Zanzibar kama vile Tanzania Bara katika mikoa mbali mbali pamoja na nchi za nje kama Diaspora.

Kwa kuwa Wapemba wanaoishi nje kama diaspora hawasumbuliwi na yeyote wala kukebehiwa kwa lugha za hofu, kinyume na wale wanaoishi Tanzania Bara ambao siku hadi siku ni masimbulizi na lugha za hofu, sio tu kutoka kwa watu wa kawaida pekee, lakini hata kwa Rais wa Jamhuri pale alipozindua Bunge la Katiba.
Je, hili huwa linafanyika kwa bahati mbaya au ni mpango maalum ulioandaliwa na upande wa pili na Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 47 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hakuna upande wowote wa Muungano wenye nia ya kukebehi au kuanzisha lugha za hofu kwa wananchi, bali nia na dhamira ya serikali zetu mbili ni kuwahakikishia wananchi wanaishi kwa pamoja na kufanya shughuli zao za kiuchumi bila ya bughudha, bila vikwazo, na kufurahia maisha yao katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; iwe Bara au Zanzibar na ndio maana hadi leo wananchi wa kila upande wa muungano wanaendelea kuishi na kufanya shughuli zao za maisha bila ya matatizo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Saleh Nassor Juma, si busara kuhusisha Wazanzibari wanaoishi Tanzania Bara ama Watanzania Bara wanaoishi Zanzibar na wale Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kwani hawa ni Watanzania wanaoishi kwenye nchi yao, na wale Diaspora ni wale Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania.

Mhe. Spika, waasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume waliunganisha nchi zetu mbili za Tanganyika na Zanzibar kwa nia ya kuendeleza umoja wetu ambao unatokana na mahusiano ya kidugu ambayo yameanza kwa miaka mingi kabla ya Muungano wa mwaka 1964.

Mhe. Spika, naomba ieleweke kuwa lipo wingu la baadhi ya wanasiasa ambao kwa makusudi wana nia ya kudhoofisha na hatimaye kuvunja Muungano, hivyo wanatumia kila mbinu ya kuficha ukweli unaosemwa hata kusingizia viongozi wetu wakuu pake wanapotanabahisha jambo kwa nia njema.

Mhe. Spika, sikubaliani na Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati anazindua Bunge la Katiba alitumia lugha za masimbulizi au kuwatia hofu Wazanzibari wanaoishi Tanzania Bara.

Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na maelezo mengine alielezea uhusiano wa kijamii na kiuchumi uliojengeka baina ya Wazanzibari na Watanzania Bara na kutoa mifano mingi yenye kuonesha udugu uliopo na haja ya kusisitiza na kuimarisha muungano wetu kwa madhumuni ya kutoa nafasi kwa wananchi kufanya shughuli zao za maisha bila ya vikwazo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, Ahsante sana kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake mama alisema kwamba hakuna upande wowote wa Muungano uliokuwa ukikebehi upande wowote. Lakini je, Mhe. Waziri kwa nini vitendo vilivyotokea katika Bunge la Katiba vya matusi ya kashfa hayakukatazwa mpaka kufika hadi baadhi ya Wabunge kuondoka katika Bunge lile. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa bahati wewe mwenyewe katika kikao cha *briefing* ulisema si vyema kuyachukua matukio yaliyotokea katika Bunge Maalum la Katiba na kuyaleta katika Baraza hili la Wawakilishi. Lakini Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwanajuma Mdachi kwamba masuala ya baadhi ya Wabunge kuondoka katika Bunge lile hususan maarufu kwa jina la UKAWA walitoka kwa sababu nyengine wanazozielewa wao na masuala haya ambayo yalitokea lugha zisizo za kuridhisha mule ndani yalitokana na pande zote mbili zilizokuwa zikitupiana maneno. Cha msingi ni kuacha tabia za namna hiyo katika mambo ya msingi ya kujenga nchi yetu. Kule Bungeni Dodoma tulikuwa tunajenga suala zima la hatma ya nchi yetu, inapaswa tuwe na nidhamu, tufanye maelezo yetu kwa kujenga hoja, si kwa kutupiana maneno ambayo hayatoridhisha kwa kila upande.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tutakapokuwa Dodoma tujenge hoja za kuimarisha Muungano wetu, tujenge hoja ya kuwa na Katiba bora. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe.Waziri kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Waziri, mimi nataka kueleza na kumuuliza Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Kwa hofu aliyosema Mhe. Saleh ni akili, na kwa kuwa hofu humfanya mtu kuacha jambo ambalo anafikiria kulisema au kulifanya, na kwa kuwa siku za hivi karibuni kumekuwa na lugha zenye kuashiria kuvunjika kwa Muungano. Je, Mhe.Waziri utakubaliana nami kwamba viongozi wa nchi kuwatanabahisha wananchi juu ya athari zinazoweza kutokea baada ya kuvunjika Muungano ni kuwaeleza jambo ambalo lina hatima njema kwao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikubaliane naye kwamba Viongozi wetu Wakuu na viongozi wote wale wenye nia njema wanazungumzia suala zima la kuimarisha muungano kwa msingi wa kujenga umoja wa nchi yetu, amani na utulivu na kutoa nafasi kubwa ya kufanya shughuli za kiuchumi.

Kwa msingi huo huchukua kila hadhari katika kuwatanabahisha wananchi wetu umuhimu wa muungano na maendeleo ya kimaisha ya kila siku ya wananchi wetu. Ndio maana wanapenda kuonesha yale mambo ambayo yanaweza kutokea na yakaathiri wananchi wetu kibiashara, kiuchumi na kijamii; mambo ambayo hayaleti mustakbali mwema wa nchi yetu. Kwa hivyo kinachofanyika na viongozi wetu ni jambo sahihi na wale wote wenye nia njema ya kuimarisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye sehemu (a) na (b).

Kwanza kwa kuwa katika Bunge la Katiba, yalizungumzwa masuala ya Wapemba wanaoishi katika Kisiwa cha Unguja wahame, na kwa kuwa tunajua kwamba Zanzibar ni Visiwa viwili Unguja na Pemba na Visiwa vidogo vilivyomo katika visiwa vikubwa hivi.

Je, ana tamko gani kuhusiana na suala hili ambalo kiasi fulani lilichafua hewa ya wananchi hawa.

Lakini la pili, kuna watu walithubutu kusema kwamba wanahoji mkataba wa Muungano wa Kisiwa cha Unguja na Pemba. Je, kuna mkataba wowote kwa fahamu yako Mheshimiwa uliounganisha Visiwa hivi vya Unguja na Pemba bila ya usawa wao. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba lile swali la kwanza alirudie sikulisikia vizuri na aseme kidogo karibu ya *speaker* ili niweze kufahamu. Sio Spika Kificho, *speaker* ile yake anayozungumzia.

Mhe. Spika: Rudia swali la kwanza.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Swali (a) nilikuwa ninauliza kwamba baadhi ya Wabunge wa Bunge la Katiba kutoka Zanzibar hasa katika Kisiwa cha Unguja walisema kwamba, Wapemba wanaoishi Unguja wahame. Je, una tamko gani Mhe. Waziri na swali hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, napenda nirudie tena maneno yangu, maneno yako na maneno ya Waheshimiwa Wajumbe hapa kwamba si vyema kuyachukua yaliyotokea katika Bunge la Katiba na kuyaleta hapa. Ni vizuri kuyatafakari yale mema tukaenda kuyaendeleza kule na yale tunayoyaona hayastahiki ambayo yanaharibu jina la Zanzibar, uwakilishi wa Zanzibar katika Bunge lile Maalum la Katiba tukayaacha, na sasa tukazungumzia mambo ya msingi ya kujenga Katiba bora itakayotusaidia.

Mhe. Spika, naomba nimjibu swali hili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Hakuna mkataba wowote wa kuanzishwa Pemba na Unguja, Pemba na Unguja tokea asili dahari na dahari ni nchi moja; na ndio maana tunayo Zanzibar na wananchi wote; awe anatoka Pemba, awe anatoka Unguja ana haki ya kuishi katika sehemu yoyote hata kule kwa Mhe. Haji Omar Kheri Tumbatu wapo wapemba na kwengine. Vile vile wapo waunguja wanaoishi Fundo na kwengine na kwengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, si vyema hata kidogo kuzungumzia masuala ya kujigawa kwa pande za Unguja na Pemba. Ni vyema kabisa kuondosha hisia hizi tuishi pamoja, tuishi kwa amani na utulivu, sisi ni ndugu; tupendane, tuachane ndugu zangu na tofauti zetu za kisiasa ambazo tumezitia moyoni. Sasa hivi ni wakati wa kufikiria mambo ya kiuchumi na kuimarisha nchi yetu ili sisi tuishi vizuri na vizazi vijavyo. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sina kawaida hasa ya kipindi cha maswali kisimame, lakini nataka nishukuru kwa majibu ambayo Mhe. Waziri ameyajibu. Lakini swali lenyewe na maswali ya nyongeza yaliyojitokeza humu ndani yanaashiria yale mambo ambayo tulikatazana katika *briefing*. Haielekei, si vyema, haifai, ni tatizo vitu vya aina hiyo kujitokeza hapa katika Baraza hili; Baraza ambalo mimi ninayeongoza ni mdau mkubwa sana wa umoja; ni mdau mkubwa. Ni jambo linaloniuma, silipendi, sitaki kusikia kwamba watu kwa namna yoyote ile Wazanzibari wanafika pahala wanabaguana hata siku moja. *(Makofi)*

Sipendi vile vile kusikia kwamba Watanzania wanafika pahala nao wanabaguana, nataka nionye Waheshimiwa Wajumbe masuala haya yasizungumzwe katika chombo hiki. *(Makofi)*

Nalisema hili kwa manufaa yetu Wazanzibari, nasema haya kwa manufaa ya Watanzania wote. Naomba sana tuzingatie kwamba wakati wowote ambapo itafika pahala wananchi wa Visiwa hivi viwili Visiwa vyengine vidogo vidogo kufikia pahala tukaleta kubaguana kati yetu, tukaleta kitu cha kusema hao waende kwao jambo hilo halitufikishi pahala. Msuguano na tofauti hizi sisi viongozi tutabeba lawama mbele ya Mwenyezi Mungu.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuzingatie sana, sisi humu ndani ndio viongozi wa nchi hii, walioko nje ni wafuasi wetu sisi viongozi. Tuseme maneno, tutoe maelezo ambayo yatajenga sio kubomoa! Waheshimiwa Wajumbe ninawasihi sana juu ya suala hili. Ninakushukuruni sana. *(Makofi)*

Nam. 84

Ajira kwa Walemavu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kumekuwa na mwamko mkubwa wa ndugu zetu walemavu kujiendeleza kielimu licha ya changamoto kadhaa zinazowakabili.
(a) Je, walemavu wangapi wenye shahada na katika fani gani
(b) Je, kati ya walemavu hao wenye shahada ni wangapi wameajiriwa.

(c) Endapo wapo ambao wana sifa lakini hawajapata ajira, Serikali ina mpango gani wa kuwapa kipaumbele katika ajira ili waweze kuendesha maisha yao.

MUONGOZO

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na maelezo yako mazuri, ningeomba sana katika kipindi cha maswali, endapo litatokea swali lolote linalohusiana na masuala ambayo tumezungumza hapa, Mhe. Spika, ningeomba swali hilo lifutwe. Ninakushuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Haya tutazingatia hayo, lile swali ambalo litakuwa halituelekezi kwa manufaa ya wananchi tutalifuta, tutaliondoa na tunamuomba Mhe. Mjumbe ambaye ameuliza swali hilo ama arekebishe lugha liwe ni swali ambalo litaleta umoja na maendeleo katika nchi yetu. Tunaendelea, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 84 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika usajili wa Watu wenye Ulemavu uliofanyika kuanzia mwaka 2012, inaonesha kuwa kuna jumla ya Watu wenye Ulemavu 31 ambao wana shahada kama ifuatavyo:

Shahada ya Kwanza 26, Shahada ya Uzamili 4 na Stashahada ya Uzamili 1. Shahada hizo ni katika fani zifuatazo:-

- Ujasiriamali
- Sheria
- Utawala na Raslimali watu
- Fedha
- Kilimo
- Uchumi na
- Ualimu

(b) Mhe. Spika**,** kati ya Watu 31 wenye Ulemavu ambao nimewataja hapo juu, 18 tayari wameajiriwa serikalini na katika sekta binafsi. Hata hivyo, bado wapo Watu wenye Ulemavu ambao wanaendelea na masomo ya juu katika ngazi mbali mbali ambao nao wamesajiliwa.

(c) Mhe. Spika, naomba nithibitishe kwamba, suala la ajira limekuwa ni changamoto kwa ujumla si kwa Watu wenye Ulemavu peke yao bali ni kwa jamii nzima. Hadi sasa kuna idadi kubwa ya vijana wetu waliomaliza elimu ya shahada ya kwanza na bado hawajapata ajira. Kwa hivyo, Watu wenye Ulemavu ni miongoni mwa jamii wanaokabiliana na changamoto katika suala hili.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba bado ipo idadi ya Watu wenye Ulemavu wenye Shahada ambao hawajaajiriwa serikalini wala katika taasisi binafsi. Sambamba na hayo, Idara ya Watu wenye Ulemavu ilifanya vikao na Tume ya Utumishi Serikalini na kuahidi kwamba Watu wenye Ulemavu wao wenyewe waombe ajira kama matangazo ya ajira yatakavyotolewa katika vyombo vya habari mbali mbali. Pindi watakapoomba ajira basi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 Watu wenye Ulemavu katika nafasi inayoombwa watakuwa wanapewa kipaumbele.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ya kutia moyo na ya kuridhisha, kwa maana hiyo Wamarekani hawakukosea kumpa shahada ya Mwanamke Jasiri bora, leo hii inathibitika na niombe Mawaziri wengine na Manaibu Waziri waige mfano kutoka kwake, amejibu swali kwa usahihi na ufasaha kabisa.

Matangazo ya ajira kuhusu Watu wenye Ulemavu na wasioona kwa mfano, upande wa magazeti na redio kwa wasiosikia huwa hawapati tafsiri yake. Je, wizara yake inachukua hatua gani kuhusu suala hilo. Hilo la kwanza.

Pili, walemavu unapofanywa usaili katika mazingira yasiyo rafiki hasa ukizingatia majumba ya ghorofa, serikali au wizara yako inatoa kauli gani kutoka hivi sasa ili kuepukana na msongamano wa kupanda ghorofa kutokana na hali yao ya kimazingira.

Mhe. Spika: Hili swali la (b) mimi nafikiri ungeliacha liko nje kidogo ya swali la ajira kuhusu Watu wenye Ulemavu. Jibu lile linalohusu suala la ajira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli Watu wenye Ulemavu wa aina mbali mbali wana changamoto katika kuweza kushughulikia maisha yao ya kila siku, hasa pia katika suala la kutafuta ajira. Lakini naomba nimhakikishie kwamba, Idara ya Watu wenye Ulemavu iko karibu na taasisi mbali mbali ambazo ni binafsi lakini moja kwa moja na watu hawa wenye ulemavu na kuwasaidia kadri inavyowezekana katika mazingira yao kuhakikisha kwamba na wao wanakuwa ni sehemu ya jamii, katika kuomba ajira kwa kadri inavyowezekana na kuwasaidia katika kila hali.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na jitihada za serikali kuajiri walemavu, lakini imeonekana katika ajira zao taasisi au mawizara yetu miundombinu yake sio mizuri wale walemavu wanapoajiriwa kuweza kufika katika maeneo ya kazi kwa ajili ya kuwajibika.

Je, wizara yako ina mikakati gani kuweka miundombinu mizuri kwa walemavu katika zile wizara ambazo hazijaweka miundombinu hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli tuna changamoto kubwa kwa majengo ambayo yanatoa huduma kwa jamii, lakini pia katika taasisi zetu, yaani mawizara na Ofisi za serikali kutokana na miundombinu mingi yao kutoweza kufikiwa na Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, Ofisi yetu inafanya mazungumzo ya ana kwa ana kuhakikisha kwamba majengo yote ambayo yanatoa huduma za serikali yanarekebishwa kwa njia moja au nyengine, yale ambayo yanaweza kurekebishwa ili yaweze kufikiwa na Watu wenye Ulemavu iwe wafanyakazi wa Ofisi hiyo au wananchi ambao wana ulemavu na ambao wanafika katika kupata huduma hiyo.

Ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu hakukuwa na sheria iliyokuwa ikiwabana moja kwa moja watu wa taasisi mbali mbali kuweka miundombinu hiyo, mwanya huo ulitumika kwa majengo mengine kujengwa bila ya kuwekwa miundombinu. Lakini sasa kwa kweli tunahakikisha kwamba majengo yote mapya yanayojengwa ya kijamii, yaani ya kutoa huduma kwa jamii, basi yote yanazingatia uwepo wa miundombinu ambayo inaweza kuwasaidia Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kwa mara ya pili kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake mama alisema jumla ya walemavu 31 wameajiriwa na wamepata shahada mbali mbali.

(a) Je, kati ya hao 31 wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi

(b) Pamoja na walemavu ambao tayari wameshaajiriwa, lakini wapo walemavu ambao wanaishi mijini na vijijini wako vitandani hivi sasa. Je, Mhe. Waziri walemavu hao hawawezi kwenda skuli wala kufanya kazi, wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia walemavu hawa ili na wao wajisikie serikali yao inawatendea haki. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, swali lake la kwanza alitaka kufahamu kati ya Watu wenye Ulemavu 31 ambao wana shahada, stashahada pamoja na shahada za uzamili wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi. Mhe. Spika, *data* hiyo kwa sasa hivi sinayo lakini namuahidi nitamletea kwa maandishi *data* hiyo.

Lakini la pili, ameulizia ni jinsi gani Watu wenye Ulemavu ambao hawako makazini wako majumbani na wengine wanashindwa kufika hata skuli kwenda kusoma kwa watoto, serikali inawasaidiaje.

Mhe. Spika, kama mtakumbuka kwamba serikali imefanya jitihada za kutosha, kwanza kutenga fedha kwa kiasi fulani za kuweza kuwasaidia visaidizi wale ambao muda mrefu wamekuwa vitandani, lakini kwa kupata visaidizi wangeweza kuondoka na kuweza kutembea kwenda katika sehemu mbali mbali kushughulikia maisha yao hususan kwa wanafunzi watoto ambao wanashindwa kufika skuli kwa sababu ya ulemavu wao wa kuweza kutembea.

Lakini suala hili ni kubwa sana ndani ya jamii yetu, juhudi nyengine inayochukuliwa na serikali ni kuhamasisha jamii yenyewe kuwathamini Watu wenye Ulemavu. Katika tafiti zetu imegundulika kwamba bado kuna familia ambazo zinawaficha Watu wenye Ulemavu na kuwanyanyapaa. Kwa hiyo, wito wangu naendelea kusema kwamba, hawa ni wenzetu na sisi sote tuliopo hapa ni walemavu watarajiwa tusiwanyanyapae na tuwasaidie.

Jitihada nyengine za serikali ni kuanzishwa Mfuko Maalum wa Watu wenye Ulemavu wa kusaidia huduma kwa Watu wenye Ulemavu ambao umeanzishwa na unategemewa kuwa Mfuko endelevu, ili panapotokea dharura kubwa Mfuko huo uweze pia kuwasaidia Watu wenye Ulemavu.

Nam. 59

Marufuku ya Nguo za Ndani za Mitumba

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Baada ya utafiti wa kina uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imebainika kwamba nguo za ndani za mitumba kwa kiasi fulani ni chanzo cha maradhi ya kuambukiza na hivyo kuanza kupiga marufuku uingizaji wa mitumba ya nguo za ndani zikiwemo sidiria, mahafu na kadhalika.

Je, serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea kuruhusu bidhaa hizo za mitumba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, si vyema kwa wananchi kutumia nguo za ndani za mitumba kwani kama ilivyobainika katika utafiti wa kina uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaweza zikasababisha maradhi. Hivyo, katika kusimamia suala hilo, Baraza lako hili tukufu itakumbukwa kwamba, tulishapitisha Sheria ya Biashara ya Zanzibar ya mwaka 2013 (*The Zanzibar Trading Act No. 14 (2013*), sheria ambayo tayari imeweka masharti ya udhibiti wa pamoja na bidhaa nyengine ni bidhaa hizi za mitumba. Katika kifungu cha 39(2) cha Sheria hiyo kinafafanua vizuri sana juu ya udhibiti wa bidhaa za mitumba ya aina ya nguo pamoja na magodoro na mito.

Mhe. Spika, na katika kuanza kulifanyia kazi suala hili, tayari Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeanza kuwaelimisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuhusu utekelezaji mzuri wa sheria hii pamoja na madhara yatakayoweza kupatikana kutokana na matumizi ya bidhaa hizi za mitumba.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa sheria ipo ya kudhibiti bidhaa kama hizi, na kwa kuwa juzi tu tumepitisha hii sheria ya viwango ya *ZBS* ambayo vile vile inataka bidhaa zenye viwango ndio ziuzwe hapa Zanzibar. Lakini kama haitoshi ni kwamba hadi leo hii bado biashara ya nguo za ndani ambazo zina tatizo kubwa la ugonjwa wa ngozi tena katika sehemu mbaya sana zinaendelea kuzagaa katika mji huu wa Unguja kuuzwa.

Je, ni hatua gani ya dharura ambayo serikali itachukua ili kutunusuru Wazanzibari ambao hatuvai nguo zile za ndani za mitumba lakini wadau wetu wanavaa, tusije tukapata matatizo ya kiafya.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, katika kulidhibiti suala hilo ni pamoja na kutoa elimu kwa wanaohusika, na tayari wizara imeshaanza kuwasiliana na wafanyabiashara wanaofanya biashara

hizo za mitumba ili kuwaelimisha. Pamoja na kuwaelimisha huko, ni kufanya ukaguzi pale bandarini kwa bidhaa hizo za mitumba na kuzizuia ili kuzifuatilia na kuona madhara yanayotokea.

Mhe. Spika, kwa sababu sio nguo zote zinaleta madhara zaidi ni hizi za ndani, kwa hiyo, uchambuzi wa kina unafanywa katika kulifanyia kazi suala hili ili madhara hayo yasipatikane kwa wananchi.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika: Waheshimiwa hapa kidogo mnanifanya nisisikie hili swali linaloulizwa. Kwa hiyo, Mhe. Omar hapo pamoja na wengine kidogo tunyamaze. Endelea Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, Waagiziaji, waingizaji wa bidhaa za mitumba ya nguo kwa wingi hapa Zanzibar ni wangapi na ni akina nani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa sababu tayari suala hili tumeanza kulifanyia kazi; ni kwamba tumeshaanza kuwasiliana na wafanyabiashara wakubwa wanaofanya biashara hii ya kuagiza mitumba. Mpaka sasa hivi tumegundua wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa za nguo za mitumba ni wanne, yupo *Three Savana.com* wa Viwanda Vidogo Vidogo pale Amani, ambaye yeye huagiza nguo kwa wingi, kwa makontena halafu hufanya uchambuzi na kuweka kwenye *bundle* na kuzi-*export*, lakini pia, kuna Kampuni ya *Damo.com*, Kampuni ya *Hakuna Matata.com* na pia kuna Mfanyabiashara mmoja anaitwa Suleiman Mwarabu, japokuwa yeye katika kuelimika huko tayari ameanza kupunguza kwa kiasi kikubwa uagiziaji wa nguo hizo za mitumba.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu wenzetu kule Bara tayari wamechukua fursa ya kuwa watu wale wanaoingiza nguo hizi bila ya kusikia, wamepiga marufuku, lakini kuna wakaidi wanazileta. Tayari wenzetu wamechukua fursa ya kuwa zikiingia nguo zile zinakamatwa na zinateketezwa kwa kutiwa moto nguo zile, ambazo ni sidiria na nguo nyengine zilizokuwa hazifai kuvaliwa za wanawake na wanaume. Je, sisi Zanzibar tutachukua hatua gani zitakapoingizwa na wakaidi ambao hawasikii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Raya Suleiman Hamad swali kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utekelezaji wa sheria yoyote ile unahitaji kanuni. Kanuni ya sheria hii ambayo ilipitishwa hapa mwaka jana iko katika hatua zake za mwisho. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tumeshaanza kuchukua hatua za kuwaelimisha, sasa kanuni zikikamilika hatua nyengine kama hizo za kuzikamata na kuzichoma moto zitatekelezwa kufuatana na kanuni zitakavyoelekeza.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru na tunaendelea.

Nam. 26

Kuchakaa kwa Soko Kuu la Darajani na Kufanyiwa Ukarabati Mkubwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali langu namba 26 maana yake kabla sijafanya *theory* naomba nililete mezani kwako kama jana kielelezo ili Mhe. Waziri apate kuona ile hali halisi ilivyo. Mhe. Spika, naomba kumkabidhi Katibu wako.

Baada ya vielelezo hivyo Mhe. Spika, ili kumrahishia kazi Mhe. Waziri na sijawahi kumuona katika soko hilo muda mrefu kulitembelea tunakutana sehemu nyengine ili kumrahisishia kazi Mhe. Waziri nimeleta aone kadhia hii.

Mhe. Spika, naomba Serikali itoe jawabu ya swali namba 26.

Soko kuu la Darajani ni la kwanza kujengwa mwanzoni mwa karne ya 20, soko hili mbali ya huduma ya kisoko lakini pia ni eneo la historia nzuri ya Mji Mkongwe ambao ni miongoni mwa urithi wa dunia. Hivi sasa hali ya soko hilo imekuwa mbaya na limekuwa likipoteza taswira yake nzuri siku hadi siku kutokana na kukosa ukarabati wa kiwango kinachotakiwa.

(a) Nani mwenye dhamana ya jengo la soko la Darajani ambaye anaonekana kuwa ameshindwa kazi ya kulinda taswira ya sehemu ile ya urithi wa dunia.

(b) Makusanyo ya kila siku yanayokusanywa katika soko la Darajani yanakwenda wapi mpaka soko hilo kushindikana kufanyiwa ukarabati mkubwa kama ilivyofanyiwa bustani ya Forodhani.

(c) Kuna taarifa ya kuongezwa kodi kwa wafanyabiashara kwenye soko hilo kwa mara tatu ya kodi waliyokuwa wakilipa mwanzo, kwa nini mapato yanayopatikana kutokana na ongezeko hilo yasitumike kuimarisha taswira ya soko la Darajani.

Mhe. Spika: Hebu mpelekee Mhe. Waziri haraka haraka pale pengine zitamsaidia. Mheshimiwa hizi picha ilikuwa zimsaidie Mhe. Waziri anayejibu swali hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Soko la Darajani kama alivyosema Mhe. Mwakilishi ni miongoni mwa majengo ya kihistoria hapa Zanzibar na limo katika eneo la urithi wa kidunia na linahifadhiwa kama yalivyo majengo mengine ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Soko hili limekuwa likifanyiwa ukarabati wa mara kwa mara kwa kufuata muongozo wa Mamlaka ya Mji Mkongwe; lakini kwa vile ni sehemu inayotumiwa na watu wengi kila siku uchakavu huwa unajitokeza kwa haraka; na kama lingekuwa halitengenezwi lingekuwa halipo tena; bali nakubaliana naye kuwa linahitaji ukarabati mkubwa kwa sasa.

Mhe. Spika, soko hili limo katika mradi wa uendelezaji wa ukanda wa Darajani na michoro inatayarishwa ya namna gani litakarabatiwa bila kuathiri muonekano wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Taasisi yenye dhamana ya Jengo hilo ni Baraza la Manispaa na hawajashindwa kulitunza ndio maana linatumika bali kuna mpango wa kuliendeleza zaidi.

(b) Makusanyo ya soko hili yanayokusanywa na Baraza la Manispaa na mapato yake kwa mwaka jana baada ya kubadilisha viwango yalifikia milioni 16 kwa mwaka kutoka wastani wa milioni 10 kwa mwaka katika miaka iliyopita. Mapato haya hayawezi kulikarabati soko hilo na kutoa huduma nyengine za uzoaji taka na malipo ya watumishi wa eneo hilo.

(c) Nakubaliana na hoja ya Mwakilishi kuwa baadhi ya kodi zimepanda, ongezeko ambalo limesababishwa na viwango vilivyokuwa vinatozwa vilikuwa vya chini sana na ni vya muda mrefu. Pamoja na kubadilika kwa kodi hizo bado mapato yake ni madogo kulinganisha na hali halisi ya gharama za uendeshaji wa soko hilo kwa sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwanza nimsifu Mkurugenzi Mkuu wa Manispaa kwa muda mfupi tu kwa kazi anayoifanya na kukusanya mapato kwa kipindi kifupi na yakawa makubwa.

Lakini sikubaliani na Mhe. Waziri kwa hoja, na ndio maana nikaleta hizi picha ili apate kuona ile hali halisi ilivyo. Kama kweli anapata milioni 16 hapa pahali nafikiri milioni 16 hapahitajiki na picha ataona kuwa nusu tayari imeshaanguka barabara inayoelekea kunakochinjwa kuku miaka 50 soko lile halijafanyiwa ukarabati.

Mhe. Waziri huoni sawa sawa na kusema nguruwe haramu lakini mchuzi wake umaunywa wakati pale pale mnakusanya kodi na tayari mabanda yale yameshaanguka, soko tayari limeshaanguka na nusu tayari linaning'inia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza simlazimishi akubaliane na majibu tayari nayatoa. Kwa sababu mimi si mwalimu mimi ni Waziri, Mwalimu ndiye anayeweza akakuuliza swali ukajibu vile anavyotaka yeye. Kwa hiyo, naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub akubaliane na ukweli uliopo kwamba soko hili ni la muda mrefu, wakati lilipojengwa soko hili lilikuwa na wafanyabiashara wachache sasa hivi soko hili lina wafanyabiashara wengi sana kupita uwezo wako.

Lakini vile vile, soko hili lina changamoto ya kukumbwa na wafanyabiashara wasiofuata utaratibu ndio maana hali ya uchafu inazidi zaidi sokoni hapa, na kama nilivyosema serikali ina mpango wa kulifanyia ukarabati mkubwa sana soko hili katika uendelezaji wa ukanda wa Darajani. Ahsante.

Utaratibu

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, natumia kifungu cha 37 Mhe. Makame Mshimba siku zote huwa ananilalamikia huwa situmii kanuni hapa nikisimama. Lakini nitatumia kanuni ya muongozo wako namba 37.

Mhe. Spika, Waziri au Mjumbe yoyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Mhe. Waziri moja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine na Mwanasheria Mkuu.

Nilichouliza ni soko tayari limeshaanguka nusu picha zipo. Waziri anijibu tu mimi kuwa litatengenezwa au basi liendelee vile vile, wale wanaochangishwa pesa zao wataziona athari yake hivi sasa wakati wa mvua Mhe. Waziri, kwa lugha nyepesi kabisa, tena laini kabisa, kwa heshima ya hali ya juu.

Mhe. Spika: Labda ufafanuzi zaidi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nilipokuwa nikijibu swali mama. Swali lake lilikuwa na vifungu a ,b na c.

Nilisema Baraza la Manispaa au Serikali kupitia Baraza la Manispaa lina mpango wa kulifanyia ukarabati mkubwa soko hili, na ukarabati haufanywi kama soko lingekuwa liko zima na liko sawa sawa. Sasa sijui Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka nimjibu majibu yepi? Maana serikali imesema kwamba tutafanya ukarabati wa soko hili wakati wa uendelezaji wa ukanda mzima wa Darajani. Sasa hizo ndizo *commitment* za serikali, na nimesema vile vile mapato yanayokusanywa katika soko la Darajani ni milioni 16 kwa mwaka.

Milioni 16 kwa mwaka ukarabati unaotaka kufanyika pale kwenye soko la Darajani haziwezi kutosha kufanya ukarabati wa soko lile.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru na nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Waziri amekiri kwamba wafanyabiashara wa soko lile wameongezeka. Je, haoni kwamba akisema hivyo ndio nikisema kwamba:-

(a) Mapato ya hesabu hiyo yameongezeka.

(b) Kwani matengenezo ya soko hilo yanategemea tu mchango wa biashara wa soko hilo na sio mfumo wa Manispaa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

(a) Mhe. Spika, kwanza kuongezeka kwa wafanyabiashara ndiko kulikopelekea pamoja na kuengezeka viwango vya ada ndiko kulikopelekea kutoka milioni 10 mpaka kufika milioni 16.

(b) Matengenezo ya soko hilo yanategemea mchango wa wafanyabiashara tu peke yake au namna gani, hapana.

Ndio maana tukasema kwamba serikali ina mpango wa kuliendeleza soko hili au kulitegeneza pale ambapo litaendeleza eneo zima la Darajani kwa kuona kwamba mchango peke yake wa wafanyabiashara hauwezi kufanya ukarabati wa soko hili.

Nilijibu vile kwa sababu niliulizwa mapato yanayotoka pale kwenye soko yanakwenda wapi? ndio maana nikalazimika kutaja idadi ya fedha ambazo zinapatikana kwa mwaka ambazo ni milioni 16 na ukweli ni kwamba haziwezi kutengeneza soko la Darajani.

Mhe. Spika: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, swali la mwisho fupi na la nyongeza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, Ahsante sana na nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo ni mwanana kabisa.

Mhe. Waziri, pamoja na majibu yako mazuri sana, hivi sasa hivi kweli umekiri kama kweli kodi imeongezeka kwa kiwango cha juu zaidi.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuongeza kodi hiyo kunawadidimiza wanyonge waendelee kuwa masikini?

(b) Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwa ulaini kabisa kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa Manispaa pesa zinakusanywa pale haziwekwi kwa mujibu wa kisheria na mwishowe wanakula hizo pesa?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kupandisha viwango vya kodi si kuwadidimiza wafanyabiashara wanyonge ila tumepandisha viwango vya kodi kulingana na viwango hivi vilikuwa ni vya zamani na ni vya muda mrefu; na viwango vyenyewe wanavyotozwa wafanyabiashara ninavyo hapa baadae nitaomba niviwasilishe kwenu ili mvione mlinganishe kama hivi viwango ni vikubwa au si vikubwa.

Ilivyotakiwa sisi na ndio utaratibu tunaokwenda nao baada ya kuja na mageuzi ya Baraza la Manispaa lazima tufanye tathmini ya biashara mtu anayoifanya ili tupate utaratibu mzima wa kuweza kumtoza ada kulingana na biashara mtu anayoifanya, na huo ni utaratibu wa dunia nzima ulivyo. Kwa hivyo, viwango vinavyotozwa haviwadidimizi wafanyabishara wanyonge bali zimewekwa kwa mujibu wa uhalisia wa mambo ulivyo.

Mhe. Spika, naomba arudie suali la pili.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudia suali la pili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa wakusanyaji wa Manispaa hizo pesa katika hilo soko hawaziweki katika mtandao uliokuwa maalum isipokuwa wanazila?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, sikubaliani naye Mhe. Mwakilishi kwamba Watumishi wa Baraza la Manispaa kodi wanazozikusanya wanakula, kwa sababu maduka na wafanyabiashara walioko katika soko tunawajua kwa namba zao na idadi zao. Ukiacha wale ambao hawako pale kisheria.

Wafanyabiashara walioko katika soko la Darajani mboga mboga wako 30, wauza nyama ya ng'ombe na nyama ya mbuzi wako 36, wauza samaki 37, maduka makubwa yapo 3, maduka ya kati yapo 16, maduka madogo madogo yapo 6, bucha zipo 7, Mama lishe wapo 40. Kwa hesabu hii hakuna mfanyakazi wa Baraza la Manispaa anayekula fedha za wafanyabiashara ambao wamewekwa sokoni na wanalipa kodi kihalali.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na tunaendelea.

Nam. 44

Sababu za Kupotea kwa Sanaa ya Fasihi Andishi

Mhe. Saleh Nassor Juma– Aliuliza:-

Sanaa ya uandishi ni moja kati ya sanaa muhimu hapa nchini ambayo jamii kupitia sanaa hiyo husoma, hujifunza, hujielimisha na hatimaye hujirekebisha. Aidha kupitia sanaa ya uandishi, wasanii wetu hujitahidi kuelezea mambo mengi yakiwemo burudani, Historia ya nchi, sambamba na hadithi mbali mbali zilizosheheni mafunzo.

Kwa kuwa Zanzibar hapo zamani ilikuwa na waandishi maarufu ambao waliipatia sifa sana fani hii pamoja na nchi yetu, mfano wa Shafi Adam Shafi na Kuli, Dkt. Said Ahmed na Nyota ya Rehema pamoja na Asali chungu n.k.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wasanii (Waandishi) wetu hapa Zanzibar kuvunjika moyo na kazi hii ya sanaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Sanaa ya Uandishi ni moja kati ya sanaa muhimu hapa nchini ambapo jamii kupitia sanaa hiyo hujifunza, husoma, hujielimisha na hatimaye kujirekebisha. Tunafahamu kwamba Zanzibar walikuwepo waandishi maarufu akina Shafi Adam Shafi, Bwana Msa na Dk. Said Ahmed. Pamoja na waandishi hao waliojiongezea ya kuandika vitabu. Mhe. Spika, Zanzibar bado inayo hazina kubwa ya kuwa na waandishi mahiri na bado waandishi hawakuvunjika moyo bali wanaendelea kuandika, vitabu vyao vipo na idadi yao inaendelea. Mhe. Spika, wale wasanii maarufu wa zamani kina Bw. Msa, Said Ahmed Mohammed na Shafi Adam Shafi, waandishi wengine wanaoendeleza fani hii ni pamoja na:-

Bw. Haji Gora - Ambaye ametunga vitabu vya Riwaya na Tamthilia.
Bw. Ali Mwalimu - Ametunga vitabu vya Riwaya, Tamthilia na Ushairi.
Mwl. Mmanga M. Mjawiri - Ametunga Ushairi.
Bw. Hamad Pandu - Ametunga vitabu vya Riwaya
Bi Leila Mshenga Mohammed Ametunga Riwaya.
Baraza la Kiswahili la Zanzibar limetunga vitabu vya taaluma yakiwemo makamusi mbali mbali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, Ahsante sana kwa kuwa amekiri Mhe. Naibu Waziri kwamba wale waandishi wa zamani kama Bwana Msa na Shafi Adam Shafi na Said Ahmed Mohammed kazi zao zimeanza kufifia na kazi zilikuwa ni kazi nzuri sana. Kwa mfano ile kazi aliyoifanya bwana Said Ahmed katika kutunga kitabu chake cha Nyota ya Rehema ambacho kimetoa mafunzo makubwa sana kwa nchi hii na sasa kazi zile zimeanza kutopotea.

(a) Je, ni utaratibu gani ambao Wizara yake itatumia kuwashawishi hawa wasanii katika Sanaa ya Maonesho wakaweza kutoa hizi sanaa andishi za Bwana Shafi Adam Shafi na kuziingiza katika sanaa za Maonesho kama alivyofanya Bwana Shaaban Robert pale alipotunga kitabu cha Wasifu wa Siti binti Saad. Yeye Siti bint Saad amefariki lakini wasifu wake tunao kupitia katika sanaa andishi.

Sasa jee ni lini Serikali itaandaa mkakati wa kuwashawishi hawa vijana hawa wanaofanya sanaa za maigizo ili kuzi-*translate* zile kazi nzuri za Bwana Shafi Adam Shafi, Bwana Msa, pamoja na Dokta Ahmed, kuziondosha katika sanaa andishi na kuziweka katika sanaa za maigizo ya maonesho ili watu wakapata kujifunza zaidi, na kupata muelekeo, kwa sababu sanaa ni sawa sawa na kioo ambapo jamii huitumia na baadae kujirekebisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba kumjibu kaka yangu Mhe. Saleh suali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu mama nimewataja wasanii hawa au watungaji vitabu, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi Wizara yangu kwa kushirikiana na wataalamu wangu, wameunganisha nguvu zao za wazee wetu hawa ili kuweza kuwaendeleza vijana wetu na jamii kwa ujumla. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi sasa hivi Baraza la Kiswahili limetunga Makamusi kwa kuelimisha jamii, ili na ile jamii iweze kuelimisha jamii ambayo itakuja kipindi kijacho au awamu ijayo Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri suali moja la nyongeza. Kwa kuwa wasanii hawa hufanya kazi kubwa kama alivyoeleza Mhe. Saleh, Serikali kupitia Wizara ya Habari haioni kwamba sasa ipo haja ya kuanzisha Tunzo nikiimanisha *award* kwa wasanii wa uandishi kama ilivyokuwa kwa wenzetu wa Tanzania Bara; ili kunyanyua sanaa hii sambamba na kuwapa moyo wasanii kuona kwamba kazi yao wanayoifanya inathaminiwa na Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe.Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, naomba kumjibu Mhe. Wanu suali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Mwakilishi, natambua kamba wewe ni kijana, na kama nilivyoeleza kwenye suali mama ni kuwa vijana wengi tunawataka sasa hivi waweze kuendeleza fani hizi za uandishi, na nakubaliana na wewe kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali tumeandaa mpango maalum wa kuweza kuwapa tunzo wale wote waliotunga vitabu na maeneo mengine yaliyomo kwenye Wizara yetu.

Mhe. Spika: Suala la mwisho la nyongeza Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe.Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize suali moja la nyongeza lenye kifungu (a) (b) na (c).

Moja kati ya faida ya sanaa ya waandishi ni vitabu vyao kutumika kama vitabu vya rejea katika mitaala ya nchi. Na kwa sababu Baraza la Mitihani siku hizi halitumii vitabu vilivyotungwa na Wazanzibari katika mitihani yao, Jee katika waandishi aliowataja Mhe. Waziri, ni vitabu vingapi vinatumika katika mitaala ya elimu ya Sekondari Tanzania.

(b) Kama hakuna, hatuoni huko ni kuwaua kiuchumi waandishi wa kizanzibari.

(c) Je, serikali ya Zanzibar kushindwa kutetea waandishi wa Kizanzibari kwenye Taasisi za Muungano hawaoni ni kuua vipaji vya waandishi hao.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo majibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe**.** Spika, nakushukuru, naomba nijibu suali la Mhe. Salma Mohammed Ali kama ifuatavyo:

Nakubaliana naye kwamba moja kati ya faida ya sanaa ya uandishi ni vitabu vyao kutumika katika mitaala ya kufundisha vijana wetu na hatimaye vitumike katika masuala ya mitihani. Hii naipa faida kubwa, lakini nataka niseme kwamba baadhi ya waandishi ambao wanatunga vitabu vyao hivi sasa, vitabu vyao vinatumika. Nakumbuka mwaka jana katika bajeti ya Wizara yetu, ni Mheshimiwa Jussa alizungumza suala hili na sisi Wizara tukalifanyia kazi. Moja ya kazi tuliyoifanya ni kwamba tulitaka kujua jumla ya waandishi ambao wanatunga vitabu hapa Zanzibar, tukapata nadhani 40 au na kidogo.

Lakini sisi Wizara ya Habari sio ambao tunatunga mitihani na tunafundisha, tulichofanya ni kuliwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Elimu hasa Mhe. Waziri hapa, na tukakubaliana kwamba wao watavichukua vile vitabu wavihakiki waviangalie mna nini katika vitabu. Kwa hivyo, katika vitabu vile 40; vitabu kama 8 hivi vilionekana kwamba vina uwezo wa kufanyiwa kazi hiyo ya mitihani na kufundishiwa. Sasa taarifa niliyonayo ni kwamba Wizara ya Elimu wamekaa na wenzao wa Bara katika suala la kuangalia namna ya vitabu vipi kati ya vile vinaweza vikafanyiwa kazi.

Kwa hiyo, ninachomuomba Mhe. Mwakilishi, afahamu kwamba sisi katika suala hilo hatujakaa kimya kama Wizara na Serikali, Wizara zetu mbili tunashirikiana kuona vipi vitabu vile vitaweza kutumika katika Mitaala. Sisi kazi

yetu ni kuwashajiisha waandishi waweze kutunga na wenzetu wa Wizara ya Elimu basi ni kuangalia namna gani Tamthilia na Mashairi yaliyomo katika vitabu vile yanaweza kutumiwa kwa kufundishia.

Mhe. Spika, kwa hiyo, naomba Baraza lako Tukufu lijue kwamba hatuwavunji moyo waandishi wetu, tunahakikisha kwamba muda wote tunakaa nao pamoja kuwaendeleza, lakini na pia kuona kwamba kazi zao za kiusanii zinatumika vizuri. Ombi langu kwa wasanii ni kwamba wajitahidi katika kazi zao ili vitabu vyao viweze kuwa na mvuto wa kutumika katika taasisi za Elimu, lakini pia ili kuweza kujihakikishia kiuchumi waweze kujiunga na kujisajili katika haki miliki ili waweze kupata manufaa ya uchumi kutokana na kazi zao za kisanii wanazozifanya. Mhe. Spika nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri. Na sasa tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Wahesimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, na mchangiaji wetu wa kwanza asubuhi ya leo ni Mhe. Suleiman Hemed Khamis akifuatiwa na Mhe. Hija Hassan Hija wakati Mhe. Farida anajitayarisha.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu lakini pia nataka nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha, ambao mjadala wangu mkubwa utakuwa juu yake kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya na maelezo marefu lakini pia na mimi nataka nichangie katika hotuba yake.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia katika masuala mawili. Moja likiwa ni suala la miradi ya serikali na la pili ni Miradi ya wananchi. Nitajikita zaidi katika masuala hayo. Katika kufanya *reference* ya kimaendeleo ya kidunia katika nchi zetu za jirani na sisi wenyewe Wazanzibari tutajikuta kwamba wenzetu ambao ni majirani zetu, Tanzania Bara wameweza kuleta mabadiliko makubwa katika nchi yao, au katika miji yao na Tanzainia Bara kama mtu aliondoka katika kipindi cha miaka mitano, akirudi katika nchi ile basi atakuta maendeleo makubwa sana yanayopatikana, katika kutekeleza au kurakibisha mji wao ukaonekana una maendeleo na mtu akasema kwa kweli katika kipindi cha miaka mitano niliyoondoka lakini leo maendeleo makubwa sana yamepatikana.

Sifa hizo hizo na sisi tunazihitajia tuwe nazo hapa Zanzibar; tuone kwamba baada ya miaka mitano je, mabadiliko gani yamepatikana. Kwa hivyo, ninalotaka kuzungumza hapa, kwamba hii miradi yetu ya serikali ambayo tunaijadili kila siku, tunaweka tayari ili watu wananchi wetu waione miradi hiyo lakini inafikia wakati miradi hiyo haikamiliki sawa sawa.

Tukiingia katika sekta binafsi tunakuta yapo maendeleo kidogo lakini upande wa Serikali inaonekana miradi hii kila siku inadidimia na kudidimia, haiji sawasawa. Na haimalizwi kwa muda ambao tayari umepangwa, ama utakuta mradi huo haujafanywa, *not done or half done* au haupo kabisa. Au vile ulivyopangwa plani ile ya mradi ule utaukuta haukwenda kwa mujibu wa plani. Mimi nataka kuuliza ikiwa Serikali inatayarisha miradi chungu nzima na baada ya muda mrefu utakuta kwamba matatizo kwenye mradi ule yamejitokeza kuwa ni mengi. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri ni kwa nini iwe hivyo, nchi hii haina *consultants*, miradi hii haifuatiliwi?

Na nitaweza kutoa ushahidi wa kuonesha kwamba miradi yetu mingi ya serikali ambayo tunaiandaa hatima yake haifikilii katika kheri, au ikatengenezwa ikawa mizuri ikajulikana miradi hii safi kabisa. Kwa mfano wa jengo moja lililojengwa Pemba Tibirinzi, jengo lile ilipewa kampuni kujenga Tibirinzi pale, hatima ya jengo lile lilididimia na liliwahi kuzungumzwa sana katika Baraza la Wawakilishi na halikupata mafanikio na mpaka leo jengo lile limebakia kama ni kumbukumbu. Jee, hiyo si hasara ya serikali, fedha ngapi zimepotea pale.

Jengo la pili ambalo nataka kulitolea mfano ni jengo letu la *Airport*. Jengo la *Airport* vile vile baada ya kupewa kampuni kulijenga jengo lile na likaachiliwa kwa muda mrefu baadae likaonekana kwamba jengo lile halifai, Jee

hiyo si hasara? Wengine wanasema livunjwe, wengine wanasema lifanyiwe ukarabati. Sasa jee kama halikuvunjwa limefanyiwa ukarabati, hatuoni kwamba ni hasara kubwa inaongezeka, fedha nyengine zinahitajika wakati fedha zile zimeshatiwa katika kampuni.Kwa hivyo, mimi nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, katika hayo mawili jee hajayaona yeye?

Nichukue mfano wa tatu ambao kuna jengo mbele yangu mimi ambalo naliona, jengo ambalo jengo la Kisonge, ambalo litakalokuwa ni la kumbukumbu ya miaka 50 ya kumbukumbu za nchi yetu. Pia nina wasi wasi wa jengo hili kama halitafuatiliwa sawa sawa, linaweza likaibuka kama lile jengo la Tibirinzi, kama lile jengo la *Airport*, na jengo lile la miaka 50. Inawezekana wakasema kwamba plan labda sivyo ilivyotakiwa au inawezekana kwamba halifai, haya ndiyo mambo ambayo sisi yanatukuta katika nchi hii. Ndio nikataka nimuulize Mhe. Waziri kwa nini iwe hivyo? Kwa nini hatutaki kuona kwamba ufundi wa nchi nyengine unakwenda sawa sawa lakini kwetu ujenzi hauwi barabara. Tuendelee kuvunja majengo, au tuendelee kuyakarabati majengo. Nataka kujua kutoka kwake.

Miradi hii ya wananchi ni miradi muhimu sana kiuchumi, na vile vile ni muelekeo mkubwa wa sifa kwa nchi yetu. Kuendeleza miradi kama hii ni shughuli za Serikali ziwe madhubuti sana. Haoni kwamba kufeli kwa miradi hii ni kuitia kasoro nchi yetu. Huyu Rais wetu aliyeko hapa akiona kila siku miradi ya Serikali inakwenda *halfway* halafu inaharibika ama ivunjwe miradi ile iliyotengenezwa au ikarabatiwe. Kwa nini iwe hivyo, ni kuitia hasara nchi yetu, jambo ambalo si zuri. Hiyo si sifa nzuri, sijui Mhe. Waziri anaona hiyo ni sifa nzuri au sifa mbaya.

Nchi lazima tuwe na usahihi wa miradi ikiwa ni miradi ya serikali au miradi ya wananchi. Mbali na miradi kama hii ya ujenzi lakini vile vile Mhe. Waziri nataka aelewe kwamba tunakuwa na miradi mengine ya barabara ambayo nafikiri kipindi kilichopita cha 2013 katika Baraza lako tukufu hapa pamezungumzwa masuala ya barabara. Ni kilio kikubwa cha barabara za nchi yetu Unguja na Pemba jambo ambalo linasikitisha. Miradi mingi ya barabara imeanguka; imefeli katika utekelezaji wake.

Mimi kwa binafsi yangu nataka nitoe mfano wa miradi ya barabara ambayo mimi katika kipindi changu nashukuru kwamba Serikali iliitikia wito wangu wa kutaka na mimi nijengewe barabara mimi na wenzangu walioko pale katika ukanda wa Kaskazini Pemba kumetayarishwa barabara tatu; barabara moja Wete-Konde, barabara moja Wete-Gando na barabara moja Wete-Chake chake. Miradi hii imeanza 2009 hadi leo 2014 na keshokutwa tunamaliza ukanda wetu wa Baraza la Wawakilishi 2015 barabara hizi bado hazijaweza kufikia popote.

Hali kama hii Mhe. Waziri ni hasara. Tunapoingia katika miradi tuwe na uhakika kamba miradi tunaikamilisha kwa wakati wake kwa mujibu wa makubaliano. Miradi hii ambayo, ndio itakuwa mizuri, miradi hii ikiwa ni ujenzi au ikiwa ni ya barabara ni moja katika haiba ya nchi, ni moja ambayo inavutia. Sasa barabara zikiwa nzuri zinatusaidia kupeleka wagonjwa wetu mahospitali, zitatusaidia kupeleka mazao yetu katika sehemu mbali mbali. Hasa kwa sababu kisiwa cha Pemba kina Wilaya ya Kaskazini, Kati na Kusini. Kwa hivyo, biashara zinataka zipelekwe kila mahala, lakini hali ya barabara kuu hizi bado hazijakamilishwa.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa ni haiba nzuri lakini barabara hizi za Wete - Gando, Wete - Konde, na Wete - Chake hazikupata mafanikio mazuri, tangu 2009 mpaka leo 2014 na tutamalizia 2015 bado bado hazijamalizika. Kwa kusema kweli barabara hizi hazina urefu mkubwa ni kilomita 15 lakini bado mpaka leo tumeshindwa kuzikamilisha.

Nataka niseme tu kwamba tatizo linaweza kujitokeza pengine naweza kusema kama ni Kampuni au vipi, lakini mimi naweza kusema hivi, hii Kampuni ambayo wamekabidhiwa barabara hizi kampuni ya *MECCO* imeingizwa umasikini katika kutekeleza miradi hii, na sababu zipo za kutiwa umasikini.

Kwa kawaida Kampuni yoyote ya ujenzi wa barabara lazima iingie katika mkopo wa Benki, hawezi kuendesha barabara kwa kutegemea pesa zile lakini lazima aweze kuwa na mikopo katika Benki ili aweze kukamilisha kazi zake. Kwa namna hiyo basi barabara hizi tatu za Kaskazini zimeshindwa kutekelezwa, na sababu zake ni za kifedha. Kwamba huyu wa Kampuni ya *MECCO* amekuwa hana fedha za kutosha kuweza kukamilisha barabara zake, ingawa katika barabara moja hii ya Konde fedha zilizobakia ni kidogo sana, hakuna sababu za hivyo kwamba wasikamilishe lakini ziko sababu zinazomfanya yeye asiweze kukamilisha kwa sababu na yeye ameingia ndani ya mkopo katika Benki. Kwa hiyo ni lazima alipe mkopo katika Benki na apate pesa za ziada kuweza kukamilisha barabara zilizobakia.

Kwa hiyo, kwa inavyoonesha kwamba Serikali inadaiwa na kampuni hii na haijalipa Serikali deni lake. Kwa hiyo kuna fedha ambazo kampuni hii inaidai Serikali. Serikali inadaiwa kwa sababu Serikali ina barabara mbili zilizokuwa zimetengenezwa, barabara moja ya Mazizini na ile ya Fumba. Kuna fedha ambazo inadaiwa Serikali *US dollar* 2,962,221. Na fedha nyengine ambazo Serikali inadaiwa ambazo hizi kwa jina la *Tanzania shillings* kiasi milioni 913,874,631.00. Na fedha nyengine ambazo inadaiwa vile vile kwa *Tanzania shillings* 349,538,845.00.

Kwa hiyo, utakuta fedha hizi kama ingekuwa huyu kampuni ya *MECCO* amelipwa na Serikali fedha hizi ingeweza kumtosheleza kujenga barabara yake ya Konde, Gando pamoja na ile ya Chake Chake, lakini bahati mbaya fedha hizi mpaka leo bado hazijapatikana. *Please, Minister for Finance, I am arguing you, I am requesting you,* nakuomba Mhe. Waziri wa Fedha suala hili ulitizame kwa umakini, muda ni mrefu, sasa hivi ni miaka mitano barabara hizi bado hazijakamilika. Na kwa sababu hiyo ningekuomba Mheshimiwa ili hii kampuni iweze kuifanya hii kazi ilipeni hizo fedha zake *US dollars* anazozidai na hizo nyengine *Tanzania shillings* anazozidai ili harakati za kazi ziweze kuendelea.

Mhe. Spika, naomba deni hili likamilishwe sasa ni miaka mitano. Je, unawaambia nini Mhe. Waziri wananchi wa Konde, wananchi wa Wete na wananchi wa Chake Chake kuhusu barabara tatu hizi kwamba mpaka leo bado zimeshindwa kuleta mafanikio. Haidhuru kidogo kidogo zinaanza lakini *speed* ya kuanza kwake ni ndogo na kuonesha kwamba anaweza akaanguka njiani asiweze kukamilisha kutokana na fedha. Kwa hiyo alipwe fedha zake ili aweze kumaliza kazi hiyo.

Mhe. Spika, jambo la pili ambalo nataka kulizungumza nilisema mmoja katika miradi ya Serikali ambayo inaipa *headache* nchi yetu kwa ujenzi mbali mbali lakini haifikii mahala. Na la pili nataka nizungumze mradi wa pili ni mradi wa wananchi. Mambo ambayo wanayoweza kuchangia katika uchumi wa Zanzibar, na hayo ni muhimu na nataka Mhe. Waziri ayazingatie kweli kweli.

Moja katika hilo linasema uchumi wa Zanzibar unategemea zaidi juu ya utalii. Utalii tunao ambao utalii huu maana yake ni mahoteli tuliyonayo. Lakini la pili ambalo linasaidia katika uchumi wetu wa Zanzibar ni suala la kilimo, bado kilimo hakijaimarishwa sawasawa na ndani yake tukizungumzia kilimo ina maana mifugo imo humo, misitu imo humo pamoja na miti yenyewe; mikarafuu ambayo ilikuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya Zanzibar ambayo nalo pia limekufa. Na uvuvi ambao ni mmoja katika msaada unaoleta uchumi wetu. Na jengine kuna biashara, lakini biashara siitii sana katika hesabu kwa sababu biashara za Zanzibar ni kutoa huduma tu hakuna zaidi, mapato yake ni madogo.

Lakini kuna mambo mengine ya uzalishaji wa ndani. Kwa mfano uzalishaji wa ndani unakuwa ni chakula pamoja na mboga mboga, na vyengine ni viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya nchi yetu. Kwa hiyo, utalii, kilimo, uvuvi, biashara, uzalishaji wa ndani pamoja na viwanda vidogo vidogo hivi ukivitia katika hesabu ni sababu kubwa za kuongeza uchumi wetu wa Zanzibar.

Lakini hata hivyo, tuone kwamba jinsi gani Serikali inashindwa kuendeleza miradi yote, miradi iliyokuwa wazi wazi inaonekana na miradi ya wananchi ni kutokana na kwamba makusanyo yetu ambayo yanakusanywa na *ZRB* na watu wengine wanaokusanya mapato. Mapato hayo yanaweza kusaidia katika suala zima la kulipa mishahara pamoja na *other charges* za Mawizara yetu. Lakini hakuna fedha nyengine ambazo zinabaki kwa ajili ya kuleta maendeleo, hakuna maendeleo ya kutosha kwa sababu fedha tunazokusanya ni kidogo sana hazitoshelezi.

Lakini niende zaidi ndani ni kusema kwamba utalii wetu ndio unaosaidia kuchangia mapato ya nchi yetu kutokana na mahoteli. Makusanyo yanayokusanywa hayakamiliki sawasawa, baadhi ya makusanyo yanapatikana na mengine yanavuja hayapatikani sawasawa katika mahoteli haya.

Jambo jengine katika masuala ya utalii niseme tu kwamba watalii idadi yao isije ikapungua. Kuna Mheshimiwa mmoja alizungumza hapa mategemeo yetu baada ya miaka tutakapofikia 2015 iwe watalii kadhaa ambao wameshakuja nchini. Lakini sasa na mimi nataka kutoa sababu ambazo huu utalii unaweza ukashindwa, unaweza ukasita kwa haya yafuatayo ambayo nitakayoyazungumza. Unaweza ukaanguka utalii na tukakosa uchumi, tukakosa mapato pindipo mambo haya yatajitokeza. Kwa mfano ikiwa kuna matendo ambayo yanafanywa na wananchi wetu kwa kuwatilia moto watu wetu moja itakuwa sababu kubwa hiyo.

Pia, wizi ambao utaingia katika maeneo hayo hiyo itakuwa ni moja katika sababu kubwa. Uvamizi katika maeneo hayo ni moja katika sababu kubwa ya kuwa watalii wanaweza wakakimbia. Jambo jengine uhalifu kama utatokezea katika maeneo hayo pia itakuwa ni hatari. Na jengine ambalo linatokezea kila siku suala la wanasiasa kujitokeza na kauli ya ugaidi. Hii nataka Mhe. Waziri, aliizungumzia kauli kama hizi ni mbaya na vitendo kama hivyo ni vibaya. Kwa sababu vitendo kama hivi vikizungumzwa hadharani au vikizungumzwa katika *TV* na redio zetu kusema kwamba Zanzibar nayo ni moja katika nchi ya ugaidi tujue kwamba tayari tumejitia katika hali mbaya ya kukosa mapato ya Zanzibar. Kwa sababu watalii wakisikia masuala haya uchumi unaanza kuanguka na watalii wanaanza kukimbia.

Nitoe mfano tu kuonesha kwamba mambo haya niliyoyataja ni mabaya, tuchukulie kwa mfano nchi ya Kenya. Nchi ya Kenya Wamarekani na Waingereza wamewasitisha watu wao kuingia katika nchi za Kenya. Kwa nini wamewazuia, kwa sababu ya mambo yanayojitokeza katika nchi ya Kenya ya ugaidi ambao unatokezea wa kuuwawa kwa watu mara kwa mara. Haya ni mambo ya uvamizi wa watu na ugaidi katika nchi ile. Kwa sababu ukisema neno la ugaidi mtalii haingii tena katika nchi.

Kwa hiyo, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba suala hili la kauli hizi ndogo ndogo wanasiasa tujaribu kupunguza mambo kama haya, tusitamke mambo kama haya tunaharibu uchumi wa Zanzibar. Wakisikia watalii kuna mambo kama haya wanaanza kuondoka kidogo kidogo na uchumi wetu unaanguka. Ili utalii udumu Mhe. Spika, hakuna namna yoyote ila pawe na amani, pawe na utulivu ambao utakaoleta uchumi wetu mzuri. Kama amani na utulivu katika maeneo yetu haya hayapatikani basi utalii utaanguka na uchumi wetu utaanguka.

Jambo jengine Mhe. Spika, katika haya haya ambayo yanayochangia katika uchumi wetu ulioshindikana ni suala zima la rasilimali yetu ya bahari. Kwa hiyo, katika bahari yetu kuna mambo mengi ambayo tunaweza kupata. Nchi za jirani ambazo zilizokuwa karibu niweze kutoa mfano wa nchi mbili Singapore pamoja na Mauritius; hizi ni nchi ambazo zimepiga hatua kubwa sana. Katika kupata uhuru wetu hatukuachana mbali, 1961 kwa 1963. Kwa hiyo, kwa nini ikawa nchi ya Singapore, kwa nini nchi kama Mauritius imeweza kupiga hatua sana ya maendeleo, hata pato la mwananchi wa Mauritius na pato la mwananchi wa Zanzibar lipo tofauti kabisa, wametutupa mbali kabisa, wapo katika 10,000 wanayopata pato la mwananchi, wakati sisi bado nimezungumza hapa na Waziri pato letu lipo chini sana. Wakati visiwa tumepata uhuru pamoja, ukubwa wa visiwa bora visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vikubwa kuliko baadhi ya visiwa vyao. Sasa hayo ni mambo ya kushangaza.

Mhe. Spika, nashukuru kwa haya niliyokwisha kutoa. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima nikiwa na wenzangu pamoja leo hii kutoa mchango mfupi sana kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mipango na Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, nimekuwa nikisema mara nyingi kwamba kusema umeunga mkono sio kazi ngumu, ni kazi rahisi na ni kazi laini, lakini cha msingi uwe na sababu ya kuunga mkono hoja iliyopo mezani.

Mhe. Spika, kwanza naomba Mhe. Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha watuweke sawa. Ni nani yupo sahihi kwenye makusanyo ya mapato ya ndani. Mhe. Waziri wa Fedha kwenye kitabu chake cha hotuba ukurasa wa 8 *paragraph* ya 59 anasema kwamba mapato ya ndani yatakuwa bilioni 305.8 lakini Mhe. Waziri wa Mipango ukurasa wa 6 *paragraph* ya 5.1 anasema mapato ya ndani ni bilioni 384.2 tofauti ya bilioni 18.4. Kwa hiyo, mmojawapo itakuwa alipotea pengine alikuwa hana muda alikuwa Dodoma. Na mimi kama Mwakilishi naweza kukubali hotuba ya Waziri wa Fedha kwa sababu ndio mwenye dhamana ya haya mapato na matumizi.

Kwa hiyo, ni nani mwenye usahihi kwa sababu kuna tofauti ya bilioni 18.4 katika hotuba ya Waziri wa Mipango na hotuba ya Waziri wa Fedha. Kwa hiyo naomba watuweke sawa nani tumfuate katika hilo jambo ambalo linazungumzwa kwenye hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi sikubaliani uchumi wa Zanzibar kwamba upo juu, kwamba pato la taifa, pato la mtu binafsi na kusema Zanzibar kwamba unapanda. Ni mahesabu tu ambayo yamewekwa na kwa hali ya kawaida wenzetu walivyo wataalamu mahesabu haya wakiyapangapanga kila mtu anaweza akaona kwamba kesho itakuwa pepo Zanzibar; lakini hakuna kilichoongezeka zaidi ya kupungua.

Na viashiria vya kuongezeka kwa uchumi ni pamoja na mapato na maslahi ya wananchi wetu. Kwa mfano Serikali imekiri hapa kwamba haina mpango wa kuongeza mishahara, bado wanaendelea kufanya mapitio ile mishahara ya watu ambao hawajafanikiwa kuongezwa. Lakini wameshindwa kutwambia kwamba mwaka jana walitutengea bilioni 17 mishahara wameongeza ngapi na zimebakia ngapi na nani waliofaidika.

Kwa hiyo, ikiwa Serikali haina mpango wa kuwaongeza mishahara wafanyakazi wake ni dhahiri kwamba hakuna mapato yaliyoongezeka bali ni usanii wa nambari ambao kwa mtu wa kawaida aliyekuwa si mtaalamu wa hesabu anaona kwamba uchumi umekua kwa hali ya juu. Mhe. Spika, hiki ni kiini macho cha mahesabu ambacho hakina uhalisia.

Mhe. Spika, mara hii Bajeti ya Zanzibar ni bilioni 707.8 ikiwa na ongezeko la asilimia 7.5. Mhe. Spika, kama uchumi wetu umepanda kiasi hicho, kama bajeti yetu imepanda kiasi hicho, tungeona utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya bajeti iliyopita ndio kigezo kikubwa.

Kwa hiyo, unapandisha namba ya bajeti mpya lakini nyuma hukufanya lolote kwa kisingizio kwamba wahisani walichelewa kutoa pesa, mradi wa Mjini Magharibi ule wa Manispaa ulichelewa, *Airport* ilichelewa mfano kwamba hili jambo ni la jana.

Mradi wa *Airport* ni mradi wa zaidi ya miaka saba nyuma lakini kisingizio kwenye bajeti hii kwamba kwa sababu fedha zilichelewa mradi ulichelewa, kwa hiyo fedha za maendeleo zilichelewa. Mhe. Spika, mahesabu haya si mahesabu halisia na kwamba bado nasisitiza kwamba uchumi wa Zanzibar upo hali ngumu, na mapato ya Zanzibar yapo hali ngumu, na si kwa sababu hatuna vyanzo vya mapato. Vyanzo vipo lakini bado hatujaamua kuvitafuta na kuvisimamia.

Mhe. Spika, mimi naomba nitoe kimoja, *GBS* ambayo Mhe. Waziri amekuwa akizungumza tangu mwaka jana kwamba Zanzibar tulitegemea kupata bilioni 40 za *GBS* sio sahihi. Mhe. Spika, naomba nimnukuu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais wa Muungano Mhe. Samiya Suluhu Hassan alisema kwamba misaada ya kibajeti ni 1.163 *trillion*, hii ukiigawa kwa 4.5 ya mgao wa *GBS* maana yake Zanzibar ingepata bilioni 52.34, Serikali wanatwambia wangetegemea kupata bilioni 40. Hizi 12 ziko wapi, nani kala, nani anazihifadhi, nani anazichukua.

Kama Waziri mwenyewe wa Muungano anakiri kwamba *GBS* ni 1.3 *trillion*, 4.5% maana yake ni *52 billion.* Kwa hiyo, ni mapato ambayo hatuambiwi ukweli, lakini Waziri wa Fedha wa Muungano anatwambia vyengine, anatwambia kwamba misaada ya kibajeti Tanzania ipo juu na kwa mahesabu ya Tanzania Bara ya Muungano mara hii Zanzibar ingepata 44.56 *billions* ya *GBS*, Waziri wa Fedha anatwambia ni bilioni 40. Hii 4.5 iko wapi.

Mhe. Spika, nikisema kwamba mwaka jana Zanzibar na mwaka huu kwa jumla walipoteza 25.14 *billions* ya *GBS*. Je, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame haya hayajui. Je, kaka yangu mpendwa Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee haya hayajui. Nani anayezuia haki yetu ya *GBS.*

Mhe. Spika, napata mashaka ama atwambie ukweli au kuna watu fedha hizi wanazichukua wanagawana watu wachache. Misaada ya nje inapokuja iko wazi kwa nini tukose mapato yetu haya ya bilioni 52 ya miaka miwili na bado Serikali inyamaze kimya watwambie bilioni 40. Mhe. Spika, hiki ni chanzo muhimu sana cha mapato na Wazanzibari wanakosa kwa nini na Serikali wanaona ukweli ulivyo.

Mhe. Spika, Zanzibar wanapata 4.5 ya asilimia ya *GBS* pamoja na mikopo. Maana yake Tanzania Bara au Muungano wanapata asilimia 95.5 ya mikopo na misaada ya nje. Lakini msamaha ukija maana yake Wazanzibari wanasamehewa 4.5% ya msamaha, Muungano wanasamehewa 95.5% ya msamaha. Kwa hiyo *automatically* maendeleo ya wenzetu yatakuwa makubwa.

Kwa hiyo, niseme mimi nimesamehewa shilingi 4 mwenzangu amesamehewa shilingi 95 maana yake yeye anaendelea. SMZ mnaliona hili hamsemi kitu, mtu anasema tu tumesamehewa msamaha lakini ngapi ni asilimia 4.5, mwenzio amesamehewa 95.5 maana yake yeye amejenga nyumba kubwa wewe kijumba kidugu umesamehewa. Nani asiyeona hizo hesabu Mhe. Spika.

Kwa hiyo, haya ndio Wazanzibari wengi wanazungumzia kwamba Zanzibar kwa kweli ipo hali ngumu kiuchumi. Lakini Mhe. Spika, nataka nitoe ushahidi wa uwazi, tunaweza kusema hapa kwamba Zanzibar inauliwa kwa

makusudi. Yadi moja ya tetroni Zanzibar ushuru wake ni 0.2 *dollar,* yadi hiyo hiyo ya tetroni Tanzania Bara ni 0.08 *dollar.* Kwa maana gani, mfanyabiashara wa Zanzibar kwenye kontena la futi 40 analipia milioni 60. Lakini Bara ni milioni 28. Ni mjinga gani mfanyabiashara wa Zanzibar atafanya Bara? Kaka yangu kasema anajua, kuweka mipango unajua lakini tatizo nini.

Mhe. Spika, tarehe 5 ya juzi na ninaomba maafisa wa *TRA* wanikosoe. *TRA* Bara wameyazuia makontena 25 kuja Zanzibar; huu hapa ushahidi. Kisa nini. *Destination* ya mwisho wamesema Zanzibar makontena yanatoka China yakapitia Tanzania Bara, wakasema yateremsheni hapa kwa nguvu. (*Makofi*)

Hapa Zanzibar. Maana yake nini wamekosa *TRA* tarehe 5 kuingiza milioni 240, siku moja. Je, mwezi mmoja? Je, mwaka mmoja. Hii miaka 50 ya Muungano. Ushahidi huu. Wote hawa wanaofanya kazi Zanzibar, wafanyabiashara wa Zanzibar, kuna wengine ni wana CCM wakubwa lakini wanalia waende wapi? (*Makofi*)

Mhe. Spika, hatuwezi kwenda. Nani anatubana, hauhusiki muungano, hakuna anayeukataa muungano, lakini watu wanatetea maslahi ya nchi. Mhe. Waziri wa Fedha atwambie kwa nini makontena haya yamezuiliwa na *TRA* Zanzibar imekosa milioni zaidi ya 200 kwa siku moja ya kodi ambayo makontena yanaingia. Mhe. Spika, ninaomba tuambiwe tatizo nini.

Mhe. Spika, lakini hoja za Waziri wa Mipango anatwambia kwamba kuna ongezeko la watu. Sisi tunajiuliza watu hawa wamezaliwa au wanaingia. Mimi nina-*challenge* mutwambie wamezaliwa wangapi hawa kwa siku na wangapi wanaingia hapa kwa siku. Kila siku Wazanzibari wanazaliwa, Mzanzibari anayeingia kwa maslahi ya Hija, Jaku, Hassan. Na ndio maana *operation* ya kuondosha wageni Zanzibar haikuja. Wameondoshwa Kigoma, Mtwara, Lindi. Zanzibar waachieni bwana, wanahitajika Zanzibar. Hatufiki!

Kwa hivyo, *population* ile ya ongezeko hili si la wazaliwa ni ya wageni. Watu wanachukua ajira, mahoteli, viwanda hapana, maana yake watapewa ajira kwa maslahi yao.

Mhe. Spika, lakini mfano mwengine wa Waziri wa Fedha. *TIRA* ni *regulator* wa Bima Tanzania. Alikuja hapa mbele ya Kamati ya Mhe. Salmin Awadh Salmin shahidi, wakasema kwamba hakuna ruhusa kwa Shirika la Bima kuingiza kodi bila ya kiwango cha *TIRA* na wakapanga gari kama *carry* bima yake ni shilingi 200000. Niambeni *Zanzibar Insurance Corporation (ZIC*) imesajili gari ngapi za *carry*. Hakuna hata gari moja. Kwa nini? *Carry* Zanzibar ni nyingi. Mtu wa *carry* atoe 200000 kwa ajili ya bima ya gari yake. Ameshindwa lakini Kampuni ya *Jubilee Insurance* wameweka kiwango cha 100000 na ushahidi ninao wameachiwa. Kumbe *TIRA* kwa Zanzibar tu? (*Makofi*)

Zanzibar wameambiwa hakuna ruhusa ya kuchukua chini ya 200000, wanaheshimu maamuzi ya *TIRA*. Jubilee wanatoa shilingi 100000 *carry* zote zipo Jubilee. Waziri wa Fedha anajua, Mipango anajua, SMZ munajua. Halafu mutwambie bwana mashirika haya hayachangii bajeti ndogo...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, una dakika 5 kumaliza hotuba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nitoe hoja; iwapo kweli Wawakilishi wetu wapo makini kwa ajili ya watu wa Zanzibar, uturuhusu tusiunde Kamati Teule, lakini tuunde timu ya wataalamu humu ndani ya Baraza tuwafuate mawaziri tuchunguze haraka. Kwa nini *Zanzibar Insurance Corporation* wamezuiliwa kutoza Bima ya chini ya shilingi 200000 na *Jubilee Insurance* wakatoza chini ya 100000. Nani katoa nguvu hiyo? (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini pili tuunde kamati kwa nini mapato ya Jubilee Zanzibar hayaji na serikali wanajua wanayafumbia macho. Je, huu si mradi wa mtu? Mhe. Spika, ninasema hayo kwa ushahidi wa chombo cha *TIRA* na ushahidi wa bei za *TIRA* kwamba hakuna ruhusa ya kuweka bei chini ya kiwango cha *TIRA*. Kwa nini Jubilee karuhusiwa kuweka chini ya bei. Maana yake nini. Maana yake *ZIC* ni Zanzibar na Jubilee inatoka Tanzania Bara, ndio yale yale mtu anakuja hapa soko lipo kubwa, mwisho Mhe. Spika, mpaka *stickers* za Bima wao wanaambiwa toeni nembo na jina, *TIRA* itapitisha. *ZIC* haina ruhusa ya kuchapisha *stickers*, wanazichapisha Bara baadae wanazinunua. Na ninao ushahidi vile vile kwamba kwa mwaka *ZIC* wanalipia asilimia 20 ya mapato yake kwa *TIRA*.

Leo munalaumu hawa maana yake mchango mdogo, shirika la magari limekufa. Mhe. Ahmed Mazrui huyo analiachia. *ZSTC* tayari inakwenda zake, Bima tayari inakwenda zake, lakini mwisho *PBZ*, sishangai sana Mhe.

Spika, Waziri mmoja alipokuwa Waziri wa Fedha alitoa wazo kwamba *PBZ* iuzwe. Kwa hivyo kama Waziri alitoa wazo kwamba *PBZ* iuzwe, sasa mimi sishangai kwamba twende hivi. Lakini walipoachiwa *PBZ* leo wapo mbali sana. Yaachieni mashirika yetu yafanye kazi kwa mujibu wa viwango vyao na taaluma na uwezo wao.

Mhe. Spika, hii ni bajeti ya maajabu na haina uhalisia na wananchi wasitegemee, wasubiri mwakani waje waangalie mnara pale Kisonge itakuwa ni kwa faida yetu.

Mhe. Spika, ninashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hija Hassan Hija. Nimkaribishe basi Mhe. Farida Amour Mohammed afuate, baadae Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Omar Ali Shehe alijitayarishe.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache niliyonayo.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijiaalia uzima na afya njema kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hili kwa siku ya leo. Pia, niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa jinsi walivyosoma hotuba zao na zimefahamika vizuri.

Mhe. Spika, katika hotuba ya mipango ya bajeti imetaja katika kifungu cha 16 (4) ukurasa wa 12 kwamba watalii wameongezeka kutoka 169 hadi 263 mwaka 2012 hadi kufikia watalii 185,301 mwaka 2013.

Mhe. Spika, takwimu hii ya watalii imenitia wasi wasi mkubwa, kwa sababu niliwahi kusoma takwimu iliyokusanywa na taasisi za takwimu za Tanzania Bara kwamba watalii wanaotembelea Zanzibar ni zaidi ya 400000.

Mhe. Spika, lakini leo hii takwimu ya watalii tuliyoambiwa hapa kwa miaka hii miwili ya 2012/2013 kiwango kilichoongezeka ni hichi. Naomba niulize swali. Takwimu zinazokusanywa hapa Zanzibar zina ukweli gani, kwa sababu vyombo vinavyokusanya watalii Zanzibar vinaficha ukweli. Sasa sijui kwa nini vinaficha ukweli huo wa kutupa takwimu zilizo sahihi. Lakini wasi wasi ni kwamba wanaficha ukweli huo kwa sababu ya kujinufaisha wao binafsi.

Mhe. Spika, sasa hilo ni tatizo. Mhe. Spika, pia niliwahi kusoma takwimu zinazokusanywa na taasisi zetu zinazochukua *data* mbali mbali zinatofautiana. Sasa pia hili ni tatizo la uvujaji wa mapato. Tegemeo letu kubwa la vyanzo vyetu vya mapato na utalii pia tunategemea sana. Lakini ukiangalia takwimu za watalii wanaoingia hapa Zanzibar ni wengi lakini mapato tunayoyapata ni madogo.

Mhe. Spika, sasa naomba niulize kwa nini serikali inafuta sera za zamani za kukusanya mapato. Ni lini serikali itaweka mashine za kisasa za kuchukua takwimu za watalii wanaoingia nchini, na lini serikali itaweka mashine za kukusanya kodi za mahoteli jambo ambalo litasaidia kukusanya mapato yetu ya serikali.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 13 *paragraph* ya 17 kitabu cha mipango kimesema kwamba wastani wa pato la kila mtu limekua na kufikia dola 66 na 67.

Mhe. Spika, serikali katika kujinasibu kwa maendeleo lazima iangalie nchi tunazofanana nazo ijilinganishe. Zanzibar na Mauritius ni nchi zenye kulingana; na kwa taarifa nilizonazo wakati tunapata uhuru miaka 1960, nchi hizi zilizokuwa kwenye bahari ya Hindi zilikuwa na kiwango sawa cha mapato ya kila mtu.

Mhe. Spika, swali la nchi ya Zanzibar kuwa mpaka sasa haijafikia hata dola 700 kwa pato la mtu. Hili suala ni la kutisha kwa sababu wenzetu wa Mauritius nao ni visiwa kama sisi, na tulikuwa tunalingana na mapato yetu yalikuwa sawa, pia wao walikuwa na uchumi mdogo, uchumi wao ulikuwa ni wa miwa lakini sisi tulikuwa na uchumi wa karafuu tokea miaka hiyo; na karafuu ni mali, lakini mpaka leo sisi miaka 50 hii, wastani wa pato la kila mtu halijafikia dola 700, wakati wenzetu sasa hivi wameshafikia dola 10,000.

Mhe. Spika, hivyo, naomba niulize. Ni kitu gani hasa kilichotusibu Zanzibar ikawa mpaka hii leo sisi bado tunajikongoja tu hatusogei mbele bado tunarudi nyuma. Hivi tatizo letu sisi ni ubovu wa sera zetu, ni ubovu wa ilani

zetu, au tuseme ni hii kabari tuliyotiwa na wenzetu ya Muungano ndio maana ikawa sisi hatufiki mbele na sisi wenyewe tunakaa kimya tu.

Mhe. Spika, hili ni tatizo lazima tulifuatilie na ninamuomba Mhe. Waziri katika hili atupe maelezo ya kina, kwa nini miaka 50 sisi bado Zanzibar tunaendelea kujikongoja wakati na idadi ya watu wetu pia nayo sio kubwa ukilinganisha na wenzetu na nchi nyengine tulizofanana na sisi.

Mhe. Spika, katika *paragraph* ya 73 ukurasa wa 52 wa kitabu cha mipango iliyosomwa na Waziri wa Nchi (OR) Ikulu ameendelea tena na mradi wa barabara ya Wete/Gando. Mhe. Spika, hili linanisikitisha, tena linanisikitisha kwa dhati kabisa.

Mhe. Spika, hivi serikali itaendelea mpaka lini kuwadhalilisha wananchi hawa. Barabara hizi za Wete/Gando na Wete/Konde ni barabara ambazo zinapata miaka saba mwenzangu aliyetangulia kusema Mhe. Suleiman Hemed Khamis alilizungumzia hili, lakini kibaya zaidi katika barabara hizi wananchi wanaathirika mno.

Sasa hivi kama hizi barabara zitamalizika, maana nina wasi wasi mkubwa sana wa barabara hii kama zitamalizika, lakini kama zitamalizika basi wananchi wetu wa maeneo hayo wengi wanaathirika na maradhi ya mapafu kwa sababu ya vumbi.

Mhe. Spika, ninasema hivyo kwa sababu mkandarasi aliweka fusi ndani ya barabara zile kisha akasita kufanya kazi. Magari yanapopita yanatoa vumbi jingi na kuathiri wananchi wetu, wanaathiri kwa maradhi na pia wamewawanyima hata kufanya biashara zao ndogo ndogo hasa wanawake.

Mhe. Spika, sasa ninavyohisi na ndivyo ilivyo serikali ina udhaifu wa utendaji na utekelekezaji wa miradi yake kwa sababu miradi hii sio ya leo, miradi hii ni ya muda mrefu na kila siku inaendelea kutajwa na kutajwa. Hii ni afadhali kama serikali imeshindwa kutekeleza miradi hii ya barabara ya Wete/Gando na Wete/Konde basi naiomba serikali wawalipe hawa wananchi wa maeneo haya fidia ya maafa yaliyojitokezea kwa ajili yao.

Mhe. Spika, kuna fidia za aina mbili; kuna watu waliovunjiwa nyumba zile katika kujenga barabara lakini pia, kuna watu waliokuwa nyumba zao hazikuvunjwa lakini zimetikisika kwa sababu ya magari mazito zimevunjika, nyengine zimepasuka na nyengine zimeanguka kabisa na hazipo zipo chini, wananchi wa maeneo haya wamehama na wamehamia sehemu nyengine na watoto wao wamehifadhiwa na majirani.

Mhe. Spika, hii hali kweli inatisha. Serikali itambue kwamba maafa si kwa sababu ya kuzama meli tu. Moto ni maafa, na haya ya kuvunjikiwa maskini ya Mungu na nyumba yake pia ni maafa. Maafa haya yatakuwa ni ya aina mbili, mbali ya maafa ya kukosa pa kuishi halafu na maradhi pia.

Mhe. Spika, ninaiomba sana serikali katika hili ilisimamie, iwalipe watu fidia zao, wanaweza kusema na mkandarasi wao lakini pia, nina mashaka, hivi huyu mkandarasi huyu ana mahusiano na nani katika serikali hii mpaka leo hii anaachiwa tu anafanya anavyotaka. Inatisha.

Mhe. Spika, mimi nilipokuwa Kamati ya *PAC* tumekwenda pale katika barabara zile za Wete/Gando tukazikagua na waliokuwepo pale walitwambia kwamba bado serikali haijaamua kuwalipa. Sasa serikali haijaamua kuwalipa tokea miaka hiyo na tukaambiwa kama kuna milioni 500 tayari zimeshatengwa kwa ajili ya kuwalipa wale watu fidia. Mpaka leo hii kuna watu bado hawajamaliziwa kulipwa, watu wanaendelea kuathirika na maradhi, watu wanaendelea na kuathirika na dhiki hawana pa kuishi.

Mhe. Spika, ninakuomba sana na ninaiomba sana serikali katika suala hili iwaonee huruma jamani Wazanzibari hasa wale walioko katika kisiwa cha Pemba waliovunjiwa maeneo yao.

Mhe. Spika, katika kitabu cha bajeti cha mipango ya maendeleo nimefurahi sana kuona kwamba serikali ina mpango wa kupeleka umeme kwenye visiwa viwili vidogo vya Kisiwa Panza na Makoongwe. Mhe. Spika, mpango huu ni mzuri sana wa kupatikana nishati hii ya umeme katika maeneo haya. Lakini Waziri anayeshughulikia mipango mara nyingi anataka kwamba utekelezaji wa ilani ya CCM, utekelezaji wa ilani ya CCM. Ninakubaliana naye kwa sababu hii ni utekelezaji wa ilani ya CCM lakini ninaomba niulize swali. Hivyo, katika utekelezaji huu wa ilani ya CCM kuna vigezo gani vilivyotumika kupeleka umeme visiwa hivyo viliopo Kusini kwenye Wilaya ya Mkoani na kwa

nini ilani hii ya CCM isitekelekeze kupeleka nishati hii katika visiwa vya Kisiwa Panza, Ukunjwi vilivyopo Kusini na Kaskazini, ikawa visiwa vyote viwili vimekaa upande mmoja.

Kuna watu wa Fundo nao wana matatizo na wao ni kisiwa hivyo hivyo. Kwa nini hii ilani ya CCM isingetekeleza kwa pande zote mbili, itekeleze katika upande mmoja kwa wakati mmoja au kuna sababu, watwambie wana CCM waliopo Mkoa wa Kaskazini kama ilani ya CCM haitekelezeki kwa upande wao.

Mhe. Spika, katika kutekeleza ilani za Chama cha Mapinduzi ambazo kuwa kiongozi wa nchi anatoka kwenye Chama cha Mapinduzi, lakini kwa vile yeye ni kiongozi wa nchi watu wote waliomo ndani ya nchi hii ni watu wake. Kwa hivyo, Tume ya Mipango, ninaomba Waziri unayefuatilia masuala haya unapofanya chochote kile, basi ukifanye kwa mgao unaokubalika katika huku na huku, kama ni kidogo tugawane hivyo hivyo kidogo kidogo. Tufuate maneno ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliyosema kwamba, "Bora kuwa na chakula kidogo tukagawana kidogo kidogo kuliko kuwa na chakula kingi tukaanza kukigombea".

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninakuomba sana, tena ninakuomba kwa nia safi, mpango wako huu uufanye katika mgawanyo unaokubalika, Kaskazini visiwa vipo na Kusini visiwa vipo. Hatuna choyo lakini roho inauma wakati mwengine na Kaskazini pia watu wanataka kupata nishati hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema hivi, wafanyakazi wanapomaliza muda wao kufanya kazi wa wizara zote basi wanategemea mafao yao jinsi wenyewe watakavyotaka kujiendesha na maisha yao. Lakini kinachosikitisha watu wanamaliza muda wao kufanya kazi, wanapeleka barua zao katika taasisi zinazohusika, lakini mtu anakaa mpaka mtu anajisahau na kupoteza yale malengo yake hajapewa yale mafao, yaani kiinua mgongo.

Mhe. Spika, sasa hapa ninaomba niulize Wizara ya Fedha, je, mtu anatakiwa au kuna vigezo gani mtu akae muda gani baada ya kumaliza na kuchukua likizo yake na kupata mafao yake, ni muda gani, na kwa nini munawacheleweshea watu mafao yao.

Mhe. Spika, kuna mambo tunakwenda mbele lakini lazima turudi na nyuma. Kulikuwa na walimu fulani walisomesha miaka mingi tu lakini kwa bahati mbaya mpaka juzi kwenye kamati yetu ya Wizara ya Elimu, walimu wale 40 wa Unguja na Pemba hawajapewa mafao yao, wale walimu waliosomesha wala wanafunzi.

Kwa maelezo ya Wizara ya Elimu ilikuwa taarifa zao zote tayari wameshazipeleka, wameshafanikisha kila kitu lakini bado sijui wizara gani iliyokuwa inalisimamia hili iliyokuwa mpaka sasa hivi inawacheweleshea watu wale haki zao ambao wengi wao ni wanawake.

Mhe. Spika, ninaiomba sana serikali walimu wale 40 wa Unguja na Pemba waliopatiwa mafunzo yale na waliotoa mafunzo, basi muwalipe haki zao haraka iwezekanavyo na wao wajione kama tayari wana haki ndani ya serikali hii. Nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Nimkaribishe basi Mhe. Rufai Said Rufai, wakati Mhe. Omar Ali Shehe anajitayarisha.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru *Allah* asubuhi ya leo na mimi nikapata nafasi hii adhimu kuweza kutoa mchango wangu juu ya hoja hizi mbili zilizo mbele yetu.

La pili, nisiwe mpungufu wa fadhila kukosa kukushukuru wewe kuweza kunipa nafasi hii na mimi nikatowa mchango wangu.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu wa bajeti ya hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, nitaanza ukurasa wa 43 kifungu cha 56 pale, kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, ujenzi huu wa bandari hii ya Mpigaduri imekuwa ni hadithi simulizi na bahati mbaya nimejaribu kutafuta maelezo ya ziada katika mapitio halali ya uchumi 2013 na kitabu hiki cha pili, lakini maelezo kiurefu sikuyapata. Katika kitabu cha Mhe. Waziri maelezo yake pia ya bandari hii hayatoshelezi ni mafupi mno. Naomba Mhe. Spika, niyakariri haya maneno kidogo kwa ruhusa yako.

Mhe. Waziri amesema, kifungu 56, ukurasa 43;

"...upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara zinazoingia mjini za Fuoni na Bububu yamekamilika kwa mapitio ya upembuzi yakinifu kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri yanaendelea". hayo ndio maneno kwisha kabisa.

Mhe. Spika, sisi wengine tulipoingia katika Baraza hili mwaka 2010 mwishoni taarifa hizi tulizipokea, zipo. Mwaka jana taarifa hizi zilizungumzwa vizuri, lakini mwaka huu zimekosa muelekeo.

Mhe. Spika, tukiangalia gati yetu ile pale Malindi. Kwa kweli uwezo wa kubeba mzigo iliyokuja pale imekuwa ni mdogo mno. Bandari yenyewe umri wake pia umeshakuwa dhaifu ni nzito sana, vitendea kazi vimekuwa ni tatizo. Mizigo inachelewa na kuchelewa kwa mizigo pale bandarini ni kuwaongezea ushuru wananchi wetu wanaoleta mizigo ile.

Mhe. Spika, sasa hii gati ya Mpigaduri kwa kweli ina umuhimu wake. Mimi naamini kwamba kama gati hii serikali itawacha ile chelewesha chelewesha ile ikaona kwamba ni njia moja ya kuweza kunyanyua uchumi wa Zanzibar, basi mimi naamini tutapiga hatua kubwa ya uchumi. Lakini hii ngoja ngoja Waswahili wanasema, "ngoja ngoja huumiza matumbo".

Tumesikia wenzetu walikuwa na mpango wa kujenga gati kubwa ya kimataifa Mkoa wa Pwani. Kama taarifa zile zilifanikisha, mimi naamini Zanzibar tungeanguka sana kibiashara katika kwa kupitia haza gati. Lakini kwa tunavyosikia kwamba ule mpango ume-*fail*, lakini tusifikiri ku-*fail* kwao, hilo halitotiwa katika fikra nyengine ili kuwezesha mpango mwingine wowote ule. Ningeiomba sana serikali katika hili iharakishe hili gati liweze kujengwa ili serikali iweze kuingiza mapato kwa wingi.

Mimi naamini kwamba serikali inahitaji mapato, kwa sababu serikali yoyote ile ikiwa haina mapato, hiyo serikali itakuwa dhaifu. Kwa hivyo, njia pekee ambayo tutawapunguzia wananchi wetu kodi ya kila siku basi nyezo kama hizi zinaweza kuisaidia serikali ili kuibuka katika mapato yake na kuondoka katika uchumi dhaifu.

Mhe. Spika, kuwa na gati kama hii ambayo tunaambiwa kwamba Zanzibar tuko katikati ya Afrika. Kwa hivyo, nchi nyingi zinaweza kama tutakuwa na gati ya kisasa kufikisha mizigo yao hapa na itakuwa ni rahisi kupeleka katika nchi zao. Lakini bado tumelemaa tu hatuliharakishi hili. Sasa kulemaa lemaa kwetu huku ndio tukawa sisi hatupigi hatua kwenda mbele ya maendeleo. Kwa hivyo, masuala kama haya ya gati ni masuala muhimu ya nchi kufanya vyovyote vinavyowezekana, lakini tukaondokana na umaskini huu wa kujitakia.

Mhe. Spika, nije katika uwanja wa ndege wa Pemba. Nashukuru kwamba Mhe. Waziri katika hotuba yake ameutaja huu uwanja, na mwaka jana tulitajiwa na mwaka huu imetajwa na mwaka juzi ulitajwa. Lakini matajo haya na tunaambiwa yanaendelea tu, mazungumzo yanaendelea, mazungumzoa yanaendelea na ndio desturi ya mazungumzo, kila siku midogo inasema. Lakini namuomba Mhe. Waziri aje atueleze mazungumzo haya yamefikia hatua gani, kwa sababu miaka mingi tunaelezwa habari hizi. Hebu Mhe. Waziri tueleze haya mazungumzo yenu na hawa Waturuki yamefikia hatua gani. Kuna hatua mbili, kuna hatua za mafanikio na kuna hatua zilizokuwa si za mafanikio, lakini wananchi watajua uwanja huu umefikia katika hatua gani.

Mhe. Spika, niseme katika viwanja hivi vya ndege cha kimataifa cha Abeid Aman Karume na hiki cha Pemba. Kwa kweli ndani ya viwanja hivi tuna tatizo sugu sana. Kwanza tuna ukosefu wa *X-Ray Machine*, hili limekuwa ni tatizo sugu. Wafanyakazi wetu pale wanatumia mikono yao, saa nyengine hata *gloves* kwenye mikono haina. Watu wanapenyeza mikono ndani ya mizigo ya watu, hili ni tatizo Ndani ya mizigo ya watu, watu wengine wana matatizo yao. Nguo chafu zimo mule mtu anatia mikono hatima yake anapata matatizo, anapata maradhi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kiwanja kama hiki cha Abeid Aman Karume, tunasema ni kiwanja cha *International*. Mhe. Spika, hili ni jina moja kubwa mno. *International Air port*, ni jina moja kubwa kweli kweli. Lakini ukifika wafanyakazi wake wanapekua mizigo ya watu kwa mikono, huu ndio U-*international*, Mheshimiwa hili ni tatizo. Mimi ningeshauri kwamba hili jina la *International* tulibadilishe kwanza mpaka tufikie huo uwezo wa kuwa na kiwanja cha *International*. Lakini unakwenda pale unawakuta wafanyakazi wanapekua mizigo ya watu kwa mikono yao hata *gloves* hawana, Mheshimiwa hili ni tatizo.

Mhe. Spika, na hizi mashine tulizungumza na watu wa uwanja hapa, kwamba tayari Wizara ya Fedha wameshakubaliana kwamba hivi viwanja vinunuliwe. Pengine ahadi aliyotuambia kwamba zitakuwa tayari hapa Unguja zishafika, pengine sina uhakika, lakini ni kitu cha kuharakisha, tunajiwekea sura mbaya ya uwanja kama ule. Kiwanja chetu leo *Alhamdulillah* wageni kila mara wanakuja, lakini wakifika kiwanja cha *International* hapana miundombinu ambayo inakwenda na wakati tulionao, hili ni tatizo.

Mhe. Spika, pia, kuna tatizo kiwanja hiki iko siku kitafungwa, iko siku Mwenyezi Mungu apishe mbali, lakini wageni wanaokuja kunyanyua uchumi wetu hapa basi iko siku kiwanja kitafungwa, kwa sababu hakina miundombinu. Kuna taarifa pale magari ya kuzima moto yamewekwa pale kiyoo tu, hapana linalofanyakazi yote mabovu, hili ni tatizo.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Rais hapa kapata ugeni, anaeshughulikia mambo ya Viwanja vya Ndege kutoka duniani, alikuja akapigwa blaa blaa huyo kenda, lakini matatizo yetu kwa kweli ni sumu. Kwa hivyo, kuendelea na matatizo haya kuyafumbia macho, kuna siku tutakuja kufikwa na tatizo kubwa tushindwe namna gani ya kujieleza. Naiomba sana serikali masuala haya wahakikishe wameyapa kipaumbele na kuyatekeleza kwa haraka. Kwa sababu tumeshaona kwamba wageni wengi wanaoingia Zanzibar wanatumia kiwanja cha ndege.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ndenge zinazokuja hapa nyingi za kimataifa na kuleta wageni, lakini miundombinu yetu ni mibaya. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu aepushie mbali likitokea tukio, serikali itatakiwa kujibu. Kwa hivyo, hatutaki serikali yetu ifikie katika matatizo kama hayo.

Mhe. Spika, jengine niseme kwamba sehemu ya ukurasa wa 34, kifungu cha 45 kuhusu kuimarisha sekta ya utalii. kila siku tunaimba kwamba utalii ni sehemu kubwa ambayo inanyanyua pato la nchi. Hilo ni kweli na tunashukuru kwamba wawekezaji wengi wamehamia Zanzibar na kuweka miradi yao mbali mbali ili kuiwezesha serikali kupata kodi mbali mbali ili kuweza kunyanya uchumi wake, ni jambo zuri, lakini ndani ya uzuri huu kuna walakini.

Mhe. Spika, fukwe zote Kusini hadi Kaskazini karibuni asilimia 90 tayari kuna mahoteli mbali mbali ya wawekezaji. Sasa tujiulize kwa nini tukawa maskini na tayari mahoteli yapo ya kisasa na ya aina yake, lakini mapato hayapatikani tujiulize kwa nini. Je, wakusanyaji kodi hawakusanyi au wenye kujenga mahoteli hayo hawatoi kodi na kama hawatoi kwa nini hawatoi? Hili ni tatizo.

Mhe. Spika, mara nyingi utakuta kodi zetu sana tunazijali sana kwa wananchi wauza dodo, hao ndio tunawakazia nati, lazima dereva alipe kodi zote, mfanyabiashara alipe kodi zote, muuza vitu mbali mbali alipe kodi zote, lakini kwa nini huku kwenye mahoteli kodi hazilipwi.

Mhe. Spika...

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Rufai Said Rufai: Nashukuru. Ukichukua kitabu hiki cha Mdhibiti, ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi na taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya mwaka 2011/12, hapa katika ukurasa wa 78 hadi ukurasa wa 84, *CAG* anasema miradi ambayo imesajiliwa, lakini hailipi kodi ya ardhi, ukurasa wa 78 hadi wa 84, ipo miradi mingi mno, lakini hawalipi kodi, lakini huku anashikwa mwananchi kwa hali yoyote alipe kodi. Miradi hii imekuja hapa kufanya kazi kuinyanyua nchi, lakini tunawafumbia macho, ni nani? Kwa nini wizara zinazohusika na mambo haya, Mhe. Waziri wa Fedha, watu wa *ZRB*, japokuwa tuseme wao ni wakala lakini wao ndio wanaohusika na mambo ya kodi, kwa nini miradi hii ikawa haisimamiwi ikakusanya kodi za nchi, na nchi ikaweza kupata pato, hili ni tatizo Mhe.
Spika.PPPP

Mhe. Spika: Ahsante sana. Nimkaribishe sasa Mhe. Omar Ali Shehe na baadae Mhe. Shadya Mohamme Suleiman.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya mimi kuweza kutoa mchango wangu kuchangia bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Spika, tunajadili bajeti ya mwaka 2014 ikiwa ni mwaka wa nne sasa huu tangu serikali hii ya awamu ya saba kuwepo madarakani.

Mhe. Spika, bajeti ni kipimo kwa wananchi katika kubaini na kupata kigezo juu ya utekelezaji wa sera, katika mipango ya uchumi pamoja na huduma nyengine za kijamii. Bajeti ya mwaka huu 2014/15 Mhe. Spika, kwa tathmini yangu ukichukua mapato ya ndani na nje ya serikali, *vis-a-vis* matumizi ya serikali Mhe. Spika, tumeambiwa kwamba tunatarajia makusanyo ya mapato ya ndani yawe ni 363.7 bilioni, lakini matumizi ya serikali yatakuwa ni 374.7 kwa matumizi ya kazi za kawaida na 348.8, kwa matumizi ya kazi za maendeleo jumla itakuwa ni 705.1 bilioni.

Mhe. Spika, ukiangalia baina ya mapato ya ndani na matumizi na ninasema hivi Mhe. Spika, kwa sababu mapato ya ndani ndio msingi wa uchumi wa nchi. Kwa hivyo, mimi nitakazia kwenye uwezo wa serikali katika kukusanya mapato ya ndani. Ukichukua baina ya matumizi ya serikali na yale mapato ya ndani utaona kwamba bajeti yetu ina nakisi takriban ya asilimia 52. Sasa kwa hali hiyo ni ushahidi tosha kwamba tuna kazi kubwa na tuna tatizo kubwa katika uchumi wa nchi yetu na tuna kazi kubwa kwa uwezo wa serikali katika suala zima la kusimamia na kuendesha suala zima la maendeleo.

Mhe. Spika, kama tukiwa tuna nakisi ya aina hiyo tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba mimi binafsi napata tatizo baina ya takwimu katika suala zima la ukuaji wa uchumi, kwa sababu tunapoambiwa uchumi unakua kwa ailimia 6.7 tafsiri yake ni kwamba tulitaraji kwamba kadiri uchumi unavyoendelea kukua ndivyo mapato nayo ya serikali yaongezeke kwa sababu kukua kwa uchumi tafsiri yake au maana yake ni kuongezeka kwa mapato ya Serikali. Inawezekana kwamba uchumi ikawa unakua lakini mapato hayaongezeki, hapa pana tatizo na tatizo hapo linapoonekana kwamba ama Mhe. Spika, kuna tatizo la kitwakimu kwamba takwimu sio sahihi au kutakuwa na suala zima la uvujaji wa mapato, uvujaji wa mapato ama mapato ya Serikali hayakusanywi.

Kwa hivyo, mimi kiujumla nina tatizo kwenye mambo yote mawili; kwanza nina tatizo kwenye takwimu kwamba takwimu tulizonazo ni takwimu za kughushi na haziowani hazina ulinganifu na uowanifu na uhalisia. Lakini na tatizo jengine ambalo mimi binafsi kama Mwenyekiti wa kamati ya kuchunguza mahesabu ya Serikali nilitoa *challenge* kwa Serikali kwamba kuna tatizo kubwa sana la ukusanyaji wa mapato ndani ya nchi yetu.

Sasa Mhe. Spika, hilo ni tatizo na kwa vyovyote vile sote tunafahamu kwamba iwapo tutaongeza ukusaji wa mapato ya Serikali kwanza Mhe. Spika, tutakuwa na upunguzaji wa utegemezi. Tuliambiwa na viongozi wetu kwamba kutegemea nchi yoyote, taifa lolote kutegemea ni sawa sawa na utumwa, ni sawa sawa na ukoloni kwa hivyo bado bajeti yetu inaonekana kwamba inategemea zaidi. Mwanzo nilisema kwamba tuna nakisi, na katika nakisi hiyo mjalizo wake utatokana na utegemezi wa mikopo na misaada. Hilo ni tatizo na vyovyote vile tulikuwa tunataraji kadiri siku zinavyoendelea ndivyo kadiri ambavyo Serikali yetu iondokane na suala zima la utegemezi, bado tatizo hilo linaendelea kutuandama.

Sifa ya pili iwapo tutaweza kukusanya mapato ya Serikali Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba tutaongeza bajeti katika sekta ya huduma. Sasa hivi kadiri ya miaka inavyokwenda tumekuwa tukishuhudia kwamba kuna ongezeko la utegemezi katika suala zima la sekta ya huduma. Sekta ya huduma bajeti yake na hivi tunvyozungumza tunazungumza bajeti hii ndio bajeti kuu ya Serikali, hapa ndio pahala hasa pa kuzungumza hatuwezi kuacha kuzungumza hapa tukategemea kuzungumza katika bajeti za kisekta.

Kwenye bajeti za kisekta hakuna kitu huko ni namna ya kupanga tu bei ya pilipili hoho kuondosha hapa ukaweka hapa, huko hakuna kitu ikiwa Serikali haina pesa ndio kusema katika wizara nako kutakuwa hakuna chochote ni kuja kupoteza na ndio maana baadhi ya nchi hasa hujadili bajeti ya Serikali na kuachana na bajeti za kisekta, kwa sababu ukisema hapa huna pesa maana yake na huko kwenye sekta huna cha kujadili.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, tutakosa kuongeza bajeti katika sekta za huduma na tukifanya hivyo Mhe. Spika, tutaendelea miaka yote kuwabebesha wananchi wetu mzigo katika sekta za huduma kama vile afya, maji, elimu na mambo mengine muhimu kama vile umeme ambapo tulitegemea kwamba kadiri miaka inavyokwenda Serikali tujenge ule utamaduni wa kupunguza mzigo kwa wananchi, hilo inaonekana kwamba haliwezekani.

Jambo jengine la tatu Mhe. Spika, ikiwa mapato hatukusanyi maana yake Serikali itashindwa kutoa bajeti ya kutosha katika sekta za uchumi. Mhe. Spika, hatuwezi kujenga uchumi kama hatujaweka fedha nyingi katika sekta za uchumi.

La mwisho Mhe. Spika, ikiwa bajeti ya Serikali na makusanyo ya Serikali yatakuwa madogo basi tutashindwa kuwekeza katika sekta ya uzalishaji, na hapa ndio penye tatizo, tulitaraji kwamba katika sekta hii ya uzalishaji kwa sababu hii ndio sekta inayowagusa wananchi wengi katika suala la uzalishaji bidhaa ndogo ndogo. Katika suala la kutoa mikopo na vitu vyengine kwa kweli hapa tutashindwa, na lile suala tunalosema kwamba tunaongeza kipato cha wananchi itakuwa ni ndoto, hatuwezi tukafikia. Kwa hiyo, mambo yote haya manne niliyoyataja chanzo chake ni kwamba ukusanyaji wa mapato ya Serikali unakuwa ni mdogo kwa mwaka hadi mwaka.

Mhe. Spika, suala la kujiuliza hapa Zanzibar hasa tuna tatizo gani na tunapaswa kujiuliza hivyo kwa sababu kwa fikra zangu Mhe. Spika, ni kwamba hatujaweza kuwa na mipango ya kubaini ni aina gani ya uchumi ambao tutautegemea kama nchi, hili ndio tatizo. Sisi Zanzibar tumekuwa ni watu wa kubabaisha babaisha tu na huu ndio ukweli miaka hamsini tumekuwa bado hatujajikita na kujua kwamba tunahitaji kutegemea uchumi wa aina gani. Hapa natoa mfano miaka ya tisini tulikuja na ile kuwa na uchumi wa maeneo huru na likaelezwa hapa kwamba ni Micheweni na Fumba, hebu leo Serikali ije mbele yetu na itwambie kwamba wamefikia hatua gani katika kuyaendeleza maeneo hayo katika suala zima la kuyafanya maeneo hayo kuwa maeneo huru ya kiuchumi.

Nakumbuka miaka ya 2000 kwa sababu siju kama huu ni mpango wa kunyanyua uchumi, wa kujenga uchumi au huu ni mpango wa *Social reform,* kwa kweli ni kuchanganya mambo ambayo hayajulikani *which is which,* hili ni tatizo kwa hisia zangu. Mkuza nao pia umefeli haukuweza kufikia lile lengo ambalo tumekusudia.

Miaka ya 2010 Mhe. Spika, Serikali ilikuja na mpango wa PPP (*Public Private Partnership)* mimi nakubaliana nao kwamba huu ni mpango sahihi lakini sasa Serikali ije mbele yetu itawambie imefikia wapi katika kuifanya na kuiwezesha sekta binafsi ili ijikite sasa katika kuelekeza uchimi wa nchi yetu serikali, iwe na mpango wa kutwambia huu mpango wa *Private public partnership* umefikia pahala gani, waje watambie kama kuna tatizo la kisera, kuna tatizo la kisheria watwambie. Kwa hivyo, tunahitaji kujua hasa mpango huu umefikia hatua gani, kwa sababu huu ndio mpango takriban nchi zote za dunia sasa hivi Serikali hazijipi jukumu kubwa katika kuwekeza hasa katika sekta za uchumi hutegemea sekta binafsi.

Mhe. Spika, katika miaka hiyo hiyo ya 2010 Serikali ilikuja pia na mpango wa *Aspora* kitu ambacho mimi nakubaliana nancho kwamba na dunia ya sasa imejielekeza zaidi katika kutumia *diaspora* katika kuwekeza uchumi. Ethiopia wenzetu sasa hivi ukienda wana mpango wa miaka mitano wa *reform* na sehemu kubwa ya Ethiopia wanategemea *diaspora*. Sasa hivi Muethiopia popote alipo Duniani mwenye uwezo wake huenda Ethiopia akiambiwa ncho ukitaka ardhi chukua bure, ukitaka mtaji huu hapa hii ndio tunahitaji sasa kujua ule mpango wa *diaspora* kuambiwa kwamba Wazanzibari tuko wengi tunahitaji kujua Serikali imefikia hatua gani katika mpango huo. Na ikifika hatua mpango mpaka kikaanzishwa kitengo katika ofisi ya Rais sasa ni wakati wa kuja kutwambia wamefikia pahala gani katika suala zima la *Diaspora* na suala zima la kuwekeza katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nilisema mwanzo na narudia kwamba ni muhimu kwa nchi kubaini ni aina gani ya uchumi na hili nasema ndio tatizo letu kubwa, mathalan wenzetu wa Finland tunawafahamu wao baada ya kujiona Finland ni nchi iliyokuwa haina uchumi na rasilimali ya aina yoyote lakini Wafinland wao wanachoringia ni kuwa na watu wenye akili. Finland wamewekeza kwenye elimu tu basi na uchumi wa Finland sasa hivi unakuja kwa kutumia wataalam wake tu. Hivi Zanzibar hakuna watu wenye akili, mbona Wazanzibari ni watu wanaosifika Duniani kwamba ni watu wenye vipaji vya akili, tumewekeza kiasi gani sisi katika kujenga *technologies* watu wetu katika kuwafanya Wazanzibari tutumie bongo zao.

La pili, Mhe. Spika, Malta ni kisiwa ambacho ni sawa sawa na kisiwa cha Zanzibar, ina idadi ya watu laki nne takriban watu 450,000, tulipata uhuru tuliwazidi sisi tulipata uhuru Januari 1964 wao walipata mwezi wa kumi 1964, hivi sasa bajeti ya Malta ni tirilion saba kwa pesa za kwetu wao wanatumia Euro, ni tirilioni saba kwenye watu

lakini nne na hamsini ni nchi inayoitwa kwamba ni *credit country*, ni nchi ambayo sasa hivi ni ya kutoa misaada tu wanachokitegemea Malta ni kitu gani, wanachotegemea ni bandari tu kisiwa chao kimezungukwa na bandari, Zanzibar hatuna uwezo wa kujenga bandari.

Mhe. Spika, visiwa vya Maldis takriban ni visiwa karibu mia tatu na kila kisiwa wameweka hoteli moja ya kitalii. Uchumi wao uko hapo tu kwenye suala zima la utalii hapo tu na Maldis inakwenda mbele sana.

Mhe. Spika, Mauritius wao wamejikita zaidi kwenye *ICT* pamoja na tourism. Mhe. Spika, Waisrail pamoja na neema zote walizokuwa nazo lakini wao sasa hivi ndio wasafirishaji wakubwa wa ndizi duniani. Israil kwa mwaka huzalisha zaidi ya tani milioni sitini ndio wazalishaji wakubwa na wao ardhi yao kwa kweli kama mnavyoijua haina chochote wanachotumia ni *irrigation*, kwenye migomba basi ni wazalishaji wakubwa, je Zanzibar migomba kule Makunduchi haioti, je Gando migomba kule vipi hivyo sisi tunashinda kusafirisha hata mkungu mmoja nje ya nchi.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru Zanzibar hapa miaka ya sitini Mhe. Spika, biashara yetu kubwa ilikuwa ni haya maji, meli zilikuwa zikija hapa na kwasababu maji ya Zanzibar yana sifa, wataalam wanasema yana sifa kubwa kweli kweli. Mameli yalikuwa yakija kufunga nanga hapa kwa ajili ya kununua maji tu.

Mhe. Spika, suala zima la bandari kama nilivyosema kisiwa cha Malta pamoja na Singapore wao wanaendeshwa na bandari tu, sisi vipi mpaka leo tunazungumzia Mpiga duri miaka 50 Mpigaduri, hiyo tokea naingia baraza hili Mpigaduri mpaka leo hata hatujui imefika pahala gani.

Mhe. Spika, wananchi wa Namibia wao takriban chumvi ni biashara kubwa kwao. Nenda katika hoteli zote kubwa na ndogo kwenye meza utakuta kuna kichupa cha chumvi na sukari, leo hakuna anayejua hapa umuhimu wa chumvi lakini kila mmoja kwa kweli ni mtumiaji mkubwa wa chumvi, na nimeorodhesha hapa nchi pamoja na makampuni mengi ambayo kwa kweli wanazalisha chunvi na ni wauzaji wakubwa na nchi zao kwa sehemu kubwa uchumi wao wanategemea chumvi.

Mhe.Spika, orodha ipo kubwa Argentina, Australia, Austria, Belarus, Beljam, Bosnia, Brazil, Canada, Chile, China, Colombia, Denmark, Egypt, France, Jaman na nchi nyengine nyingi zinaendelea humu, jamani chumvi sisi hapa Zanzibar hatuna. Ukenda Kojani huko kuna milima kwa milima ya chumvi, watu wameshapofuka macho kwa kuangalia chumvi kila wakati, hebu twambie tu Serikali mnashindwa kuwasaidia watu hawa. Mnashindwa kuwasaidia wazalishaji chumvi na kuisaidia nchi katika kui-*export* chumvi au si chochote si lolote, tuna mifano hai ambayo Serikali na makampuni makubwa duniani wanaotegemea chunvi.

Mhe. Spika, tuna uwezo wa kusafirisha mazao na ndio ikawa kipato chetu kikubwa kwa nchi pamoja na mambo mengine, lakini hivi niseme tutaendelea mpaka lini Mhe. Spika, kusafirisha karafuu hivi hatuna uwezo wa kuisanifu karafuu na kuuza *product* ya karafuu. Hatuna uwezo wa kuuza mwani na kusafirisha *by product* ya mwani. Mhe. Spika, kinachohitajika ni sera na kuwa na Serikali makini.

Mhe. Spika, mwisho namalizia kwamba tuna tatizo la wataalam, tuna wataalam sijui niwaite wataalam gani, inawezekana wataalam wetu wana matatizo wataalam wa uchumi au pengine Serikali haitaki kusikiliza mawazo ya wataalam tulionao na kwa maana hiyo basi tumeshindwa hadi leo miaka 50 kubaini aina ya uchumi tunaohitaji, lakini nasema Zanzibar kama tutakuwa na wataalam na Serikali itakuweko makini tuna uwezo wa kutegemea kila sekta. Mhe. Spika, wenzetu wanategemea bandari, wenzetu wanategemea viwanda vya uvuvi Zanzibar tumezungurukwa na bahari kila upande Mhe. Spika.

Pendekezo langu Mhe. Spika, na hapa naomba niseme kwa taratibu naomba niishauri Serikali ili sasa tuitishe mjadala wa kitaifa ili kuweza kubaini Zanzibar tunahitaji kuweza kuegemea kwenye uchumi wa aina gani, na nasema tuitishe mjadala wa kitaifa ili tujue kwamba sasa Zanzibar tunataka kuegemea kwenye aina hii na hii, lisiwe ni jambo la kisiasa kwa sababu likiwa ni jambo la kisiasa maana yake nini. Maana yake Rais atakayekuja atakuja na sera zake mbali; atakuja na mipango yake mbali itakuwa siku zote tunaondosha hili tunaweka hili ndani ya miaka mitano hakuna safari. Tukiitisha mjadala wa kitaifa tutajua kwamba taifa letu ndani ya miaka 50 tunategemea aina hii ya uchumi au ndani ya miaka 100 tunagemea aina hii ya uchumi.

Hiyo itaondosha kwamba chama chochote kitakachokuja pengine kitakuja na sera tofauti katika utekelezaji wake, lakini ule msingi hasa wa uchumi bado utakuwa umesimama pale pale kama kitakuja chama tofauti au kama atakuja Rais tofauti ndani ya miaka mitano au kumi kwa kweli atabadilisha sera lakini tutakuwa tuna aina hii, tunasema kwamba uchumi wa Zanzibar ni aina hii kwa hivyo sote tuelekee huko, lakini kwa utaratibu huu tulionao Mhe. Spika, kwamba kila Rais miaka mitano anayekuja aje na sera zake, siku zote tutaendelea kusimama hapo na wananchi wetu watakuwa hawana uwezo na wataendelea kuwa masikini katika nchi yao iliyojaa neema na utajiri.

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Shadiya Moh'd Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha kuhusu Mapendekezo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa fedha kwa namna ya usimamizi wa fedha za Serikali pamoja na jitihada zake za kuongeza mapato.
Vile vile nimuombe Mheshimiwa Waziri bado aongeze jitihada za kazi zake hasa akizingatia kwamba kuna watu wachache wasio waaminifu na hawapendelei mema kwenye nchi hii.

Mhe. Spika, pongezi nyengine nimpongeze Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoshiriki kuja kusikiliza bajeti ya serikali yetu siku Waziri wa Fedha alipowasilisha na namna anavyoonekana ndani ya Bunge kutetea haki ya fedha za Wazanzibari zinazotokana na Muungano. Hiki ni kitendo cha uungwana na utendaji bora wa kazi na tunamuambia hongera Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naishukuru Serikali kwa bajeti inayomalizika kurekebisha mishahara ya wataalam na wazoefu. Nataka nimuarifu Mheshimiwa Waziri kwamba bado kuna matatizo kwa baadhi ya wafanyakazi kutopata haki zao, kwa hivyo ni vyema suala hili Mheshimiwa Waziri akalifanyia kazi kwa haraka sana.

Mhe. Spika, nije kwenye kitabu ukurasa wa 40 mashine za risiti ni suala zuri sana kuanzisha utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mashine kwani tutaondoa matatizo ya wale watu wachache wasio waaminifu. Lakini namuomba Mheshimiwa Waziri hili kabla halijaanza kufanyiwa kazi ni vyema kuanza kutoa taaluma kwa wafanya biashara, ili tusije kupata usumbufu kama wenzetu wa Tanzania Bara waliofikia kufungwa kwa maduka yao.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba naunga mkono asilimia mia bajeti hii ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Serikikali ya mwaka 2014/15 na kabla ya kuchangia nimpongeze sana Mheshimiwa Shadya kwa kupunguza wakati ambao Mheshimiwa kwa heshima kubwa naomba muda huo uniongeze ili kufidia.

Mhe. Spika, kwanza unajua kuwa katika vitabu vyetu vya bajeti vimeonesha namna ya makusanyo yalivyo na sekta ya ukusanyaji na matumizi na namna ya uchumi ulivyopanda au ulivyoongezeka. Lakini ukiangalia hali ya wananchi wenyewe badala ya uchumi kuwa unakua hali zao za kimaisha kwa jumla zinazidi kwenda chini, na kiutaalamu ningeliomba Mheshimiwa Waziri husika, anieleze uchumi unakuwa vipi mpaka hali ya wananchi ikawa iko duni zaidi. Wakati mimi nikifikiria kuwa kila uchumi ukikua na hali ya maisha inakuwa nzuri zaidi, hilo ni moja. Na kwa sababu ya wakati nianze na kilimo.

Mhe. Spika, katika vitabu tumeona kuwa safari hii yaani 2013 ukilinganisha na mwaka 2012 hali ya kilimo kwa baadhi ya mazao imeongezeka. Kwa mfano 2012 mpunga uliovunwa ulikuwa ni tani 6655, 2013 ni tani 33,655 ikiwa ni ongezeko la asilimia 528.2 haya ni maendeleo makubwa ya kilimo.

Mahindi kutoka tani 857 mwaka 2012 hadi kufikia tani 1419 mwaka 2013 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 65.5 pia ni maendeleo katika kilimo.

Viazi vitamu kutoka tani 31768 mwaka 2012 hadi kufikia tani 53957 mwaka 2013 ikiwa ni ongezeko la asilimia 68.9 pia ni maendeleo ya kilimo.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la watu lilivyo ardhi inavyopungua na mahitaji ya kilimo ningeliiomba Wizara itumie mbinu iliyotumia kwa kuongeza ufanisi wa kilimo hiki, kuongeza zaidi na hasa kwa mazao mengine ya mboga mboga na kadhalika ambayo yanahitajika sana katika soko lile la utalii na humu hayakuanishwa.

Jengine Mheshimiwa ukusanyaji wa kodi ni muhimu sana kweli kweli ili kuweza kuendesha shughuli zetu. Na kama kodi zitakuwa zinakusanywa ipasavyo katika sekta zote ninaamini nchi hii isingelikuwa na umaskini.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa ni kuwa utalii ni sekta kiongozi na ndio inayoingiza fedha nyingi za kigeni kuliko sekta zote nyengine. Katika nchi hii na utalii una fedha inayokusanywa kutoka kwa watalii binafsi na kuna fedha inayokusanywa katika sehemu ya ardhi kwa shughuli zao za kimaendeleo ya kiutalii. Ikiwa hii ni sekta kiongozi na mimi naomba nizungumze zaidi katika sekta hii, mimi binafsi sijaona kuwa serikali iko serious kwa kukusanya kodi katika sekta hii.

Kwanza kwa sababu ni sekta kiongozi, hapa kujisifia kwa kupata watalii 181,301 mwaka 2013 kutoka 169233 mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la watalii 12,068 mimi naona tusijisifie na tujue mpaka sasa hivi kama kweli kungelikuwa na umakini katika kukuza soko hili la utalii na kwa sababu tunasema kwa Zanzibar kuna vivutio vya utalii. Kwa hivyo watalii wangelikuja wengi zaidi.

Ninasikia kuna visiwa vya wenzetu katika nchi za watu huko watalii wanafika mpaka milioni mbili, milioni tatu kwa mwaka, kwa nini sisi iwe ni 181,000 tu, ni idadi ndogo sana. Lakini ni wajibu wetu Mhe. Spika, kuilinda idadi na kuongezeka. Tunajua sipendi kusema hivyo lakini lazima niseme hii biashara ya utalii ni biashara tete sana inahitaji kulindwa kwa nguvu zote na tumeshuhudia viashiria chungunzima ambavyo kama havikudhibitiwa visitokee tena na hii idadi hii itazidi kupungua na hali yetu itakuwa mbaya kabisa kabisa.

Sote tunajua kuna watu hapa mpaka watalii walimwagiwa tindi kali, hili jambo ni baya sana kweli na serikali ilikuwa iwe makini kuangalia kuwa tendo kama hili halitokei tena maisha. Kuna mahoteli makubwa ya watalii yametiwa moto na vitendo hivi vimetokea mpaka hivi karibuni, ni jambo baya sana la kuwafukuza hawa watalii. Tuone kuwa hili halitokei tena na mambo mengine ambayo yanawatisha kuhudhuria katika au kuingia katika kisiwa hiki. Kwa hivyo ninaiomba serikali sana kama hii ni sekta kiongozi iwe makini, isiwe na muhali kuona kwamba vitendo vyovyote ambavyo vinasababisha watalii wasiingie katika visiwa hivi vinaondolewa kwa gharama yoyote.

La pili, kuna ubovu mkubwa sana kweli kweli wa ukusanyaji kodi kwa mfano, tumesoma kitabu hiki cha Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kitabu kinachohusiana na ripoti ya ukaguzi yakinifu kwa miradi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Humu nitazungumza machache tu kwa sababu ya wakati, lakini tutaona kuwa kama ingelikuwa serikali iko makini na inakusanya kodi ipasavyo k sisi tusingelikuwa na tatizo katika kuendesha nchi yetu.

Mfano, kuna malipo ya kodi ya ardhi yaliyolipwa pungufu US Dollar 98209 ikiwa ni sawa sawa na Tanzania Shillings 150,224,724 maelezo yake ni marefu lakini natoa tu kama ni taarifa kwa sababu ya wakati, kwa sababu Mhe. Spika, hakusema kuwa ataniongeza zile dakika zilizobaki kule. Halafu kuna miradi ya ardhi iliyosajiliwa ambayo hailipi kodi ya ardhi hii iko katika ukurasa wa 52 ya kitabu hiki na yote imeandikwa ningeliisoma lakini wakati hamna. Ni miradi iliyokuwa haipungui 70 ipo tu ishasajiliwa lakini hailipi kodi ya ardhi.

Sasa ikiwa myanya ya upotevu wa ukusanyaji wa kodi unakwenda kama hivyo unafikiri sisi tutafika wapi. Lakini hawa si kwa kuwa hawalipi kodi ijulikane kodi hii inapita wapi ikawa katika hali hii kwenye ardhi tu huko. Kuna maeneo ya uekezaji ambayo hayajaingizwa katika mtandao wa ulipaji kodi ya ardhi, vilevile iko katika ukurasa wa 55 kuna kiambatanisho kilichoanza 107 mpaka 113 ni miradi 102 na katika hiyo miradi 18 ni ya wageni na miradi 84 ni ya wenyeji. Hiyo ni miradi ya uekezaji ambayo haijaingizwa katika mtandao wa ulipaji kodi wa ardhi inafanya kazi tena vizuri na ipo mpaka leo na si kwa kuwa hailipi kodi yenyewe haijui serikali tu, ninaiomba serikali iangalie wapi kodi hii inakwenda, mapato hayo.

Kuna malipo ya kodi ya ardhi yaliyolipwa pungufu hii tayari nimeshaieleza. Halafu tena kuna miradi mengine ambayo mpaka sasa inafanya kazi lakini haijaingizwa hasa katika ule mtandao wa ulipaji kodi. Kwa hivyo, ninaiomba serikali kwa ujumla, pamoja na kuwa sekta hii ina Wizara yake ione ni kwa sababu gani sisi tunatilia nguvu utalii. Watalii wanafanya shughuli zao lakini kodi hazilipwi, pesa nyingi sana haya ni mambo ambayo

kayaona tu mkaguzi lakini kuna mengine chungunzima hayajaonekana na halafu kama kuna hatua ichukuliwe au vyenginevyo iundwe Tume ikachunguze kwa makini kwa sababu ni pesa nyingi sana.

Mhe. Spika, halafu kuna makubaliano wenzetu wanapotaka kuekeza na kujenga mahoteli, kuna masharti yake, wanapewa wajenge mahoteli yao katika hali ambayo kutakuwa na mita 30 mpaka kufika kule bahari inapofika wakati maji yanapojaa katika sehemu za fukwe au mita 10 katika sehemu za mawe. Lakini wenzetu wamejenga mpaka wamejenga jeti wamekwenda mita wanazozitaka wenyewe kwenye bahari huko na katika kufuatilia hakuna utaratibu uliowekwa katika maandalizi ya ujenzi wa jeti hizi.

Malipo yake na pia hakuna utaalam wala wanasheria wanaohusika wataifanya vipi ardhi inayotumika katika bahari ili iweze kulipiwa kodi, kwa sababu kwenye ardhi ya nchi kavu inawezekana lakini kwenye bahari utaalamu huo hakuna. Kwa hivyo kuna jeti nyingi sana katika visiwa hivi vinatumika wenzetu wanapata fedha lakini hazilipii kodi wala hakuna utaratibu wa kulipiwa kodi, hayo ni mapato yanapotea.

Kwa hivyo, Mheshimiwa, mimi sitaki nizungumze sana kwa sababu ya wakati lakini tujuwe tu kuwa kuna mapato mengi yanapotea si kwenye ardhi tu na kwenye taasisi nyengine na serikali haiko *serious* lakini naamini mapato hayo yanatumika katika njia ambayo siyo iliyokusudiwa

Jengine Mheshimiwa, tumejiingiza katika uvuvi wa bahari kuu, tuna mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu na bahari kuu ni kwenye samaki wengi sana na tunayo ofisi inayohusiana na uvuvi wa bahari kuu. Nililoshuhudia katika ofisi ile kuna wafanyakazi ambao ni wapungufu wa idadi hivi sasa, kuna nafasi kadhaa hazijajazwa. Lakini kazi kubwa wanayoifanya ni kutumia pesa nyingi sana kwa kufanya doria kule baharini ili samaki wetu wasiweze kuvuliwa kwa njia ya kuibiwa. Nini kinaingia hakuna, sasa na wakati serikali ina mpango wa kuekeza katika uvuvi wa bahari kuu, mpaka leo hatukupata taarifa yoyote.

Mhe. Spika, na tuseme mathalan itokezee japokuwa siombi itokezee wakakamatwa hao wavuvi haramu hawa samaki waletwe hapa Zanzibar kwa sababu ndio eneo walilokamatiwa wanataka kufanywa nini. Hapana pa kuhifadhia, hapana pa kuwaweka na hapana watu wa kuwanunua. Kwa hivyo, mimi ninavyosema ili kuweza kuingiza fedha na tusitumie tu kwa sababu kukuza uchumi vile vile ni kuzuia fedha isitoke kwa njia ambayo si ya lazima, ni lazima tujiimarishe ili mamlaka hii ya uvuvi wa bahari kuu iweze kufanya shughuli zake ipasavyo.

Kuweko na bandari yao maalum, kuwepo na majumba ya kuhifadhia hawa samaki na ikiwezekana hakuna sababu kwa nini sasa Zanzibar haianzishi rasmi ujenzi wa Viwanda kwa sababu ya kuhifadhia samaki. Tunavyoambiwa kuwa kuna samaki huko wa kutosha katika eneo letu lakini hatuna vya kuwafanya kulinda tu haisaidii chochote isipokuwa ni kupoteza fedha ya wananchi.

Mhe. Spika, jengine Mheshimiwa, nchi yetu kama tunavyojua ina visiwa na tukitaka tusitake tukiitumia bahari ilivyo tunaweza tukaingiza fedha nyingi sana na sidhani kuwa kuna nchi maskini kama yetu yenye mazingira katika haya. Mimi Mhe. Spika, nashangaa sana kweli kweli kuwa sote tunajua kama tukizikuza bandari zetu lazima biashara itakuwa kiasi ambacho hatuwezi kufikiria.

Mhe. Spika, mpaka leo tuangalie tokea bandari yetu ya Malindi kufanywa lile tuta na kuharibu mazingira kama inavyofanya hivi sasa kulikuwa na mradi mkubwa wa kuongeza eneo la Mpiga Duri na eneo lile kwa utafiti ni lenye kina kikubwa cha maji na kwa Zanzibar *position* iliyo katika ukanda wa Afrika Mashariki ingelikuwa ni sehemu nzuri sana ya biashara. Kila siku watu wanakuja, mikataba inawekwa halafu tena mambo yanafeli, basi sijui tunataka tupate maelezo serikali hasa imeliona vipi kitega uchumi hiki kikubwa kabisa kikaweza kudharauliwa kiasi chote hiki. Miaka 50 imepita bado tuko katika hali ile ile.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ninashukuru, Mhe. Spika, pia kuna sababu gani mpaka leo Zanzibar hii kuwa na bandari moja tu, kwa nini kama Mkokotoni hakuwekwi bandari na tuhakikishe ikiwekwa itatumika na itaingiza kweli kweli. Zaidi ya kuwasaidia wananchi lakini itakuza uchumi wetu, ile kufanywa Pemba kuwa itakuwa ni *International* kama ilivyozunguzwa pale iwe ni mpitio wa biashara imefikiwa wapi naona mpaka leo tuta liko vile vile hakuna maendeleo yaliyofanywa.

Sasa Mheshimiwa, ili tuweze kubadilika ni lazima na sisi tuingie katika *system* tusinganganie kujisifu kwa kukusanya kodi kwa wananchi tu lakini serikali ione kuwa imeleta maendeleo makubwa ya kuingiza fedha katika nchi ili Zanzibar ibadilike iwe kama visiwa vya wenzetu vilivyo katika sehemu nyengine za ulimwengu.

Kwa sababu ya wakati Mheshimiwa, ninashukuru kwa kupata nafasi hii. Ahsante sana.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini pia na ile hotuba iliyoitangulia hii iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ikulu na Utawala Bora Mhe. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Spika, wakati Waziri wa Fedha alipokuwa anawasilisha hotuba yake, alituomba wajumbe ambao tulikuwa na vitabu hivi vya hotuba yake kwamba *paragraph* ya 9-11 isiwemo. Mimi Mhe. Spika, kwa sababu nilikuwa sijaisoma nikasema sawa. Lakini nilipozisoma *paragraph* hizi mimi sikuona sababu kwa nini zitolewe. Ni *paragraph* nzuri zenye mantiki na kweli hasa zinatia mbolea hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Kwa hivyo mimi sioni sababu za msingi na ninamuomba Waziri kwamba hizi zibaki kama zilivyo. Kwa sababu kitabu hiki kwa sisi ambao tumekipata tunajua hilo lakini mtu mwengine yeyote ambaye hakusikiliza hotuba yake au hana taarifa ile ataisoma kama ilivyo. Kwa hivyo sioni sababu kwa nini, ninamuomba Waziri kwamba bado ibaki kitabu hiki, hakuna cha kutoa kwa sababu humu ambacho kinakera au kinaleta kitu ambacho kinaifanya hii isiwe hivi ilivyo. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha ilitanguliwa na hotuba ya Mhe. Mwinyihaji na tulipewa vitabu hivi, kitabu cha kwanza mapitio ya hali ya uchumi 2013 na utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Zanzibar 2013/14 na kitabu namba mbili, Muelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2014/15.

Mhe. Spika, ukifungua kitabu cha pili, ukurasa wa 98 kuna *cluster* hizi lakini nazungumzia namba III ambao ni Utawala Bora na Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, hii inaingiza na haki za binaadamu. Haki za binaadamu ni jambo la msingi duniani kote na haki za binaadmu kama hazikulindwa, hazikusimamiwa basi dunia itakuwa na machafuko makubwa.

Saa nyengine yanayotendeka hapa Zanzibar huwa tunajiuliza, Mhe. Spika, mimi nikikutusi, nikikukashifu, nikikusingizia nakuvunjia haki zako za binaadamu. Sasa kama vitabu hivi vinazungumzia utawala bora, haki za binaadamu, lakini yanayotendeka hapa ni tofauti ya yaliyoko humu inakuwaje.

Mhe. Spika, wanaofuatilia mikutano mbali mbali ya hadhara inayofanywa na hapa sitaki nitafune maneno kwamba na chama fulani , wenzetu walioko humu Chama cha Mapinduzi matusi yamekithiri, tena anayetukanwa ni miongoni mwa viongozi wakuu wa nchi hii, Maalim Seif Sharif Hamad. Matusi kila mkutano ni kama ibada, ni kama desturi. Sasa mimi nafikiri tusirudishwe kule tulikokuweko hatuzikani, imamu huyu hafuatwi, msikiti huu hausaliwi. Nasema hivi kwa sababu Maalim Seif Sharif ni Makamu wa Kwanza wa Rais na Katibu Mkuu wa *CUF*. Lakini Chama cha Mapinduzi vile vile kina Rais, kina Makamu wa Pili wa Rais pia kina Makamu Mwenyekiti. Sasa kama huku kuna Katibu Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, huku kuna Makamu Mwenyekiti, Rais. Mimi sitaki niende mbali sana lakini tusifikishane pabaya, panya hafundishwi kula usufi.

Mhe. Spika, jana taarifa tulizozipata kulikuwa na ziara ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi katika Soko la Mwanakwerekwe, ameanza mahala pamoja panaitwa Asha Fatuma ni sehemu hiyo hiyo, lakini ziara hiyo ikaishia kwenye soko ndani, alikuwa yeye na wajumbe wengine na wakereketwa. Hakuna marufuku ya kwenda mahali, lakini ujumbe aliokuwa akiupeleka hauashirii kwamba nchi hii huko mbele itakuwa na amani. Ujumbe Serikali Mbili lazima zibaki, hilo si tatizo kwa sababu tunajadili, kama ni mbili, kama sita, sawa. Lakini haya yaliyofuatia baadae asiyetaka Serikali Mbili aende kwao, wapi? Anayechezea Muungano akachezee na ndevu za Seif Sharif Hamad. Sisi ndio viongozi tusipoyasema haya humu tukayaseme wapi. Sasa hayo ni mambo mimi nasema si vizuri kufikishana mahali tukarudi kule nyuma.

Jengine alilokuwa anaongeza kama kibwagizo Serikali ya Umoja wa Kitaifa lazima ivunjwe, hayo ndio maneno aliyokuwa akisema, masikini roho yake.

Mhe. Spika, mimi ninajiuliza Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa imetangazwa muda mrefu kwamba kitakachotumika, kitakachoongoza ni Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ni sera za CCM zitakazotumika kuendesha serikali hii. Sasa yanapotokea haya ndio sera yenyewe? Ndio ilani yenyewe? Mimi siamini, na kama yanatendeka haya yananyamaziwa maana yake nini, tuamini ni hivyo?

Mhe. Waziri wa Fedha rafiki yangu nimeona katika hotuba yake ya bajeti kuna vipaumbele asilimia 80 ya bajeti ni vinne, miundombinu shilingi 160 bilioni sawa na asilimia 48+, Afya asilimia 9.3 sawa na shilingi 30.6 bilioni, elimu shilingi 28.4 bilioni. Mimi namsifu kwa sababu katika mipango yoyote lazima uwe na vipaumbele, lakini kipaumbele kinakuwa kimoja na hapa maana yake inayo-*lead* ni miundombinu. Lakini kwa sababu umesema na hivi ni vipaumbele basi katika kutekeleza kipaumbele cha elimu mwaka huu 2014/2015 ada ya mitihani ya *Form VI* kama ilivyo ya *Form IV* itafutwa nakupongeza sana.

Mhe. Spika, kitu ambacho nataka hapa niongezee katika kipaumbele cha elimu kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe, unapowekeza kwenye elimu hata kama utachukua muda lakini ukiweza kuwekeza kweli kweli, baada ya muda huna matatizo tena. Sisi tunawekeza kidogo kidogo mno na ndio maana elimu sasa ni katika jambo ghali.

Mhe. Spika, Waziri wa Fedha ameshakuwa Mbunge wa Jimbo, ameshapata kesi mbali mbali kama tunazopata sisi, yangu mimi, Mhe. Salmin Awadh, kila aliye na jimbo anaendewa na baadhi ya wanafunzi katika jimbo lake. Mimi sina hili, skuli nimeambiwa niende na hiki, Mheshimiwa nisaidie, kuna *fees* mpaka kutoka darasa moja kuingia jengine.

Sasa hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanakwambia aa hiyo sio rasmi, lakini watoto wanafukuzwa, wanarudishwa makwao. Ukizikusanya ada zile wanafunzi 400,000 kila mmoja shilingi 15 elfu *average* ili aweze kwenda skuli darasa moja kuingia jengine bila ya bughudha, utoe na pesa nyengine za kujenga skuli, hizi zitakuwa kama shilingi bilioni sita (6). Lakini *six billion* hizi mimi nashauri sana kabisa katika kipaumbele cha elimu wanafunzi hawa bughudha hii ingeondolewa ikajulikana kabisa, baya zaidi ni kwamba fedha hizi kama inavyoelekezwa kwamba hii sio rasmi, baadhi ya skuli walimu ndio mtaji wao wanakopeshana wala hawalipani, mtoto hakwenda na shilingi 3,000 anarudishwa, asilimia 20 ya wanafunzi wamekuwa watoro kwa sababu hawana ada hii.

Sasa Waziri wa Fedha namuomba sana ili suala hili liwe limekwisha mwaka huu ndio sawa, lakini *Inshaallah* mwakani Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee kuwa Waziri wa Fedha hili aliwekee kipaumbele angalau wanafunzi hawa 400,000 waondolewe hii bughudha na si wanafunzi peke yao hata hawa wazee.

Jengine ni kwamba amesamehe, amezungumzia habari ya kusamehe ushuru baadhi ya misamaha ya kodi. Kuna wawekezaji anachukua mradi anaambiwa una *grass period* miaka mitano wewe hiki hulipi, na hiki hulipi; ikifika miaka minne na nusu mradi anauhamisha kwa mwengine, yule mwengine naye ni mpya anakuja na *right tape* yake maana yake hivi, maana yake vile. Mheshimiwa kuna mahoteli huu ni mwaka wa 20 kila miaka minne na nusu anabadilishwa huyu, linabadilishwa jina hili, halipi kodi inakuwa tena mradi ule sasa hatujui ni mpya, mkongwe au vipi.

Sasa Mhe. Waziri wa Fedha kwa hili namuomba aliangalie mno tusifanywe kama vile ni watoto wadogo hapa sisi, mradi miaka mitano sawa, hujamaliza miezi sita unamhamishia mwengine na mwengine anakwambia na mimi nisamehewe ushuru. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali anayajua sana haya, sana kabisa. Kwa hivyo, hili mimi nashauri sana kuwa na hili liangaliwe kwa sababu linatupotezea mengi sana na tunafanywa kama watoto wadogo. Sisi si watoto wadogo nchi hii ina viongozi wazuri, nchi hii ina watu na akili zao tusibabaishwe kwa sababu mtu ana mradi leo hoteli hii inaitwa *club* gani, keshokutwa inaitwa Sheraton, ikishindwa kesho inaitwa sijui ***Rip,*** kila miaka minne na nusu jina linabadilika na *owners* wanabadilika.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Jengine ni kwamba Mhe. Waziri wa Fedha amezungumzia masuala ya kampuni za msimu. *ZANTEL* Makao Makuu yake ni hapa, kwa hivyo zile kodi analipa hapa, lakini *ZANTEL* vile vile ina-*serve* Bara kama ambavyo *TIGO*, *VODACOM*, *Air tell* wana Makao Makuu yao Bara, lakini vile vile wanatoa *service* Zanzibar. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha amesema kwamba kutakuwa na fomula itakayotumika katika utaratibu mpya. Mimi namuomba Mhe. Waziri hapa atwambie vizuri, hata hiyo fomula kama anaijua basi atwambie. Kwa sababu

sisi ndio tutakaokwenda huko kwenye *ZANTEL* kama kamati. Je, fomula hii inatumika vipi? Mumelipa ngapi? Mutalipa lini? Nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha hilo ni moja, hiyo fomula kama anaijua basi atupe, kama haijui awaambie ili si muda mrefu na sisi atupatie.

Mhe. Spika, mambo kama haya tumeshaambiwa sana. *ZRB* na *TRA* washakubaliana habari ya ushuru lakini hakuna utekelezaji, hapa ndio wasi wasi wangu ulipo. Suala la magari kutoka Zanzibar kupelekwa Bara yakakaa pale mpaka yatakaribia kuoza ulipe ushuru mwengine kila siku tunaambiwa ni kero ya Muungano lakini hiyo tumeshaimaliza. Haya peleka gari kama mshaimaliza basi kama halitokaa pale miezi miwili au mitatu mpaka ulipe, kumaliza kwenyewe ni kupi ni kunyamaza kimya?

Sasa haya ndio yanayokera. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha rafiki yangu tena rafiki yangu kweli kweli, hebu haya ayaweke vizuri, ayaweke wazi na ukweli ili sisi kama Wajumbe wa Baraza tulifanyie kazi.

Mhe. Spika, jengine la mwisho kuhusu leseni. Kuna leseni sasa hivi za mwaka mmoja, miaka miwili na mitatu, lakini waziri katika mbinu zake za kuongeza mapato ameona kwamba mfumo wa kutoa leseni sasa miaka miwili, mitatu na mitano. Moja katika sababu zake ni kwamba inaondoa urasimu lakini ninachozungumzia hapa ni kwamba, bajeti hii ni ya mwaka huu 2014/2015, mwaka unaoanza kesho. Watu kwa sheria hii au kwa amri hii watakata leseni wengine miaka mitano katika mwaka huu wa fedha unaokwenda wa 2014/2015, atakayekata miaka mitano mwaka 2015/2016 hakati, 2016/2017 hakati, 2017/2018 hakati mpaka miaka mitano ishe na atayekata miaka mitatu hivyo hivyo.

Kwa hivyo, bajeti hii kwa mwaka 2014/2015 anaweza akapata ahuweni, najiuliza mwaka 2015/2016 maana yake hii ni nchi na hii ni serikali hutasema kwamba baada ya mwaka 2014/2015 hakuna tena serikali, hii serikali inaendelea na itakuwa na bajeti yake. Kwa kipindi hiki sawa, *yourself*. Je, mwaka 2015/2016 Mheshimiwa ambapo nafikiri watu wengi watakuwa leseni wameshalipia kwa miaka mitatu, minne au mitano mbele unalionaje hili. Kwa nini tusingeiacha kama hii *system* inavyokwenda. Lakini nasema haya ni masuala ambayo akitufafanulia ndio tutapata kujua kipi kinaendelea na miaka mingine ikija inakuwaje.

Mhe. Spika, sitaki nihimizwe tena na nashukuru sana kunipa nafasi hii na mimi kuchangia angalau haya.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuwa katika hali ya uzima. Lakini pia nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kujadili na mimi mustakabali wa nchi.

Kabla sijampongeza Mhe. Waziri kwanza naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jinsi anavyojituma na kuhakikisha kwamba nchi hii iko katika hali ya usalama na utulivu. Si hayo tu, pia tumeshuhudia wazi jinsi Mhe. Rais anavyojali watu na maendeleo ya nchi hii.

Ninasema hivyo kwa sababu ni hivi karibuni tu, tumejionea wenyewe kutimia miaka 50 maendeleo mengi sana ambayo yamepatikaa kwa upande wa Zanzibar. Sasa mimi nishangae wale wanaosema hakuna maendeleo, naomba tuingie katika mjadala wa kuitakia mema nchi yetu kwa kuiombea nchi yetu kujikita katika maendeleo kama sisi tumeletwa na wananchi katika Baraza hili.

Mhe. Spika, sasa nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora. Vitabu hivi ndio dira na ndio malengo ya kuhakikisha kwamba tunasimamia utekelezaji wa vitabu hivi viwili. Mimi nitoe tahadhari tu, kwa sababu bajeti yetu sisi ni tofauti na bajeti ya wenzetu wa Bunge. Sisi humu tumepitisha wenyewe kwenye kamati, sasa mtu anapokuja kusema hapa wizara fulani hakuna pesa au kufanywe hivi, miradi ifanywe hivi, tumeshapitisha miradi Mhe. Spika, lililobaki. Sisi humu ni kutafakari na kutilia mkazo mambo ambayo yameshapitishwa kwenye bajeti hii kuhakikisha kwamba sisi ndio wasimamizi wakuu wa bajeti hii.

Mimi kuna baadhi ya maneno tu nitamuuliza Mhe. Waziri, pia nitakuwa sitendi haki kwa sababu tumesema sisi tunajadili bajeti tusitoke nje ya mada. Lakini leo hapa msemaji aliyekaa kitako sasa hivi katoka nje ya mada, kama ni kutukanwa Maalim Seif Sharif na Rais Dr. Ali Mohammed Shein anatukanwa, Makamu wa Pili wa Rais anatukanwa. Sasa tusiseme maneno ambayo ukamuelekezea mwenzako kidole hiki kimoja wakati hivi vyengine vyote vimekuelekea wewe.

Tumekuja humu kujadili bajeti sasa nadhani mambo yaliyopita nyuma si vizuri kuyaleta humu na hii ni siasa tu, tukitoka humu siku zote tunasema tuwe wamoja na ndio maana tukaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili tuwe wamoja, lakini tukifika kwenye viriri kila mmoja anajisahau anasema maneno anayoyataka yeye mwenyewe. Sasa *are we serious?* Kama ni hivyo tungoje mwaka 2015, tukae kwenye viriri tusubukuwane hapo ndipo tutafanya jambo la maana lakini sio sasa hivi (*Makofi*).

Mimi Mhe. Spika, watu wameanza kusema maneno humu mie sitojibu, kwa sababu tunaingia kwenye bajeti hatuingii kwenye malumbano ya aina nyengine yoyote. Sisi tumeletwa humu na wananchi Mhe. Spika, kuwatakia mema wananchi waliotuleta humu. Mimi nadhani tusijaribu kupotosha, tujaribu kusimamia kwa sababu sisi ndio wananchi wanatutegemea.

Mhe. Spika, imetajwa habari ya Umoja wa Kitaifa hapa, mimi namwambia Mhe. Salmin Awadh lete hoja ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa kama ni mbivu au mbichi itajulikana humu kwa sababu naona hatujitakii mema sisi wote Wazanzibari. Tukikaa humu tunakuwa wamoja, tunachekeana, tunafunua midomo hivi tukitoka nje sote hakuna anaemthamini mwenzake. Kwa nini tumeleta Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Spika, kwa maana tulikuwa tunakwenda vizuri tu sijui kulikoni kilichoingia.

Sasa mimi nadhani tuache malumbano, tuache mambo ambayo hayatutakii mema na wala tusifanye mambo ambayo tukajisuta sisi wenyewe, nilisema hilo nilizungumze Mhe. Spika. Lakini sasa nije katika bajeti sasa.

Mhe. Spika, nasema kwa nini nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake, ni kwamba bajeti hii inakuja kwenye uhalisia. Bajeti hii inatuonesha wazi kwamba hapa ndio uwezo wetu tulionao" *Mtu hujikuna ajipatapo*" mkono huu nikitaka kujikuna nikiupeleka huku haufiki. Sasa mtu hujikuna pale anapojipata.

Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwamba bajeti hii ameileta na kutueleza hata kwenye kamati zetu mbali mbali, tumeona uhalisia kama kipindi cha mwaka haja kilichopita, hatukuweza kutekeleza kwa sababu ya uhalisia wa bajeti ambayo ndiyo tunayoipanga. Lakini mimi nitakuwa na masuala kidogo, isipokuwa naomba tu pale penye nguvu ambapo tunaona tunataka tutekeleze basi nguvu zetu zote tuzipeleke pale.

Jengine nimuulize tu Mhe. Waziri kwa nini kwenye bajeti hii ya maendeleo kutofikia? naomba aje atoe ufafanuzi hapa ili watu huko nje waelewe Mhe. Spika. Pia kuna watu kwamba wanakataa uchumi wetu umekuwa pia atutolee ufafanuzi watu nje wasikie, kukua ni kiasi gani, kumekuwa vipi? Nitamuomba Mhe. Waziri hili alifafanue.

Pia nitamuuliza Mhe. Waziri kuna miradi mingapi ambayo tumeikubali na miradi mingapi ambayo imesimamishwa na kwa sababu zipi? naomba Mhe. Spika, pamoja na kwamba umetia kwenye kitabu na tunaona kwenye wizara mbali mbali bajeti. Lakini tunataka ufafanuzi ili wananchi waelewe, naomba sana.

Nikienda kwenye Utawala Bora, mimi niseme tu kwamba mipango bado tuifanyie utafiti Mhe. Spika. Kwa nini nikasema hivi, kwa sababu vitabu vinaoana hivi. Kwa nini huu mji wetu wa Zanzibar uko kiholela holela ni sababu zipi zinafanya kuwa kiholela, ni mipango miji kwa nini hatuipangi na tukakusudia kwamba tunaiweka hapa Manispaa ya Zanzibar ni kama kioo ambacho ndicho cha kuwavutia watalaii. Mhe. Spika, niombe sana Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Rais Utawala Bora kwa sababu ndio tumeletewa kipindi hiki, niombe sana mashirikiano yao ya hali ya juu.

Kuna jambo jengine ambalo nitalizungumza Mhe. Spika. Kila nikisimama hapa nalizungumzia, sijui lina ugumu gani watwambie kuwa na *One stop Centre* ya mambo yetu ya wawekezaji ambao wanakuja kuekeza. Hebu kwa nini tunakataa hili kuwa na *One stop Centre* ili kuwarahisishia wawekezaji wetu katika mambo yetu ya maendeleo katika mambo ya uwekezaji katika mambo ya aina yote ambayo ukiwa na *One stop Centre* ni kurahisisha mipango ambayo itasaidia.

Mhe. Spika, mimi niliwasikiliza haadhi ya Wajumbe hapa wanasema njia mbaya hakuna hiki, hakuna hiki. Lakini nimesahau kitu muhimu nimpongeze tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kwenda kufungua njia Pemba, njia ambazo zimeleta tija kwa wananchi wetu, njia ambazo zimewatoa watu waliokuwa wanakaa machokoroni wakawa sasa wanajenga karibu na baranbara. Jamani hayo si maendeleo kweli tunataka maendeleo gani tena?

Hayo ni maendeleo na tulikuwa tunapiga kelele humu hakuna njia Pemba, sasa hivi tumshukuru Mwenyezi Mungu *alhamdulillah* ni imani yangu kwamba na hizo zitakazobaki zitamaliziwa.

Mhe. Spika, mimi sitaki nizungumze mengi kwa sababu naiongejea bajeti hii tuipitishe ili sisi ndio wasimamizi wakuu wa kusimamia bajeti hii utekelezaji wake. Lakini naomba Mhe. Waziri wa Fedha na namuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Rais ile miradi ambayo kwa kweli tulikuwa tunaitegemea kutupa tija basi muisukume haraka haraka ili kuweza kupata mapato zaidi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kwa sababu leo hali yangu sio nzuri niunge mkono hoja za wizara zote hizi; Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawa Bora pamoja na Wizara ya Fedha mia chini ya mia, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniona kunipa nafasi hii ili nipate kuchangia katika hotuba hii ambayo inaendelea hapa mbele.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema wakati tunajadili bajeti yetu. Lakini vile vile nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye yeye bado ndio Mwenyekiti wa Tume hii ya Mipango ya Zanzibar.

Vile vile niwape pongezi sana Mawaziri wetu wawili hawa waliowasilisha Mipango ya Bajeti kwa hotuba nzuri ambazo wamewasilisha kwetu hapa. Lakini vile vile niwapongeze sana Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Naibu Katibu Mkuu, Katibu wa Tume na Wataalamu wengine wote kwa kuandaa na kuandika kitabu hiki kizuri zaidi. Mhe. Spika, kwanza niseme tu naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia.

Mhe. Spika, kwanza kabisa kabla sijaendelea na hotuba yangu nilifikiri na nilikuwa na imani kubwa sana kuwa Waheshimiwa Wawakilishi safari hii watawasifu na kuwaita kwa sifa za pekee wataalamu wetu waliofanya bajeti hii ya uhalisia. Wamefanya kazi kubwa na wameonesha kiwango kikubwa cha utaalamu ambao wameandika bajeti hii iliyokuwa sio tegemezi.

Mhe. Spika, sasa niende tu katika hoja moja kwa moja nizungumzie kwanza zao la mwani. Zao la mwani kuna Mjumbe mmoja alisema kama hapa patachimbika. Sasa nataka niwambie kwa sababu ya mazingira tusiweze kuchimba tufukie ili tuweze kupata njia wetu mji uwe safi na uwe bora zaidi.

Sasa nataka kumwabia tu zao hili la mwani tayari serikali na kwa niaba ya serikali nilitia saini tarehe 8/4/2014 na Shirika la *FAO* mradi maalum utakaohusiana na kutatua changamoto za mwani hususan za bei.

Mhe. Spika, kuongeza mradi huu utatatua mambo manne yafuatayo sasa hivi tuko kwenye *BRM*, tuko katika mradi wa kutekeleza miradi mikubwa sana. Sasa mambo hayo manne yatakuwa ni:-

(1) Mpango mkakati wa zao la mwani.
(2) Taaluma ya wakulima wa mwani juu ya kupambana na changamoto za mwani.
(3) Bei ya mwani.
(4) Muongozo wa uwekezaji katika sekta ya ufugaji mazao ya baharini yakiwemo hilo zao la mwani.

Mhe. Spika, kuhusu uchunguzi wa maradhi ya mwani tayari zao hili limefanyiwa uchunguzi kupitia katika Taasisi ya *IMF* iliyokuwa Zanzibar. Moja tulikuwa na uchunguzi wa kufanya jambo la haraka au la moja kwa moja lakini jengine lilikuwa la muda mrefu.

Hili la haraka ambalo lilifanywa kwa ushirikiano na taasisi na hiyo tulibaini kuna mwani wa aina ya ***Polisponia*** ambayo huota juu ya mwani na kusababisha maradhi yale ya mwani au usiote kabisa. Kuhusu haya maradhi ya mwani tatizo linawezekana kutatuliwa kwa wakulima wetu kuondoa katika ile sehemu ambayo wanalima na kuweka katika sehemu nyengine au ule mwani kuupiga moto na kupanda mwengine katika sehemu tafauti.

Huu utafiti wa muda mrefu sasa hivi unaendelea na tukipata matokeo yake tutayatoa kwa wakulima wetu wa mwani. Nataka kuwaambia tu wakulima wetu tunaendelea uzuri na utafiti na wasiwe na wasi wasi tutatoa katika majumuisho yaliokuwa mazuri zaidi.

Mhe. Spika, nije kwenye Bahari kuu. Hapa kuna mambo mawili ambayo Wawakilishi walitoa maoni yao juu ya tatizo hili.

(1) Ilikuwa ni ununuzi wa Meli ya Bahari Kuu.

Mchakato huu umeendelea, tulitoa tenda ya mwanzo lakini kutokana na Sheria ya *Procurement* tulishindwa kwa sababu ya watu wawili ndio waliochukuwa tenda hii na sheria hizo zinatukataza. Lakini wizara ilitangaza tena tenda hiyo na watu 3 ndio waliomba tenda hiyo na kampuni zenyewe ambazo ziliomba ni *Yell Limited* kutoka Dar-es-salaam, *Some and Azan Boat Builder* kutoka Dar-es-salaam na *Crystal Tanzania Limited* zote za Dar- es-salaam.

Katika kuangalia bei zao zote zilikuwa kubwa tofauti na lile lengo la serikali lililojiwekea. Tukaona sasa kwa nini tusipeleke au tukaelekeza nje kama nchi zile ambazo zinaundwa maboti makubwa ambayo ya kisasa na yanayolingana na bahari yetu ndiyo maana tumechelewa na mchakato huo unaendelea nchi zenyewe zilikuwa kama Sri-lanka, India na kwengineko.

Vile vile, kuwasomesha wananchi wale ili kwenda katika Bahari Kuu. Hivi sasa tumefanikiwa kuwasomesha wananchi 25 kupitia katika Taasisi yetu ya Bahari, katika Chuo kishiriki kile cha Mbegani na watu hao 13 walitoka Zanzibar na 12 walitoka Tanzania Bara na tayari wamesha-*graduate*, wamepata vyeti vyao Jumamosi iliyopita ya tarehe 17/5/2014.

Nataka kusema jengine, Mhe. Spika, niseme tu kama bado muda haujesha. Mwaka huu wa Fedha tutasomesha watu 25 wengine na safari hii Zanzibar watatoka 12 na Tanzania Bara watatoka 13 wote watakuwa 25 tutakuwa tumesomesha kwa mwaka huu vijana 50. Sasa nini kusudio la serikali juu ya jambo hili?

Lengo la Serikali juu ya jambo hili ni kutengeneza *Pool* ya wavuvi baadae zile meli zetu ambazo zinaomba kupeperusha bendera ya Tanzania, bendera ya Zanzibar wale vijana wawe na *certificate* za kutosha ili kuwaingiza mle na kupata ajira ya kutosha kwa kipindi kile. Mhe. Spika, hii ndio dhamira hasa ya serikali na kuleta uvuvi wa kwenda katika Bahari kuu.

Mhe. Spika, jengine limeguswa hili josho la Mjimbini Pemba. Hili tayari mkandarasi ameshapatikana na tayari tumeshafungiana mkataba na mwisho wa mwezi wa 5 ataanza kujenga josho hili na josho hili litachukuwa miezi mitatu kukamilika kwake. Sasa ningeomba tu Waheshimiwa Wawakilishi wavute subira juu ya jambo hili na serikali inafanya jitihada zake zaidi ili kuona basi tunaendeleza hatua kubwa ya kuwafikishia maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Spika, kubwa zaidi la wavuvi wetu labda wamesema wavuvi wengi sasa hawapewi misaada mikubwa kama ile iliyokuwa ikitolewa zamani. Kwanza naomba nitoe taarifa tu kwamba ule mradi wa mwaka 2007 mpaka 2010 tayari mradi wa *MACEMP* umekwisha kazi yake. Sasa ndio maana *speed* ile imepungua lakini katika bajeti yetu ya mwaka jana nilisema patakuwa na harufu ya miradi miwili.

Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa tu kuwa miradi iko katika sehemu ya pili ya majadiliano na tayari imekuja. Huu mradi wa *Seo fish* na mradi wa *Smart fish* tunatarajia sana ikifika muda kuweza kuwainua wavuvi wetu na kupata vifaa bora. Lakini hata hivyo sio tu kama serikali imelala au haiwasaidii wavuvi wale. Tumshukuru sana Mhe. Rais Dr. Ali Mohd Shein kwa kufanya ubunifu wa kuunda Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu ya kujua watu wengi wa Zanzibar ni wavuvi na wamezungukwa na bahari.

Sasa tulikuwa na hizi hifadhi za bahari, kuna Minka, Heka kwa Pemba na Menai, hizi pia zinatoa misaada na misaada hii mbali mbali inapokea pale. Misaada ambayo inatolewa pale kwanza misaada ya maafa na vifaa mbali mbali ambavyo vinaweza kuwasaidia wavuvi wetu. Sasa Serikali bado tu ina mtazamo mkubwa wa kuweza kuwasaidia wavuvi pamoja na wafugaji wote ili kuona hali bora inapatikana kwa kila Mtanzania au kwa kila Mzanzibari.

Mhe. Spika, nirudi kwenye bajeti yetu ya uhalisia. Niendelee kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa hatua kubwa ya kuleta hii bajeti ya uhalisia. Lakini nataka nimshauri Mhe. Waziri akija inaelekea Waheshimiwa Wawakilishi au bado na wananchi wetu hawajaweza kuijua vizuri hii bajeti halisia. Sasa aje awaambie ina maana gani na ina mtazamo gani, lakini baada ya kuielewa hii nafikiri wanaweza wakaipongeza wote kwa jumla.

Mhe. Spika, ilikuwa niseme hilo tu na ninakushukuru sana na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpendae naunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha mzima wa afya. Vile vile nampongeza Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuweza kuongoza nchi hii kwa ujasiri. Pia sina budi kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuleta bajeti hii ambayo ina kila nafasi ya kuweza kuhakikisha kwamba ina nafasi nzuri ya kuweza kuweka uchumi wetu sawa. Pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwa kuanza kuchangia ukurasa wa 66 kifungu cha 55 kuhusu maendeleo ambayo tumeyapata nchini Zanzibar hasa kuhusu barabara zetu za nchi hii kwamba zimeimarika. Sina budi kumshukuru au kumpongeza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa shughuli nzuri anazozitekeleza za mabarabara. Hivi sasa kwa kweli nchi yetu imeimarika sana hasa barabara zetu za mashamba ambazo zimeimarika vizuri sana. Tukiangalia kabla ya Mapinduzi ya nchi hii barabara ya kutoka Makunduchi hadi mjini ndivyo ilivyo kwamba ukitaka kuja mjini lazima ulale kwenye gari kuanzia usiku wa saa moja ili ufike mjini saa tatu asubuhi. Ukiangalia Nungwi halikadhalika ilikuwa hivyo hivyo utoke Nungwi tangu saa kumi na mbili ndio uhakikishe kwamba unafika mjini saa mbili asubuhi.

Pia, ukiangalia barabara zetu za Pemba zilikuwa hivyo hivyo, ukitoka Kiuyu hadi mjini unaweza kuhakikisha kwamba bora upande gari la punda utafika mapema kuliko ukapanda gari. Hivyo sina budi nimshukuru Waziri kwa kazi nzuri za barabara ambazo anaziimarisha kwa nchi yetu.

Kwa kweli hivi sasa vilio vya barabara vimemalizika sana nchini Zanzibar, yaliyobaki ni mambo madogo madogo ambayo ni kuziba tu nyufa ambazo zinatokea katika barabara zetu. Lakini kwa kweli tatizo la barabara kusema Zanzibar kipo kijiji ambacho hakipitiki hivi sasa nafikiri vinamalizwa. Ilikuwa barabara kubwa ambayo ina matatizo ni kutoka katika jimbo langu ni Unguja Ukuu/Chwaka na hivi sasa unaweza kupita barabara ya Unguja Ukuu ukakata pale Cheju na ukajihakikisha kwamba tangu alipokufa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliianza barabara na hivi sasa inamalizwa. Kwa hiyo sina budi nimpongeze sana Waziri kwa juhudi na kukumbuka yale aliyoyaacha Baba wa Taifa kwamba wanayaendeleza.

Mhe. Spika, kwa kweli ni mengi sana Serikali yetu inaendeleza kuyachukua ambapo yalikuwa zamani hayapo na sasa tumeona kwamba yanaendelea vizuri.

Nikienda katika Wizara ya Elimu. Mhe. Spika, Wizara ya Elimu hivi sasa imeimarika vizuri sana kwa sababu ninavyokumbuka mimi hapo zamani enzi yako Mhe. Spika na mimi ilikuwa hupati sekondari hadi uje mjini ndio unaweza kupata elimu. Na utakuta wananchi wengi kwa kipindi hicho kabla ya Mapinduzi walikosa elimu ya juu kutokana na kwamba Serikali ilikuwa haisomeshi mashamba au katika mikoa kuweza kuweka sekondari.

Leo kama utaenda Chokocho na sehemu nyengine unaweza kukuta sekondari. Kama utakwenda Nungwi, Makunduchi utakuta sekondari, wakati zamani tulizoea kwenda *Fidel-Castro* Pemba, ama uje Zanzibar ukute Lumumba. Lakini hivi sasa kuna majengo ya kisasa ya maghorofa ya sekondari katika mikoa tofauti, na zamani ilikuwa huwezi kupata sekondari katika mikoa au majenzi ya kisasa katika mikoa yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli ni mengi sana yameimarika tangu baada ya Mapinduzi na bajeti zetu zinaendelea vizuri. Kwa kweli hivi sasa tumeimarika sana, tuna mahospitali kila mkoa ama wilaya unakuta daraja la kwanza zipo katika wilaya zetu ama mkoa ambalo ni jambo adimu sana kabla Mapinduzi kuweza kuikuta hospitali ya daraja la kwanza laya. Kwa kweli sina budi nimpongeze sana Mhe. Rais kuhakikisha kwamba mengi ambayo ameacha Baba wa Taifa hakuyamaliza hivi sasa yanamalizika kwa pamoja akishirikiana na Waziri wetu wa Fedha kupanga uchumi vizuri ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana.

Kwa kweli Mhe. Spika, kwa muda mrefu sana hali ya Zanzibar ilikuwa ni ngumu sana eneo la giza. Hivyo nizungumzie mambo ya umeme kwa kweli nashukuru sana hivi sasa umeme umeimarika, nchi ya Zanzibar. Umeme kila sehemu utaukuta, hakuna mkoa wa Zanzibar ama wilaya hivi sasa ambayo haina umeme. Jambo ambalo lilikuwa adimu sana mtu wa mkoa au wilaya ama jimbo kabla ya Mapinduzi, ama ni ndoto hasa katika mikoa yetu ya mashamba.

Ukiangalia ndugu zetu wa Pemba walikuwa umeme kwao ni ndoto kabisa, walikuwa hawaujui hata unavyowasha taa. Nakumbuka kabla ya Mapinduzi ilikuwa ni jambo la ajabu sana kwenda Chake Chake au Mkoani ukakuta umeme, ukikuta nguzo ya taa labda utakuta karabai ndio imewekwa pale kwenye nguzo ya umeme. Hiyo sitetei lakini najua kabla ya Mapinduzi walioijua Pemba ilikuwa kabla ya miaka 50 umeme hamna. Leo ukienda Micheweni ilikuwa ni pahala pagumu sana kujua kwamba kuna umeme. Leo Micheweni utakuta umeme unawaka bila hata matatizo.

Mhe. Spika, nikichangia kuhusu masuala ya ajira naweza kusema katika ukurasa wa 26 kifungu cha (vi) kinazungumzia kuhusu suala la upatikanaji wa ajira bora hasa kwa vijana. Mhe. Spika, kuhusu suala la ajira kwa kweli hivi sasa ajira zimekuwa ngumu sana katika Serikali yetu, lakini utakuta ajira hivi sasa zinapatikana kwa shida sana, na utakuta kwamba hata zikipatikana ajira hizo zinapatikana kwa vijana wa mjini ama vijana kutoka Pemba. Lakini ajira kwenda kwenye mikoa ama kwenda wilayani hilo ni jambo adimu sana.

Utakuta unaajiri watu 50, 25 kutoka Unguja, 25 kutoka Pemba, lakini utakapojumuisha katika ofisi watu 50 watu 35 wote wanatoka Pemba, watu 15 tu ndio utakuta wa Unguja. Na hao wa Unguja utakuta vijana 10 wanatoka mjini, vijana watano tu ndio utakuta wanatoka katika mikoa yetu ya mashamba.

Mhe. Spika, kwa kweli ajira izingatiwe tena na ajira zitoke hivi sasa kwa mikoa, kila mkoa upewe ajira ya watu wake, kwa sababu sasa hivi hakuna mkoa ambao hauna sekondari, hakuna mkoa ambao hauna chuo. Ukija katika mkoa wangu mimi kuna vyuo viwili vya diploma na digrii, ukenda Tunguu utasoma, ukenda Chwaka utasoma. Iweje kwamba hivi sasa vijana wetu watoke mjini ama watoke Pemba.

Unakwenda katika ofisi unataka umwone mtu ambaye unamfahamu unatoka kwenye mkoa unashindwa unaona sura tupu za mjini, unaona sura tupu kutoka Chake Chake Pemba na sehemu nyengine. Sisi katika mikoa yetu unashindwa kuweza kumuomba mtu nisaidie hili. Kwa kweli hivi sasa viangaliwe vyeti vya vijana wanapokwenda kupatiwa ajira. Kila mkoa ahakikishe yule kijana ambaye amekwenda kweli amezaliwa katika mkoa ule, kama umezaliwa Mkoa wa Kusini kweli uoneshe umezaliwa Makunduchi, kama umezaliwa katika Wilaya ya Kati ujulikane kweli ni Wilaya ya Kati. Sio vijana 50 wanachukuliwa kwenye ajira lakini ukija ukitizama vyeti vyao vya kuzaliwa kutoka Chake Chake, Wawi na sehemu nyengine, hiyo inaturejesha nyuma.

Kwa kweli wananchi wetu wanapata tabu sana kupata ajira, na vijana wetu wanasikitika sana katika mikoa yetu kwamba hawapati ajira. Mhe. Spika, hilo ni jambo kubwa sana kwa vijana wetu na hivyo Serikali ipo haja kwamba kurudia upya ajira zinazopatikana hivi sasa.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya kilimo ama ya biashara. Kwa kweli Mhe. Spika, hivi sasa tuna matatizo makubwa sana kuhusu mambo ya kilimo kwamba nchi yetu hatuzalishi chochote kuuza nchi za nje, hilo ni tatizo kubwa sana. Ipo haja Mhe. Waziri ahakikishe anafufua mambo mengi kama kilimo ambavyo tulivyokuwa zamani tunakipatia nafasi ya kupata fedha za kigeni. Kwa kweli hivi sasa tuna matatizo makubwa dhidi ya karafuu, hakuna kingine ambacho tunakisafirisha nchi za nje na kuweza kupata fedha za kigeni. Utakuta kwa muda mrefu ilikuwa tuna ndugu zetu wa Muyuni walikuwa wanapeleka boribo nje na zilikuwa zinatupatia fedha za kigeni, lakini sasa hivi boribo zile haziendi hatujui kwa vipi akija hapa Mhe. Waziri itabidi atueleze upya, kwa nini sasa boribo hatuwezi kusafirisha nchi za nje.

Akija Mhe. Waziri atueleze kwa nini sasa hivi hatuwezi kupeleka mbata nchi za nje ambazo zilikuwa zinatupatia fedha za kigeni. Kwa nini hatupeleki pilipili hoho ambazo ni zao kubwa la Jimbo la Koani na Wilaya ya Kati ambalo ndio lilikuwa linatupatia fedha nyingi, sasa hatupeleki katika nchi za nje. Akija Mhe. Waziri atuhakikishie kwa nini mazao hayo hayapelekwi nje na yanaoteshwa sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, zaidi ya hayo naona muda uliobakia umekuwa ni mdogo sana lakini kwa vile ninazo dakika za kumalizia nizungumzie kwamba hivi sasa tuna matatizo mengi madogo madogo ambayo yanahitaji kurekebishwa.

Kutokana na suala la siasa kwamba imekuwa muda mrefu sasa watu wetu wanazungumzia siasa ndio kazi. Ni aibu kukuta vijana saa za kazi, saa 4 au 5 wamekaa katika vijiwe wanazungumzia siasa. Sasa utakuta kwamba nchi yetu badala ya kwenda mbele tofauti na mikoa yetu ya huko mashamba, si rahisi kukuta wamekaa vijana 10 kuzungumza katika vijiwe, labda wakati wa kwenda kwenye michezo hasa mpira ndio utaweza kukuta vijana.

Vijana wanashangaa hapa mjini, utakuta muda mwingi vijana wanakaa katika vijiwe kungoja pale kapita mwanachama wa Chama cha Mapinduzi ama kiongozi wanasema huyo huyo. Ile ni kutukana nchi, mimi ukitaka ni kiongozi, tena kiongozi shujaa na kiongozi mimi ni kiongozi kamanda naweza kuliongoza jimbo lagu, na jimbo langu linaniamini ndio likanichagua kuhakikisha kwamba nipo katika jimbo. Nawahakikishia vijana ambao wanakaa kuwatukana viongozi ole wao tutakapoamua na sisi kurejesha mapigo dhidi yao.

Tunasema wapo viongozi wa upinzani hatuwaogopi kurudisha mapigo upande wao. Tuhakikishe sisi ni viongozi wa kweli na tuna uwezo na tunajiamini na tunahakikisha nchi yetu, tutailinda kwa hali yoyote ile. Na tuna uwezo wa kulinda nchi hii tukawa salama kila wakati. Na wahakikishe kwamba sisi ni wazee wao, sisi tunakaa na wazee wao wasije kusema kwamba sisi ni wageni wa nchi hii. Sisi ni wananchi halali katika nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa hayo machache.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni kwa mashirikiano makubwa, kuendelea na mjadala kwa utulivu, pamoja na utelezi mchache mchache lakini hatimae tunakwenda kwenye mada ambayo ipo mezani. Nawashukuru sana.

Waheshimiwa Wajumbe, jioni nitakuwa na wachangiaji wanne tu na baada ya hapo itakuwa mjadala huu tunaufunga. Na kama kutakuwa na Wajumbe ambao wana lolote basi haraka wawaandikie Waheshimiwa Mawaziri kwa maandishi. Wachangiaji wetu wanne wa jioni ni pamoja na Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Assaa Othman Hamad, tutamalizia kwa kumsikiliza Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.

Hao ndio wachangiaji majina niliyonayo, wengine kama wana lolote basi wawaandikie Waheshimiwa hawa kwa maandishi. Wanne hawa ndio tutawasikiliza jioni na baada ya hapo tutamsikiliza Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora.

Waheshimiwa Wajumbe kuna tangazo moja. Waheshimiwa wafuatao wanatakiwa wahudhurie kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi ya UWAWAZA ambao watakutana katika chumba cha Kamati namba 3 mara baada ya kuahirisha kikao hiki. Waheshimiwa wenyewe ni Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Salma Mussa Bilal, pamoja na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Wakutane mara baada ya kuahirisha kikao hiki.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa tusitishe shughuli zetu hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Hamza Hassan Juma.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba muongozo wako kwa sababu leo saa saba kabla hujaahirisha Baraza letu ulitoa maelekezo kwamba Waheshimiwa Mawaziri wajiandae kuja ku-*wind up* hoja zetu, lakini vile vile, ulijaribu kuwataja Wajumbe kama wanne hivi ambao uliwataka waje wamalize mchango yao na waliobakia wapeleke kwa Mawaziri kwa maandishi.
Mhe. Spika, sasa kwa kuwa hii ni bajeti kuu ya serikali na bajeti hii kuu ndio imo msingi wa bajeti zote za mawizara yetu yote ambayo tutakuja kuyajadili hapo baadae, ingawa kwa mujibu wa taratibu zetu hatuwezi tukaweza kubadilisha mafungu kutoka wizara moja kwenda nyengine, lakini bado tuna nafasi kubwa ya kuishauri serikali yetu kuonesha ni maeneo gani ambayo tufanye jitihada na tuweke mkazo kwa ajili ya kuongeza mapato yetu au kuibua vianzio vipya.

Mhe. Spika, sasa ninadhani Waheshimiwa Wajumbe wote wamepata vitabu hivi vinne na ninaamini wametumia muda wa siku tatu tulizopewa kupitia na kusoma ili kuweza kuja kuishauri vizuri serikali.

Mhe. Spika, sasa mimi ninadhani kwa kuwa bado Wajumbe wengine wapo hawajachangia na naamini kuna maeneo mengi ambayo wanahitaji kuweza kuyatoa ushauri na kwa kuwa ratiba yetu kesho ndio ilikuwa ni siku ya mwisho kuja kuijadili na kuifanyia maamuzi bajeti kuu ya serikali.

Mhe. Spika, sasa ushauri wangu kwa sababu kila Wajumbe wengi wakipata kuchangia, wanampa nafasi nzuri Mhe. Waziri kumpa wigo mpana wa kuangalia ni maeneo gani ambayo ya kuja kumsaidia baadae kuja kukusanya kodi.

Mhe. Spika, katika ushauri wangu ninadhani ungeturuhusu Wajumbe wako waliobakia wakaendelea kuchangia kwa siku hii ya leo ili kesho asubuhi, Waheshimiwa Mawaziri moja kwa moja baada ya maswali na majibu waje watujibu hoja zetu mbali mbali.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilichukua karibu muda saa moja kujadili hoja mbili kwa maandishi na *still* sikuweza kumaliza zile hoja zangu nilizokuwa nazo. Hivi sasa kama utanipa tena muda wa ziada, nipo tayari kutumia dakika nyengine kama 60 bila ya kusoma kwenye kitabu, kwa sababu bajeti ya serikali ninaiona ninaichambua kama pesa, kwa sababu ni wizara zote ambazo matatizo yao ndio tunayoshughulikia huko katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naamini bado Waheshimiwa wanayo nafasi kubwa ya kuweza kutoa michango yao ili tukaitia nyama bajeti hii ya serikali, ili kutoa wepesi wakati wa kuja kupitisha wizara mbali mbali kuja kupata unafuu.

Mhe. Spika, mimi leo wizara moja tu Naibu Waziri alijaribu kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya zile hoja nilizozijenga, kwa kiasi fulani nimeridhika kwa sababu waliichambua ile ripoti yangu na wakaijadili na wakaweza kuitoa majawabu. Kwa hivyo, naamini na wengine vile vile wana michango kama ile ambayo Waheshimiwa Mawaziri watakuja kupata nafasi kuyatoa ufafanuzi ili kuja kuwapa wepesi wakati wa kuja kupitisha bajeti zao.

Mhe. Spika, sasa naomba utusaidie katika hili uwape nafasi Waheshimiwa Wajumbe waliokuwa ambao hawajachangia bajeti, basi waweze kuchukua nafasi hii wakamaliza michango ili kesho kuja kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, lakini la pili, kesho pia na mimi ninatakiwa kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Wenyeviti ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria za Kodi. Kwa hivyo, pia, nilikuwa ninahitaji nipate nafasi nzuri ya kuweza kumalizia, kazi kubwa nishafanya, lakini naamini kesho asubuhi nitapata nafasi ya ziada kuja kufanya marekebisho madogo madogo ili wakati wa jioni nije niisome ripoti ile baada ya Mhe. Waziri kuwasilisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kodi na mimi ninafikiri nitakuwa tayari nimeshapata nafasi nzuri ya kuja kuwasilisha ile ripoti kwa umakini mkubwa sana.

Mhe. Spika, sasa ninadhani kwa hoja zangu hizo ninaamini utazitilia maanani, basi utatusikiliza ombi letu ili sasa kutupa nafasi tuweze kuichambua bajeti ya serikali vizuri na kuweza kuishauri vizuri serikali yetu kwa ajili ya kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kuweza kunivumilia na kunisikiliza. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mashauri ya Mhe. Hamza Hassan Juma na mambo yake sio mabaya, ni mashauri mazuri sana. Nimepata Wajumbe 35 walioomba kuchangia na katika 35 hao wanne ndio wale ambao niliowataka kwamba watamalizia hivi jioni.

Waheshimiwa Wajumbe, jana ninafikiri Mhe. Hamza Hassan Juma ulikuwa hupo, lakini ilifika pahala ikawa sina Wajumbe na ikawa najaribu kuokotaokota. Ninakumbuka Mhe. Abdalla Mohamed Ali yeye nilimlazimisha baada ya kuona anahangaika hangaika, yule anataka kusema, nikamwita, ndivyo hali ilivyokuwa. Kwa hivyo, kimsingi Wajumbe walikwisha kuchangia vya kutosha na mpaka ninawataja wale hakuna Mjumbe mwengine ambaye aliyekuwa ameomba. Sasa jana uliniaga ukasema una shughuli fulani unataka ukafanye na ndio maana hukuona ile hali ilivyokuwa. Nikawahi kusema kwamba Mhe. Waziri hivi inaonesha tushadhirika, hiyo kauli niliitoa wakati jana wewe hupo.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa ndio wakajitokeza waliojitokeza, tumewasikiliza na kimsingi tumefika pahala si pabaya. Jumla yake Wajumbe ambao tumewasiliza nadhani ni idadi kiasi, 35 sio kidogo. Kwa hivyo, katika ile tafuta tafuta ile ndio nikapata Wajumbe wapatao 14, ile baada ya tafuta tafuta, lakini kimsingi baada ya kufikia 19 ilikuwa hamna wengine. Kwa hivyo, tukaokotaokota, ndio tukapata kama hivi 20, tena wengine tukamaliza muda wa jana na leo tukawaita mpaka tulipofikia.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo, nadhani idadi hiyo kwa mazingira inaonekana imefikia pahala si pabaya. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba ulikuwa unaniona ninaruka hapa na pale, kimsingi baadhi ya wale walioomba walikuwa wala hawamo. Hivyo, sasa ikawa ninatizamatizama nani yupi nimwite yeye, mwengine namuacha kwanza mpaka tukafikia pale ambapo tumepofikia.

Waheshimiwa Wajumbe, idadi ya Wajumbe tuliopata na michango yenyewe namna inavyokwenda, nadhani inafikia pahala kwamba tumeridhika, tumefikia pahala si pabaya.Kwa hivyo, bajeti zinazokuja huko, maana munaposema inaonekana kuna baadhi ya maeneo mutahitaji muda zaidi, nitakuja kuutoa wapi?

Waheshimiwa Wajumbe, sasa hapa pahala ambapo inaonekana kwamba tumefikia pahala kidogo tumeridhika, basi hakuna ubaya ku-*save* muda ukaja ukatumika huko, maana tunaelewa mambo yanavyokuwa hapa ndani. Kwa hivyo, yanahitaji muda, ninataka mambo haya *smoothing democratical* na kila mmoja aweze kuridhika kwa kile ambacho kinaamuliwa humu ndani.

Waheshimiwa Wajumbe, hivyo, tulipofikia pia si pabaya na ndio maana ikawa kumekuwa na uhaba mkubwa wa Wajumbe mpaka pale nikatoa kauli ile.

Waheshimiwa Wajumbe, nakuombeni tuendelee kwa utaratibu ambao tumejiwekea pale asubuhi na kutokana na hivyo, basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Bikame Yussuf Hamad. Baada ya hapo Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mungu kwa kunijaalia afya njema nikaweza kusimama hapa na kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba hizi mbili zilizowasilishwa katika Baraza lako tukufu, lakini pia, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais Mstaafu Amani Abeid Karume pamoja na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad ambaye kuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa nini nianze kuwapongeza viongozi hawa, ninawapongeza viongozi hawa kwa makusudi kutokana na hali tuliyokuwa nayo ya kisiasa miaka ya karibuni. Sasa viongozi hawa wanastahiki kupongezwa sana na ukilinganisha na matokeo mbali mbali yanayojitokeza hivi sasa, likiwemo suala moja ambalo kuwa lilizungumzwa hapa kuletwa wa kuondolewa Serikali hii ya Umoja wa Mataifa (*GNU*). Kwa hivyo, mimi ninasema tunauomba mswada huo uletwe na tutaupokea kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini tujue kila mwenye kuomba balaa, basi akumbuke yeye mmoja wapo litakalomfika wa mwanzo na yeye anayeomba heri, basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia heri ile tufaidike sote.

Mhe. Spika, kwa sababu tunajijua hali tuliyokuwa hapo nyuma, hali ngumu ya kisiasa tuliyokuwa nayo, tulikuwa hatutembeleani, hatuzikani, lakini baada ya matokeo haya, viongozi wetu hawa wawili wakaona hakuna haja ya kuendelea na matatizo haya isipokuwa ni kuunda Serikali hii ya *GNU*. Kwa hivyo, kama kuna mswada unataka kuletwa katika Baraza hili tunaukaribisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niingie katika kitabu hichi cha Mhe. Waziri wa Fedha. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kwa hotuba yake aliyoitoa ya bajeti ya Serikali ambayo sote tuliisikia. Kwa kiasi fulani mwenyewe amesema kuwa katika ukusanyaji wa mapato taasisi nyingi zimevuka lengo. Hivyo, tulitegemea kuwa utendaji katika wizara mbali mbali utakuwa na mafanikio mazuri, lakini jengine alizungumzia kuhusu masuala ya mishahara kuwa kipindi hichi hawatoongeza mishahara, lakini ninachomuomba Mhe. Waziri aangalie sana muhimili mmoja mkuu wa serikali ambao ni suala zima la Mahakama, kama yeye ni Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, katika muhimili huu kumekuwa na matatizo mengi na changamoto nyingi hasa katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakimu wake. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri katika hili asiongeze mishahara, lakini huu muhimili huu auangalie kwa jicho la huruma sana ili watendaji hawa waepukane na mambo ya kuchukua rushwa. Changamoto wanazo nyingi hasa suala zima la usafiri kufikilia katika vituo vyao au Mahakimu hawa kufikia katika vituo vyao vya kuendeshea mashtaka.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kuwa Mahakama ni muhimili mkuu wa nchi, lakini pia, ndio unaotoa haki katika nchi yetu. Kwa hivyo, kuendelea kuwepo changamoto nyingi kwa watu kama hawa ni tatizo, si vyema watu kama hawa kukosa hata usafiri wa kufikia maeneo ya kazini wanapokwenda na wanamopangiwa na badala yake kuingia ndani ya madaladala, kitu ambacho kinaweza kikasababisha matatizo.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika kitabu cha hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora. Niendelee katika utekelezaji wa maeneo yaliyopewa kipa umbele.

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze na yeye Mhe. Waziri kwa hotuba yake na mipangilio yake ambayo amejipangia. Tukianza katika maeneo ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele, kwanza niende kwenye *paragraph* ya 47 ambapo kuwa kumeandikwa kuimarisha sekta ya viwanda. Juhudi hizi za kuwavutia wawekezaji wa viwanda nchini pamoja na kutoa vivutio maalum kwa wawekezaji wa sekta hiyo ikiwemo miundombinu ya barabara, umeme na maji.

Mhe. Spika, maeneo haya siku zote yanazungumzwa na siku zote, ni maeneo yanayopewa kipaumbele, lakini hatimaye yake utekelezaji wake hauonekani. Tuchukulie mfano kuna haya maeneo huru, lakini haya maeneo huru yamekuwa yanatajwa tu, hatuyajui utekelezaji wake ukoje, yamepangiwa vipi maeneo haya au yataanzia wapi na kumalizikia wapi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri katika utekelezaji huu wa maeneo yaliyopewa kipaumbele, hebu aje atuelezee katika suala zima la maeneo huru yaliopo Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini suala jengine ni kwenye *paragraph* ya 48, kuna kuimarisha sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, siku zote sekta ya kilimo inaimarishwa, wala hatujaona hiyo hatua inayofikiwa, lakini mimi ninataka nisema kuwa katika suala hili Mhe. Waziri ametwambia ni kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji na hapa kaandika kuwa umwagiliaji maji kutoka *metres 500* kufikia *metres 800*, lakini ukiangalia kuna haya mabonde ambayo yaliyokuwa yameshaanzisha zamani ambayo kuwa mengine hawajaanzisha wao, lakini yana changamoto nyingi.

Mhe. Spika, maeneo hayo mengine hayakidhi haja hayo ya umwagiliaji maji, miundombinu yake ni mibovu, hakuna ukarabati wowote unaofanywa katika maeneo hayo. Sasa kama yale mabonde ambayo yameshaanzishwa zamani hayashughulikiwi, sasa haya mapya kweli tutaweza kuyaendeleza.
Mhe. Spika, lakini katika suala hilo hilo kuna suala zima la madawa ambayo serikali wanadai kuwa kuna punguzo la mbolea. Mimi ninaloliona punguzo kubwa la mbolea liliopo ni mbolea ile ya Urea, lakini kuna zile dawa za magugu ambayo dawa ile ya magugu inatoka *litre* shilingi kumi na mbili mpaka kufikia *litre* shilingi elfu ishirini, halafu kuna dawa ile ya wadudu wa wale wa *hispa*, ile ni shilingi 30,000 tangu mwanzo na mpaka hivi sasa. Sasa punguzo hilo kama dawa hizi hazipatikani na wananchi wetu kama tunavyowajuwa hali zao, hicho kilimo cha umwagiliaji maji kweli kitaendelea.

Mhe. Spika, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atueleze amekusudia nini kufanya katika sekta hii ya kilimo? Lakini jengine katika kuimarisha huduma ya afya, mimi nataka nichukuwe fursa hii kumpongeza katika kuongeza ujenzi wao wa Hospitali inayoendelea, Hospitali ya Micheweni katika wodi ya wazazi, ni sawa ziongezwe wodi ili tujenge Hospitali, lakini je, hizo Hospitali zilizopo mahitaji yanapatikana?

Mhe. Spika, bado tuna tatizo hili katika Hospitali na vituo tunavyo vingi, lakini ukosefu wa madaktari bado unaendelea, madawa bado yanaendelea kuwa hayako Hospitalini na Hospitali nyingi hasa hizi Hospitali za wilaya tuliambiwa hapa katika hotuba ya Rais kuwa zitapandishwa daraja. Sasa tuone kuwa kuna mambo muhimu tuyapate katika ile Hospitali pale kama Hospitali ya wilaya, tuambiwe kwa kupandishwa daraja tumefikia wapi? Lakini siku zote tukiendelea kuwa Hospitali hizi majengo yanaendelezwa, lakini pale Micheweni wakiwa wanataka kung'olewa jino hapana daktari, uende ukatowe shilingi 5,000 uende kwenye hospitali za watu binafsi ukang'olewe jino.

Mhe. Spika, kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba sana katika mipango hii, basi tuwe na umakini wa hali ya juu tujenge, lakini tuangalie na mahitaji mengine ambayo kuwa ni muhimu kupatikana katika Hospitali zile hasa za wilaya.

Mhe. Spika, suala jengine kuna upatikanaji wa maji safi na salama. Kifungu cha 58, Mhe. Waziri amesema; matengenezo ya miundombinu ya usambazaji wa maji safi kwa ajili ya kuzuwia upotevu wa maji yameshaanza katika vijiji fulani. Nataka nimwambie Mhe. Waziri, kuwa mpango huu unaowekwa ni mzuri, lakini yale maji safi na salama yapatikane.

Mhe. Waziri, tulilalamika sana hapa katika kijiji kimoja cha Tumbe kuwa upatikanaji wa maji katika kisima kile maji yake hayafai, maji yake sio katika maji mazuri, lakini kinachoendelea ni kwenda kufungiwa mita pale tulipie maji kwa bei kubwa, lakini tunatumia maji ya visima kwa matumizi mengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hilo pia ulione kile kisima mtakifanya vipi ili tuweze kupata hayo maji safi na salama?

Mhe. Spika, niende katika muelekeo wa Programu za Mradi. Mhe. Spika, programu hizi za miradi zimezungumzwa sana na zimeelezwa sana na Wajumbe wengi, lakini ni miradi hii tangu tulipoingia katika Baraza hili, ujenzi huu wa mabarabara haya ya Ole Kengeja, Wete Gando siku zote yamo ndani ya vitabu wala hatujajua hatima yake ni ipi, hiyo barabara ya Konde na Wete imeshatiwa fusi zinafika mara 20. Hivi sasa gari halipiti.

Mhe. Spika, sasa kama serikali haijawa tayari, bora waachie zile barabara ziwe vile vile, kuliko kuleta yale matengenezo yakachukua muda mrefu, kwa sababu inapofika wakati wa kiangazi, basi njia zile huwa hazipitiki kwa vumbi. Kwa hivyo, tusitafute matatizo ambayo kuwa hatujawa na uwezo nayo kufanya shughuli hii, tukaendelea kuyatifua majia na hatimaye kuleta madhara kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine nataka nimuombe Mhe. Waziri katika programu hizi za miradi. Kulikuwa kuna mradi mmoja wa uhakika wa chakula na lishe ambapo mara hii katika kitabu hiki sijauona, ilikuwa ni hadithi mpaka imetosha.Uhakika wa chakula na lishe tunakarabati mahala, tunajenga ofisi, sijui tunapewa nini. Sasa hebu waje watuambie uhakika wa chakula na lishe umefikia wapi? Maana mbio za sakafuni huishia ukingoni. Sasa aje atuambie Mhe. Waziri, umekwenda wapi, maana mara hii siuoni kwenye kitabu. Sasa kutafuta mambo makubwa hatuna uwezo nayo, tukayatafuta mambo tukayajaza humu ndani ya vitabu, halafu hatimaye yakatushinda njiani.

Mhe. Spika, yakishatushinda njiani, tunaona tabu hata kuyaandika humu kwenye vitabu. Kwa hivyo, huu mradi wa uhakika wa chakula na lishe, mimi niliposikia kwenye mradi huu nilitegemea mambo mazuri. Zanzibar kuna uhakika wa chakula na lishe, nikaona haya mambo mazuri, humu ndani ya hiki kitabu mara hii sijauona. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anieleze mradi huu wa uhakika wa chakula na lishe, ule ukarabati wa mahala umefikia wapi au tayari vyakula vimeshahifadhiwa huko? Hilo ni moja.

Mhe. Spika, lakini jengine la mwisho kuna suala moja la mradi mmoja wa ule mkonge, nalo pia sijalisikia kuzungumzwa, mkonge sijui ndio dude gani hilo. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja anieleze hili suala la mkonge nalo limesimamia wapi au umeshafanikiwa, kama umefanikiwa, basi tuambiwe, maana naona humu mara hii sijaona. Kwa hivyo, hii miradi ikishafanikiwa tupeni taarifa.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana. ilikuwa baada ya Mhe. Asaa Othman Hamad, nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma, lakini yeye ameondoa jina lake ameridhika na michango iliyopita. Kwa hivyo, namkaribisha sasa Mhe. Asaa Othman Hamad na baada ya hapo tumkaribishe Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema yake ya uhai tukaifika bajeti hii ya mwaka huu bado tuko salama *Inshaallah* atuwafikishe tufike na ya mwakani mpaka tuwafikishie Wazanzibari mahali stahiki kwenye uchumi wa nchi yao na matarajio yao ya muda mrefu.

Mhe. Spika, niwapongeze wenzangu waliotangulia kuichangia bajeti hii, wamefanyakazi nzuri na ni matarajio yangu serikali imesikia vilio vya wananchi namna Wawakilishi wao wanavyowawakilisha.

Mhe. Spika, bado tuna tatizo la uchumi na tatizo hili tunavyoliona sisi huku nje linakuwa siku hadi siku, haidhuru wataalamu wetu na mimi wala sitaki kubishana nao nawaheshimu sana na naamini wanafanyakazi nzuri sana. Napata mashaka makubwa sasa tatizo liko wapi? Maana wataalamu wapo wazuri, serikali iliopo madarakani tunaambiwa ni sikivu, hivi haisikii kutoka kwa wataalamu ama wataalamu wamefikishwa wapi?

Mhe. Spika, nayasema haya mwenzetu Saidina Omar tuko naye humu ndani na muda mwingi tumekaa naye tukamwambia kwamba kwa namna ya kumshauri, hebu fanya tupate angalau siku tatu tukaye mahali, Waheshimiwa Wawakilishi hawa wana miono mingi, uzoefu wa muda mrefu, tukichanganya na wale wataalamu wako tunaweza kuiambia serikali neno na baada ya hapo labda kwa sifa tunayoisikia ya usikivu huwenda tukaondoka hapa tulipo. Saidina Omar mimi ni mwenzangu wa karibu sana, sijui ombi langu hili na la wenzangu limekwama wapi? Ugumu uko wapi?

Mhe. Spika, nakuambia ni mwenzangu. Hivi karibuni alikuwa na safari yake nje ya nchi hii. Saa 8:25 usiku, ananipigia simu sasa nashuka ndege kiwanja fulani, ama niliamka kwa *message* yake ya simu. Hali ya namna hiyo napata kigugumizi, hili mbona ni gumu na hili ni la nchi? Hizi simu na ujumbe ule wa simu ni mimi na yeye.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema bado wananchi wa nchi hii tunahangaishwa na suala zima la uchumi, bado wananchi wa nchi hii uchumi huu unaotajwa ndani ya vitabu hivi tunawaomba wenzetu sasa waielekeze serikali tuwe na uchumi shirikishi ili uonekane kwa wananchi. Haiwezekani mwananchi anapata mlo mmoja kwa siku.

Mhe. Spika, hii hali nadhani sote humu ni mashahidi namna wananchi wetu maisha yanavyokuwa magumu huko nje, namna vijana walivyokosa ajira.

Mhe. Spika, miaka 30 nyume iliyopita kumuona mama wa Kizanzibari akibebe sufuria, moto na vikaango na kila kitu kichwani anahangaika barabarani kutafuta rizki, leo tunawaita mama lishe, mambo haya hayakuwepo. Sasa kitabu hiki unapokisoma kwamba uchumi umekuwa kwa kiasi hiki, lakini bado hadhi yetu ndio hiyo. Watafsiri wa kutafsiri uchumi watafahamu, lakini walengwa wa uchumi wenyewe wataendelea kutokufahamu.

Mhe. Spika, vimetajwa vipaumbele kwenye kitabu hiki cha swahiba wangu Saidina Omar, pametajwa elimu na afya. Nitarudia kusema kwamba na bahati nzuri vitabu hivi ni vya watu wawili, wote ni watu wangu wa karibu mno. Dkt. Mwinyihaji Makame na huyu Saidina Omar bin Yussuf bin Mzee. Hawa watu sio tu kwamba wana taaluma kubwa, lakini 'kuaga nchi ni kujua nchi' ni muda mrefu wenzetu wanapata nafasi ya kuona dunia ya wenzetu. Mimi huwa namuuliza Dkt. Mwinyihaji Makame, hukereki kuziona hizi barabara zetu hivi zilivyo?

Mhe. Spika, jana napita darajani kinamama wale wanafyagia vumbi mtindo mmoja, vyakula vimewekwa pale pembezoni, watu wanaotoka kule Mnazi Mmoja Hospitali. Nikasema *Yarrabbi Stara*. Hiyo dengue sijui nini iliyoingia huku sasa hivi, haijulikani inaingia vipi na vumbi hili. Ninachosema Sheikh Omar, afya ya binadamu ni muhimu katika masuala ya kujenga uchumi, tukipunguza tatizo la magonjwa, basi tunapunguza matumizi ya serikali.

Mhe. Spika, wananchi wakiwa na afya njema, basi hawa ndio wazalishaji wa uchumi, wananchi hawa maradhi matupu leo hapa, tunaimba uchumi utokee wapi?

Mhe. Spika, tukija kwenye elimu, hii elimu yetu tunakaa tukajiuliza tumefikia wapi? Elimu hii ya Zanzibar leo serikali kwa nia njema imetanua, sekta binafsi na wao mashule yao, lakini tunayasimamiaje kama serikali? Kwa sababu bado serikali ni dhamana, leo majina mazuri *International*, *International* hiyo elimu inayotolewa huko, kweli ni *International*. Waziri wa Elimu hili unalifuata na unalijua, siku yako itafika tutakuja kukuuliza maswali.

Mhe. Spika, kilimo, bado nitarudia kusema, tutaweza kujitaja kwenye kilimo kwa hapa tulipoelekezwa na Mwenyezi Mungu. Hii ni *Spice Island*, tulimeni *spices*, lakini tuzilime *spices* kileo, tulibakishe jina letu duniani kwamba Zanzibar ni *Spice Island*, sio hivi tulivyofanya sasa na tunavyoendelea kufanya. Haya yaliomo ya umwagiliaji maji, sijui heka elfu ngapi? Hii ni hadithi tu.

Mhe. Spika, hutamwagilia maji, narudia hutoweza leo Zanzibar hii na geographia yake tukaja tukajilabu tunamwagilia maji ili tuzalishe kilimo, kweli hizo ni ndoto za alinacha. Tutakachoweza kujilabu kwenye kilimo

nakuambia tena ni kwenye *spices* na matunda, huko kuanguka kwenye *green houses*, tutaweza kusafirisha tani na tani, wataalamu wamo humu ndani.

Mhe. Spika, mwenzangu kasema tusiyataje mambo ambayo hatuyawezi yametupita kimo, hayo mambo hatuyawezi na sisi kimaumbile Zanzibar haikuumbiwa huko.

Mhe. Spika, uchumi wetu uko baharini kwa asilimia zaidi ya 70, tuitumie bahari. Kulitajwa bandari ya Mpigaduri, Sheikh Omar Yussuf anatuambia hatujachelewa, hivi ni mpaka lini mpaka tuamini hatujachelewa sisi?

Mhe. Spika, hivi Bagamoyo ijengwe bandari matayarisho yanayoendelea hivi sasa, Mwambani Tanga ijengwe bandari, Mombasa wanaifanya *extension* ya bandari, hivi hatujachelewa kweli? Mbona tuna lugha za namna hii? Hicho kidogo baada ya yote kinafika kwa walengwa.

Mhe. Spika, nchi inanuka kwa rushwa hii, kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi, tunaendelea kufanya kosa, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mahesabu ya Serikali kinasomwa hapa, halafu tunabariki ule wizi tunapeleka tena bajeti mpya, watu wakaibe tena, tunawatendea haki Wazanzibar hivi tunavyofanya? kwa nini ripoti ya Mdhibiti Serikali haichukui hatua kwa wale wahusika?

Mhe. Spika, walipa kodi hawa ni hawa mama lishe, walipa kodi hawa ni hawa wamachinga, tunakamua hawa watu masikini, ndio kodi hiyo inayofika mikononi, tunaachia Makampuni ya mabilioni misamaha ya kodi isiyo kikomo, hiyo leo *good Friday,* sijui *morning* nini? Lugha tele alimradi pasilipwe kodi, hawa watu wa kuwaachia wasilipe kodi, ndio wanaokamuliwa Mhe. Spika, nimeona eneo hili.

Mhe.Spika: Mheshimiwa Asaa Othman Hamad una dakika tano.
Mhe. Assa Othman Hamad: Mhe. Spika, nashukuru nitamaliza milioni kumi kumsajili mfanyabiashara, ni pesa ndogo mno, mtizame mfanyakazi anayelipwa shilingi laki moja na sabini, mtizame mchuuzi wa samaki anayepato laki nane kwa mwezi, mfanyakazi huyu amesameheka kodi, milioni kumi unamlipisha kodi halafu tunasema tunaifungua *Private Sector,* ajira hakuna watu wanajiajiri wenyewe, huko tukiendelea kuwakamua namna hii, hivi kweli tunawatakia mema hawa Saidina Omar nataka na mimi uje unipe nilikuuliza mkonge wa Taifa vyereje na Wizara ya Fedha badala ya kukaa mawasiliano, siku ile ulinipa majibu uliyonijibu kitabu hiki hakikugusa mkonge wa Taifa, leo nakuomba majibu yangu mie liwe suala la kwanza.

Mhe. Spika, Pencheni ya wazee, Mheshimiwa haikutajwa kwenye kitabu, wazee hawa wameitumikia nchi hii kwa nia safi kabisa, michango yao tunaiheshimu, serikali ione kwamba pencheni ya sasa hivi hii imepitwa na wakati, watizamwe upya, Mhe. waziri, hebu fanya jicho la hisani kama huruma haipo tena, tukubali kwamba wametufanyia hisani hawa watu, wazee wetu wamefanya kazi kubwa hii.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema hivi nyimbo mbaya hachombezewi mtoto, Wazanzibari kwa imani yao ama imani zao walifuata kule walikoelekezwa, sasa ni vizuri wakasema yaishe na yakaisha,wakakubaliana tukae pamoja tule pamoja tuowane sasa, tuzikane na tushikamane kwenye kamba aliyoitaja Mwenyezi Mungu, bahati mbaya sana la kusikitisha hata wale waliosimama kusimamia lile la kheri, leo wanasimama tena kuhubiri shari.

Mhe. Spika, una dhima, wewe ndio unayetuongoza una mwenzako Dk. Ali Mohammed Shein, kuna mwenzio Jaji Mkuu kwa nafasi yake, nadhani yanayoendelea sasa mpaka unashauriwa utuchafue tuwe hivi tulivyo na tusiwe hivi tena, hivi tunakwenda wapi? Wazanzibari ndivyo walivyotaka wao wenyewe kwenye Mamlaka ya nchi hii tuishi hivi tulivyo, hizo hasama, balaa, ndwele na nini, basi Mungu atusamehe.

Mhe. Spika, leo unaonyeshwa mkoba kwamba kaamuriwa mtu alete mswada humu ndani, umeonyeshwa hivi humu ndani, mimi nataka nikuonyeshe tena miwili zaidi, ukiletwa mmoja, tutaongeza miwili, Waheshimiwa wetu ni nyinyi, Wazanzibari wamesema hili basi hawalitaki kama kuna watu na utashi wao ni wao wenyewe na *Inshaalla* Mwenyezi Mungu nia zao wanazijua wao na hakimu ndiye yeye, wala hatutaki kumfundisha sie.

Mhe. Spika, mimi nasema tu na wewe utaulizwa, kwa mapenzi yangu kwako ndio nikasema, halahala mti na macho yaliyopita yamepita wala tusiyaombe, kuna watu wenyewe hawajijui, Zanzibar hii hawaijui wanacheza ngoma wasiyoijua na zumari ikinyamaza ndani ya ngoma, watu wanatawanyika.

Mhe. Spika, nimejaribu kuzungumza kijitu kizima nikiamini unanielewa, nawaomba Wajumbe turudi tushikamane na tupendane, Zanzibar ni ya Wazanzibari waliokuja na mji wao watarudi wenyewao.

Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Spika: Sasa nampisha Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na nimepata ombi kutoka kwa Waziri wa Kilimo kwa ajili ya kufafanua baadhi ya mambo, Mhe. Shamsi karibu sana.

Mhe. Shamsi Vuai Nahodha: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali Mpango, mimi nitazungumza kwa kifupi sana mambo manne, kwa sababu mambo mengi yameshazungumzwa. Kwa hivyo, nisingependa sana kurudia rudia yaliyokwisha kuzungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe kwa ufanisi sana na kwa ufasaha.

Mhe. Spika, la kwanza utakumbuka katika awamu ya sita kuliundwa sheria inayohusu ada ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi, wawekezaji na hasa hasa kwenye sekta ya utalii wanakatwa kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya kuchangia fedha za mfuko huo wa kukuza ujuzi, wakati awamu ya sita inahitimisha muhula wa mwisho katika mwaka wa fedha 2010/11, mfuko huu wa kukuza ujuzi ulikuwa na shilingi bilioni tatu, napenda kumuuliza Mhe. Waziri katika kipindi cha miaka minne mfuko huu umekusanya kiasi gani na vijana wangapi wamenufaika na mfuko huu? Tunapenda kupata majibu ya masuala haya kwa sababu juzi nilipata taarifa zinanitatanisha kidogo, nimesikia fedha za mfuko wa kukuza ujuzi hivi sasa zinatumika katika kuwafundisha wanafunzi, wanaochukua Shahada za kwanza na Shahada za pili.

Mhe. Spika, sina tatizo na kuwasomesha vijana kwa sababu ninaujua umuhimu sana wa elimu, tatizo langu hatuwezi kufanya jambo zuri kwa kuvunja sheria kwa sababu mfuko huu umeanzishwa kwa shughuli maalum, kazi yake ni kuwaelimisha na kuwapa ujuzi vijana wetu ambao wanajifunza katika chuo cha utalii ili kuongeza ujuzi pamoja na vijana wanaojifunza katika taasisi mbali mbali zinazohusiana na masuala ya mafunzo ya amali.

Mhe. Spika, sasa leo tukitumia fedha za mfuko huu kwa ajili ya wanafunzi wa chuo kikuu, mimi nadhani hili si sahihi. Kama wahusika na serikali inadhani bodi ya mfuko wa elimu ya juu ambayo kazi yake ndiyo kuwapatia elimu vijana wetu, elimu ya Shahada ya kwanza na kuendelea, fedha hizi hazitoshi, basi naomba sheria hii iletwe itafanyiwe marekebisho ili sasa tuigeuze ifanye shughuli nyengine, lakini kuendelea tu kimya kimya, narudia tena, mimi nadhani jambo hili si sahihi na tusivunje sheria kwa kufanya jambo jema.

Mhe. Spika, jambo la pili, kilimo kina mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu na kilimo kinatoa ajira kwa zaidi ya asilimia sabini ya wananchi wa Zanzibar. Naishukuru sana serikali kwa kutoa ruzuku na kuendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya wakulima mbali mbali. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa kilimo na kutokana na mchango wa sekta ya kilimo, mimi nadhani serikali inapaswa kutoa ruzuku kubwa zaidi kutenga fedha nyingi zaidi kuliko inavyofanya sasa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia hapa katika mwaka wa fedha unaomalizika 2013/14, serikali imetoa mbolea karibu tani 150 na kutokana na ruzuku hiyo ya mbolea kiasi kidogo hicho tulichokitoa, yamepatikana mafanikio makubwa sana, tumepata taarifa hapa tumeongeza uzalishaji wa kilimo cha mpunga kutoka tani 6000 mpaka 33000, sasa kiwango hiki kama takwimu hizi ni sahihi, basi nasema kiwango hiki si kiwango kidogo sana na kwa maana hiyo tunaiomba serikali basi iongeze fedha zaidi.

Mhe. Spika, eneo la pili, naiomba serikali iweze kuweka mkazo mkubwa zaidi eneo la kilimo cha umwagiliaji maji, mtakumbuka serikali imetenga eneo la hekta elfu nane ambalo linafaa kwa ajili ya shughuli za kilimo, lakini kwa bahati mbaya sana kwa takwimu ambazo tumepewa hapa hazitupi matumaini makubwa sana juu ya kuendelea kwa kilimo hiki, maana leo ikiwa tumeongeza eneo la umwagiliaji maji kutoka mita mia tano mpaka mia nane, nafikiri itachukua karibu miaka arubaini kumaliza eneo hili la hekta elfu nane, sasa sina hakika kama Mhe. Waziri, amekusudia mita, hekta au eka, sina hakika, lakini kwa vyovyote viwavyo nadhani kiwango hiki ni kidogo sana.

Mhe. Spika, suala la tatu, nchi yetu haina rasilimali nyingi kama zilivyobarikiwa nchi nyengine duniani, lakini kwa bahati nzuri Zanzibar ina binaadamu ambao ndio rasilimali kuu katika Taifa na hasa ukisoma dira ya maendeleo 2020 inatambua jambo hilo, kwamba moja katika dhamira yetu kuu ni kujenga jamii ya watu walioelimika, mwanafalsafa mmoja wa kichina aliwahi kusema maneno yafuatayo; "Ukitaka kupanga mipango ya mwaka mmoja,

panda maua, ukitaka kupanga mipango ya miaka kumi, panda miti na ukitaka kupanga mipango ya karne moja, somesha watu wako".
Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana sekta hii ya elimu pamoja na kutambua umuhimu wake kwa kutambua dira ya maendeleo 2020, bado serikali yetu haijawekeza kiasi cha kutosha, ukitembea maskuli huko, ama vifaa vya maabara ni vichache sana, ama katika baadhi ya skuli nyengine hata vifaa vyenyewe vya maabara pamoja na maabara hazipo, hatuwezi kuingia katika dunia hii yenye ushindani mkubwa sana, wakati tunaendelea kuipuuzia sekta ya elimu kiasi hicho.

Mhe. Spika, natambua sana serikali inakabiliwa na uhaba wa fedha, lakini kupanga ni kuchagua tu, yuko mtu mmoja aliulizwa ukipata uwezo utawekeza kwenye sekta gani, akasema elimu, akaulizwa mara ya pili, sekta gani, akasema elimu, akaulizwa mara ya tatu, sekta gani, akasema elimu, kwa mnasaba huo, basi tunaendelea kuiomba serikali yetu tukufu ifanye kila linalowezekana tuisaidie sana sekta ya elimu, hali si nzuri sana kama tunavyofikiria.

Mhe. Spika, sote kwa umoja wetu tukusanye nguvu ili tuweze kuimarisha sekta hii ya elimu. Juzi nilipata bahati ya kuzungumza na Mwakilishi wa Kampuni ya Shell, Kampuni ambayo imetiliana saini makubaliano ya ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya mafuta na gesi. Sasa katika mazungumzo yetu amenipa taarifa za matumaini kidogo, amesema Kampuni yao imetenga dola milioni moja kwa ajili ya kuwafanyia mafunzo maalum, walimu wa masomo ya Kiengereza na Hesabu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa nini wanafanya hivyo, wanasema Zanzibar kiwango chetu katika taaluma ya Kiengereza na Hesabati kiko chini sana na haya masomo mawili haya ndio msingi wa masomo ya sayansi. Kwa maana hiyo, wamedhani hatuwezi kuingia kwenye sekta hii ya gesi na mafuta bila ya kuandaa vizuri vijana wetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Elimu mimi ninafikiri tu apate nafasi ya kulifanyia haraka jambo hilo, mimi nadhani ni jambo la faraja sana.

Mhe. Spika, jambo la mwisho la nne.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Shamsi Vuai Nahodha: Mhe. Spika, nimewasikia wazungumzaji wengi hapa tangu juzi, wengine wanatamani Zanzibar iwe kama Singapore, wengine wanatamani Zanzibar iwe kama Mauritius, mimi sina matatizo na jambo hilo na ninahisi hili ni jambo jema na kama wengine wameweza, sioni kwa nini Zanzibar isiweze? Tatizo langu ni moja tu najiuliza, je, hili tunalolisema kama tunatamani Zanzibar iwe kama Singapore linatoka moyoni au linatoka mdomoni?

Mhe. Spika, mwaka 2004 nilipata nafasi ya kuwahutubia mabalozi katika eneo la Ngorongoro na wakataka nitoe tathmini juu ya hali ya Zanzibar na mustakbali wa baadae wa Zanzibar, nilisema maneno mawili na vizuri nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wanisikilize vizuri. Nilisema hivi Zanzibar inaweza kuwa na mwanga wa matumaini, Zanzibar inaweza kutoka kwenye matatizo ambayo tumekuwa tukikabiliana nayo kwa muda mrefu kama tutafanya mambo mawili.

Mhe. Spika, la kwanza, iwapo tutafanikiwa kuunda wakati huo 2004, Serikali ya Umoja wa Kitaifa na la pili, kuimarisha uchumi, hili la kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu limewezekana, tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na sasa hivi ni mwaka wa nne, lakini kwa bahati mbaya hili la pili, mimi naona hatujalifanya vizuri. Sasa wasiwasi wangu bila ya kuwa na Zanzibar yenye uchumi imara, Wazanzibari kila siku hatutakwisha kugombana, kwa nini?

Mhe. Spika, nitoe mfano mmoja hata kwenye familia zetu kama baba mwenye nyumba ana uwezo wa kuiendesha nyumba vizuri, basi watoto watamwita baba yao kwa jina la Kiengereza, watamwita *baby* hata baba hawasemi na yule mkubwa wao atatumia naye vile vile jina la Kiengereza, hatumii, sasa hii inaashiria nini? Mahali penye utulivu na amani panapatikana umoja, watu wanaaminiana, mahali ambapo uchumi unalega lega, watu hupoteza matumaini, watu hupoteza umoja, watu hupoteza mustakbali wa Taifa. Narudia tena nasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa itumie nafasi hii vizuri, tusipoitumia nafasi hii vizuri, wale watu ambao wana shaka juu ya jambo hili, watapata sababu, binaadamu siku zote anaishi kwa matumaini.

Mhe. Spika, sasa mimi nasema tu fursa tuliyoipata Mwenyezi Mungu aliyotujaalia hatujaitumia vizuri, watu wana matarajio na walitegemea tu tukiunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa *manna na sal-wa* itaanguka, baadhi ya watu walifikiria hivyo, lakini mimi ninafikiri zama hizo za *manna na sal-wa* hazipo tena, tulitengeneza au tuliratibu mipango ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili tuwe na utulivu, tuwe na amani ili kwa pamoja tutengeneze sera za uchumi zitakazotusaidia kuwa na Zanzibar yenye ustawi na maendeleo ili Wazanzibari waendelee kupata maisha bora na ya utulivu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo ili kufafanua machache kama alivyoomba.

Naibu Wziri wa Kilimo na Maliasili: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niseme machache ambayo yaliyozungumzwa ili kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza kuna suala ambalo limejitokeza jana katika mchangiaji Mhe. Mohammed Abdalla kuhusu malengo ya mwaka 2011/2015 kuhusu sehemu ya umwagiliaji.

Mhe. Spika, kwanza naomba Baraza lako tukufu litambue kwamba miundombinu ya umwagiliaji ni gharama kubwa mno, hili naomba watambue. Katika jambo lenye gharama kubwa ni miundombinu ya umwagiliaji.

Mhe. Spika, katika suala hili ambalo limejitokeza katika ujengaji wa mitaro mita 500 hata Mheshimiwa aliyechangia hapa alisema ni ujengaji wa mitaro mita 500 hadi 800. Kwa hivyo, mwaka jana ukiangalia ilikuwa ni mradi ambao uliofadhiliwa na *KOIKA*. Mheshimiwa ndio maana tukajenga miradi mitaro 500 ya saruji katika mradi wa *KOIKA*. Kwa bahati mbaya hatukupata pesa za serikali hapa, lakini pia, nasema imejitokeza na safari hii pia kuna mita 500 vile vile. Mheshimiwa hapa hizi mita 500 iliwekwa hapa kabla ya *ceiling*, tuliweka huu ujenzi wa mita 500, lakini kitabu chetu cha bajeti hatukuweka vile vile kwa sababu ya ukosefu wa fedha, lakini sio kwamba suala hili ambalo kama tulivyosema ni suala la gharama.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hivi karibuni tulitia saini katika mradi kwa wenzetu wale *Exim Bank* ilikuwa ni karibu ya wiki mbili nyuma zilizopita, wenzetu hawa kwa ajili ya ujenzi wa mitaro hii mita 2150. Kwa hivyo, kwa uwezo wake *Allah subhana llahu wataala* Mwenyezi Mungu akitujaalia nadhani tutapata mafanikio kwa hili.

Mhe. Spika, jengine lilizungumzwa sana suala la nerika. Suala la nerika ni suala ambalo ni mbegu kama mbegu ambazo zilivyo nyengine, ringa, *Super Becan* na *Super* India, ni sawa sawa na nerika. Kwa hivyo, nerika ni mbegu ambayo ilipokuja hata wakulima waliifurahia sana na mpaka leo bado mbegu hii inazalishwa, lakini katika kuzalishwa, mimi nakumbuka hapo nyuma kulikuwa kuna mbegu moja inaitwa kibawa, mbegu ya kibawa ilikuwa ikipendwa sana na siku ukimuona mzee kafurahi anachinja kuku, siku hiyo anapika kibawa.

Mhe. Spika, lakini mbegu hii Mheshimiwa ni mbegu ambayo wakulima wengi nao walikuwa hawapendi kuipanda kwa ila moja tu, mbegu tamu, mbegu inatia vizuri katika mazao yake, lakini wakulima walikuwa hawawezi kuipanda kwa sababu ni ngumu kupiga. Kwa hivyo, mkulima ana haki na yeye ya kuchagua mbegu haidhuru wakulima wetu katika kuipokea nerika waliipokea vizuri na wakazalisha mbegu, lakini mkulima huwezi kumng'ang'ania, lazima alime mbegu fulani.

Mhe. Spika, kwa hivyo, tatizo lilojitokeza katika mbegu hii, wakulima wengi wanasema kwamba hii mbegu ni ngumu kupiga. Utaikuta ni tatizo ambalo mbegu ya nerika ina mashuke mengi na inazaa kwa wingi, lakini mkulima anakwambia katika kuipiga ile mbegu kwa kweli wanapoteza nguvu nyingi. Kwa hivyo, hii ndio sababu iliyofanya wakulima wengi wanaikimbia kidogo kuitumia hii mbegu, ndio maana ikaonekana kwamba imeshuka.

Mhe. Spika, lakini bado mbegu ya nerika ipo na si kama mbegu hii inatumika wakati wa masika, inatumika katika sehemu za juu ambako kuna maeneo maalum ndiko inakotumika sana. Ni sababu hiyo tu kwamba mkulima huwezi ukamlazimisha kwamba lazima alime hii mbegu, keshakwambia ngumu kupiga na ni kweli ana haki ya kuchagua mbegu mwenyewe anayoitaka.

Mhe. Spika, lilizungumzwa pia suala la mabwana shamba ambao hawafiki katika sehemu za kilimo, ni kweli hili suala tuna upungufu wa mabibi shamba tunao. Ukipiga hesabu Pemba kuna mabibi shamba ambao walio kazini hivi

sasa 40, tuna upungufu 80. Unguja 182 tuna upungufu 27 ukipiga hesabu 107, lakini hata hivyo hivi tumeomba wafanyakazi ambao hawa mabibi shamba tupate 40 kwa mwezi huu pia tumeajiri 9. Kwa hivyo, tukipata na 40, lakini bado tuna upungufu mkubwa. Kwa hivyo, hawezi kutokana na upungufu huu, hali tuliyonayo inawezekana kuna sehemu nyengine kwamba hawafiki, kwa sababu bwana shamba mmoja au bibi shamba mmoja anapewa shehia 4, hii ni kweli inaleta usumbufu.

Mhe. Spika, tutajitahidi kuajiri na hasa tatizo hili liko Pemba, tuseme ukweli, kwa sababu kubwa inayojitokeza Pemba lile suala lilioko katika Wizara ya Elimu lililokuwa linapigiwa kelele na Wizara ya Afya na Wizara ya Kilimo lipo. Mheshimiwa ukishamchukua mwanafunzi ambaye unamsomesha hapa, akishamaliza kusoma akeshahitimu, unamuajiri, basi tayari mfanyakazi yule anaolewa kaajiriwa Pemba, akeshaolewa, ina maana maadam kama yuko Pemba anarudi aje akae Unguja, hili ni tatizo nalo tunalolipata.

Mhe. Spika, kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa na mara nyingi wanakuwa watu wao Waheshimiwa wanapenda kupenya mlango wa nyuma mwanangu kaolewa arudi hapa. Kwa hivyo, hili ni tatizo, ndio maana unakuta Pemba ndiko kwenye usumbufu mkubwa wa mabibi shamba. Kwa hivyo, hili ni tatizo ambalo tunakabiliana nalo na tutajitahidi kwamba kuona tatizo hili linapungua baada ya kuomba hawa 40 tupatiwe katika uajiri.

Mhe. Spika, baada hayo, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, *Allah Subhanahu Wataala* aliyeweza kunisimamisha hapa na ni kutoa ufafanuzi kidogo kuhusu suala la mfuko wa JK na AK, lakini pia, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii adhimu.

Mhe. Spika, pia, naomba nichukuwe nafasi hii kuwapongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala kwa hotuba zao nzuri na safi zilizopangika vyema. Naomba kabla sijatoa ufafanuzi niseme kwamba hotuba zote mbili naziunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nikianza na kutoa ufafanuzi, naomba niseme niwaambie Wajumbe kwamba mfuko wa JK na AK umetokana na fedha zilizotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete) na Mheshimiwa wa awamu ya sita (Mhe. Rais Dr. Aman Abeid Aman Karume).

Mhe. Spika, hawa walitoa kila mmoja shilingi milioni 600 na wakaufanya mfuko huu wa JK na AK kuwa na shilingi bilioni 1,200,000,000, fedha hizo zilipelekwa Benki ya Watu wa Zanzibar kama wao ndio dhamana wa kuzitoa zile fedha, lakini ilikubalika kwamba lazima kwa vyovyote itoe mikopo yenye thamani ya mara tatu zaidi. Hivyo, kwa vyovyote zitoke bilioni 3,600,000,000. Benki ya Watu wa Zanzibar ilikubali suala hili na mikopo ilitolewa kwa wananchi 756 Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, baada ya kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji, wananchi kiuchumi mifuko yote iliyokuwa ikiratibiwa na Idara ya Mikopo ilihamishiwa katika mfuko huo wa uwezeshaji. Kwa hivyo, naomba niwaambie kwamba mfuko wa JK na AK ulihamishiwa mfuko huu katika mfuko wa uwezeshaji kiuchumi na kupelekwa fedha shilingi milioni 600,000,000 na kukabidhiwa wateja wa mfuko huu wa JK na AK. Hivi sasa uko mfuko mmoja tu wa uwezeshaji kiuchumi umerithi wateja wote wawili hao wa JK na AK na kwa bahati nzuri sasa hivi tumeandaa muongozo maalum wa kutolea mfuko huu, yaani wa kutolewa mikopo kwa wananchi ili waepukane na matatizo madogo madogo ya kiuchumi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, naomba niseme kwamba mfuko huu tunategemea sana kutokana na utaratibu wake kwamba utakuwa mfuko endelevu.Wananchi watapatiwa mikopo na tutahakikisha kwamba wanairudisha mikopo ili wananchi wengine nao wapate kukopa.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe, sasa ni wakati muwafaka nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena nikushukuru kwa kunipa wasaa wa kufanya majumuisho katika hotuba yangu ambayo ilizungumzia Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015, lakini pia, tulitoa Maendeleo ya Hali ya Uchumi kwa mwaka uliopita.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana mwenzangu Mhe. Waziri wa Fedha ambaye baadae atakuja kuchukua ile ngwe ya fedha, lakini hata kunisaidia kwa yale mengine ambayo nimeyaacha kwa udhoefu wake.

Mhe. Spika, kwa kweli tumepokea maoni, mawazo na maelekezo mengi sana kwa Waheshimiwa Wajumbe waliyoyatoa kutuasa, kutuelekeza na kupanga hapa hapa, ile *process* ya kupanga imeanzia hapa. Kwa kweli maoni yao niseme tumeyasikia, tutayazingatia na itakuwa ndio kama kitendea kazi chetu cha kwanza kabisa baada ya kupitisha Mpango huu wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, nikianza na mwenyewe Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti tunamshukuru sana, niseme ningechukua muda kuichambua hii yake tu, nafikiri hiyo saa moja niliyopewa na Mhe. Spika, isingetosha, hii yake tu peke yake. Hii inadhihirisha wazi umakini wa Kamati ya Wenyeviti iliyoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tulikaa nao tukajadili kwa kina na wao wenyewe waliridhika kwa sababu hatukuwa peke yetu Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, lakini tulikuwa na watendaji wa sekta zote. Kwa hiyo, kama serikali nzima Mhe. Hamza Hassan aliiweka kwenye kikao kile, mengi aliyoyazungumza Mhe. Hamza Hassan Juma au Mwenyekiti wa Wenyeviti, niseme ni maoni au ni *observation* zake alizoziona *Field*. Pia, alizozipata kwenye majadiliano yetu. Kwa hiyo, mimi namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, lakini zuri zaidi kwa upande mmoja alikuwa *very specific* baadhi ya *issues*, alikwenda moja kwa moja. Sasa hizi namuomba sana sisi tutazipeleka kwenye sekta na *Inshaallah* wenye sekta wakija wakati wao watazi-*address* vizuri sana, hawatangojea aje awaulize tena. Ni imani yangu kwamba tutawagusia na watayatolea maelezo wakati huo. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti na alikuwa na *specific issues* nyingi.

Mhe. Spika, vile vile, namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwanza pale asubuhi alipojibu baadhi ya hoja na sasa hivi Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili naye alijibu baadhi ya hoja. Kwa ujumla Waheshimiwa wengi walichangia kama nilivyosema kwa lengo la kutushauri, kutuelekeza, kutukosoa na lazima tukubali. Unapopanga ukatekeleza, ndio unapoyaona makosa, kama hutekelezi, basi makosa huyaoni na lazima ukubali kukosolewa na sisi hilo tunalikubali moja kwa moja, yale mapungufu ambayo tumeyaona na kwa kweli mfano tuseme mipango yote inapangwa, sio na wizara yetu tu, mawizara mbali mbali na nchi mbali mbali, ingekuwa inatekelezwa asilimia mia kwa mia, nafikiri tungekuwa peponi kabisa.

Mhe. Spika, lakini ndio matatizo yapo na matatizo yapo mengi kwenye *capacity* ya utendaji, fedha na hali ya hewa, kuna mambo mengine huyatarajii yanakuja. Sasa hayo yote yanatokezea kwenye utendaji.

Mhe. Spika, kwa ujumla mimi na wenzangu tumeyaona kama mambo 13 ambayo Waheshimiwa wengi haya wameyagusa, niseme wameona wachangie au waulizie. Suala ambalo Waheshimiwa wengi waliuliza ni suala la uchumi, yaani kukua kwa uchumi, maana yake nini ? Na hali halisi ilivyo mbona hatuoni? Wengine wamelinganisha na Mauritius na kwengineko.

Mhe. Spika, suala la pili, ni suala la kilimo na hasa suala la mpunga wa umwagiliaji maji. Namshukuru kama nilivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa kutoa maelezo ya kina kabisa, lakini suala jengine ambalo Waheshimiwa wengi wamezungumza ni suala la uvuvi hasa Bahari Kuu. Pia, katika hii bahari yetu ya ndani matatizo ya zana, boti na mengineyo.

Mhe. Spika, lakini suala kubwa nalo Waheshimiwa wengi waliloligusia ni suala la miundombinu hasa ya bandari tena Bandari ya Mpigaduri. Haidhuru Mhe. Hamza Hassan Juma aligusia Chelezo kile cha Mangapwani na Bumbwini, hili tumelipeleka kwenye sekta kuna matatizo pale, mwenzangu atakuja kuligusia. Pale kuna matatizo ya kimazingira kwa maeneo yale, lakini niseme tu kwamba nalo tumeliona kweli ni suala muhimu, zito na tutalishughulikia.

Mhe. Spika, vile vile, Waheshimiwa wengi wameguswa na suala la barabara. Ninachotaka kusema nafikiri nyote mtakubaliana na sisi kwamba katika nyanja ambayo tumepiga hatua kubwa serikali yetu ni mawasiliano ya barabara. Sasa matatizo yaliyotokezea hivi juzi kwa mvua hizi za masika yale ni ya kawaida na siku zote lami na maji na *friction* ile ikitokezea, lazima utarajie mashimo. Kwa hiyo, *Inshaallah* Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Naibu Waziri baada ya mvua naamini wana mipango mizuri sana, kwa kweli huwezi ku-*repair* barabara wakati wa mvua, naamini kabisa *repair* nzuri itafanywa baada ya mvua.

Mhe. Spika, suala la elimu nalo limechukua mkondo wake, wingi wa madarasa, ubora wa elimu na idadi ya wanafunzi kwa mwalimu. Waheshimiwa wengi wali-*query* ile *ratio* iliyotolewa, tutaitolea maelezo kidogo na wenye sekta wakati wa bajeti watakuja kuelezea sababu kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Spika, lakini suala la zao la karafuu nalo pia watu wengi wameulizia wanataka kujua faida yake na mwenendo wake na juhudi ambazo serikali yetu inachukua. Suala la mwani, matatizo, maradhi, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, asubuhi pale alitoa jawabu kwa ufasaha kabisa tunamshukuru sana.

Mhe. Spika, suala jengine katika suala la uchumi, watu wengi walijaribu kutulinganisha sisi na Mauritius tunakwenda vipi? Mbona wenzetu wametupita na wamekuja juzi? Nitaelezea tu kwamba vigezo walivyotumia wao ni viwili tofauti nitaelezea kwa namna gani? Lakini suala la msingi jengine ambalo Waheshimiwa wengi wame-*observe* au wamezungumzia ni suala la *PPP*, lakini vile vile, suala la MKUZA, wengi wameuliza wengine hata wakatupa changamoto mbona MKUZA haufanyi kazi? Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba hapa tulipofika basi hizi ni juhudi za MKUZA, tena sio juhudi zetu peke yetu ni *Collective Afford*, hii ni juhudi yetu sote. Sote tulikuwa sehemu ya kupanga *Private Sector* na wengineo wote wamejumuishwa katika mipango, huo ndio mkakati wa siku hizi *Collective Leadership*, lakini *Participatory Approach* kwamba sote tunahusishwa kwenye jambo linalotuhusu. Huo ndio mtizamo wa kileo, hupangi peke yako ukajifungia milango, lahashaa!

Mhe. Spika, suala ambalo nalo Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Wenyeviti) linamkereketa sana ni suala la Mradi wa *ZUSP*. Nafikiri wakati ukifika Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalu za SMZ atakuja kulitolea maelezo ya kina, lakini nataka kumhakikishia tu Mhe. Hamza Hassan kwamba asiwe na wasiwasi, kulikuwa na matatizo ya kiutendaji, lazima tukiri kwa upande wetu sisi, lakini zaidi upande wa Benki ya Dunia, yule Ofisa aliyekuwepo pale alipoondoka yeye hakuwa *very effective*, alikuwa hasukumi mambo. Sasa tunashukuru tumepata mtu mpya ambaye anasukuma kweli kweli na utaona hasa ile *component* na miradi mingi midogo midogo na mingi kwa kweli imesha-*take-off* na hiyo iliyobaki, basi iko njiani kukamilika. Kulikuwa kuna matatizo ya *Procurement*, hilo ndio tatizo kubwa sana, lakini asiwe na wasiwasi haujafutwa ule mradi, pesa zetu zipo na *Inshaallah, impact* yake itaonekana kwenye mitaro yake.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la DIASPORA. Waheshimiwa wengi walifurahishwa na wazo hili la DIASPORA na wakataka kujua hasa vipi wanachangia au wanatusaidia katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la mwisho ni suala la maeneo huru. Najua Mhe. Mnadhimu wangu hakupata nafasi, lakini suala hili nalo siku zote linamkereketa sana, nasema kwamba mipango ipo mizuri na tutagusia kidogo vipi linavyoendelea, lakini hata kwenye kitabu cha pili limeelezwa nitalizungumza baadae.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mengi Waheshimiwa wamegusa, lakini nitajaribu kuyatolea kwa kifupi ndani ya saa moja hii uliyonipa haya maeneo ambayo nimeyataja.

Mhe. Spika, naomba kabla sijaendelea ninyanyue Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa Uchaguzi Mkuu mwaka 2010. Katika kupanga siku zote mtu ana dira yake na sisi kama Chama Tawala hii ndio dira yetu na kama Chama Tawala hii ndio inayotuongoza. Mimi kama mwana CCM na wenzangu wanasiasa nasema kwa kweli hii imekidhi haja zote na wala Mhe. Abdalla Juma Abdalla najua alinitania alininyanyulia *Manifesto* ya *CUF* na mtani wangu Mhe. Saleh Nassor Juma, lakini nasema kwa sasa inayotumika ni hii na naomba ninukuu kidogo tu kwenye ukurasa wa kwanza kabisa kwa ruhusa yako Mhe. Spika, inasema;

"Ilani hii ya CCM imejengeka katika kukiri kwamba changamoto kwa serikali katika kipindi hiki ni ya kujenga uchumi wa kisasa na Taifa linalojitegemea. Vile vile, CCM inatambua kuwa *modernization* ya uchumi na

uwezeshaji wananchi kiuchumi ndio mikakati sahihi ya kujenga uchumi wa kisasa. Aidha, mafanikio ya azma hii unategemea kutambua hali na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya Karne ya 20 ya dunia na ya nchi".

Hii ilani imetoa muongozo katika uzalishaji mali, katika miundombinu na huduma za kiuchumi. Sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, sekta ya huduma za kijamii na mazingatio maalum ya ilani kuhusu Zanzibar. Pia, na maeneo mengine ya kipaumbele.

Mhe. Spika, kwa hiyo, kwa hii pamoja na miongozo mingine kama *Millennium Development Goals* au malengo ya milenia ambayo yako manane pamoja na MKUZA, hizi ndio nondo zetu tunazozitumia, hatuendi labda kama walivyozungumza wengine kwamba tunaikamata ilani peke yake na wanafikiri kwamba inatupotosha. Mimi nasema ni sahihi na ukitizama hayo malengo au ilani yetu na hayo malengo ya milenia na mengine kwa kweli tunakwenda sambamba.

Mhe. Spika, na hili usingoje kusifiwa, hawa wahisani wetu kwenye maendeleo wakija hapa wanaonesha kuridhika kwao na wanatwambia kabisa na kusifu, ndio maana utakuta inamaliza ilani na unamaliza mradi *Phase I* unakuja mwengine. Kwenye elimu, afya, mabarabara wanasifu kabisa utekelezaji wetu *Alhamdulillah*, sio kwengine sitaji wapi, lakini mradi ule wanakuja pale wanakuta msingi tu kwenye ripoti anaambiwa ushakamilika. Leo wanatembea hapa Vituo vya Afya vilivyojengwa wakimaliza kituo wanakwambia vipi hamtaki nyumba za wafanyakazi? tunataka, wanatoa. Kwa hiyo, walimu nao hivyo hivyo, chukulia mfano skuli za sekondari za *World Bank* zilivyojengwa nchi nzima, watu wameridhika kabisa na wanatupa na nyengine, miradi ya *TASAF* nayo hivyo hivyo.

Mhe. Spika, kwa hiyo, nataka kusema hatupangi peke yetu tu mipango na sisi tunakwenda Kimataifa na wenzetu, tunakwenda kwenye makongamano na tunakwenda kwenye semina. Tunapozungumza labu hatukuanza sisi, hizo labu na wenzetu wamefanya na tukapata kujua aa! ndivyo wanavyokwenda hivi na wenzetu wameonesha mafanikio kwa hizo labu. Kwa hivyo, nataka kusisitiza tu kwamba kupanga ni kuchagua, lazima uwe na nadharia kubwa na unachagua katika nadharia hiyo wapi wamefanya vizuri.

Mhe. Spika, hii imeshatuonesha mafanikio mbali mbali ambayo tumeyapata. Kuna baadhi ya wenzetu walisema kwamba miaka 50 hakujafanyika kitu. Hivyo, jamani tuchukulie miaka 203 ile ya Mkoloni kulikuwa na nini huko na uone hapa miaka 50 tu, hutaki kuvaa miwani wala hutaki kufanya uchambuzi wa kisiasa, mambo yako wazi kabisa. Sisi wengine tulilalia nyumba za makuti, tukapata pesa kidogo tukalalia nyumba ya debe, makuti na baadae madebe yale yanaitwa *kerosene*, baadae ikaja vipande vya mabati. Leo *Alhamdulillah* sio mabati tena, vigae na ukiruka na ndege unaona hasa hali ilivyokuwa nzuri.

Mhe. Spika, kwa hiyo, maendeleo kama haya si ya kubeza na yapo wazi kabisa, si Unguja, si Pemba. Naomba na imani yangu kwamba Waheshimiwa wengi tulipata hizi takwimu za mwaka 2012 zinaendelea kutoka kila mara na taarifa za kimsingi ya ki-*demographia*, kijamii na kiuchumi. Kwa kweli wametoa humu wamejaribu ku-*compare* sisi na wenzetu wa Tanzania Bara katika kusoma na kuandika kweli elimu tuko juu. Ukenda kwenye kiwango cha wenye kujua kusoma na kuandika kwa miaka 15 na zaidi tuko juu, ukija kwenye kiwango halisi cha uandikishaji katika shule za msingi tuko juu.

Mhe. Spika, hali ya makaazi ndio kabisa, mote kwa kweli humu tuko juu, vifaa vinavyotumika kujengea ukuta tuko juu wengine matofali ya udogo, sisi tunatumia saruji kabisa, vifaa vinatumia kwa kusakafia tuko juu, chanzo kikuu cha Nishati ya Kuangiza tuko juu. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba wakati mwengine mtu maendeleo yale mwenyewe hayaoni yalivyo. Kwa hiyo, nataka kusema kwa kweli tumepiga hatua kubwa sana jamani ndani ya miaka 50 yetu na imani yetu kwamba tutapiga hatua zaidi na zaidi hasa kuondokana na umasikini ambao tulikuwa nao.

Mhe. Spika, naomba niendelee kwa kifupi sana kuwakumbusha tu idadi ya watu tulikuwa wapi? Kwa sababu kadiri tunavyokuwa ndio lazima tunawajibika sasa kupanga vizuri na kuleta hatua mbali mbali za kimaendeleo. Mwaka 1964 Mapinduzi matukufu yanakuja, tuko watu laki tatu thalathini na moja elfu mia saba na sabini. Sensa ya mwaka 1988 tulichelewa kidogo kufanya sensa tukawa watu laki sita arubaini elfu mia tano sabini na nane. Ongezeko la watu laki tatu elfu nane mia nane na nane au sawa sawa na asilimia 93.

Mhe. Spika, Sensa nyengine mwaka 2002 tumetoka watu laki sita tukawa watu laki tisa thamanini na nne elfu mia sita ishirini na tano, sawa na ongezeko la watu laki sita hamsini na mbili elfu mia nane hamsini na tano au sawa sawa na asilimia 196.7. Sensa ya juzi ya mwaka 2012 tuko milioni moja laki tatu na tatu mia tano sitini na tisa. Ongezeko baada ya Mapinduzi watu laki tisa sabini na moja elfu mia saba tisini na tisa asilimia ongezeko 292. 9 milioni. Sasa hii inamaanisha nini kimipango?

Mhe. Spika, hii inamaanisha wazi kwamba tunauhitaji MKUZA. Hapa ndio kupanga, ndipo tunapopanga tunapochambua barabara hebu kumbuka 1964 zilivyokuwa, maji yalivyokuwa 1964, huduma za afya zilivyokuwa 1964. Mwenendo mzima wa serikali ulivyokuwa 1964. Sasa inaonesha wazi tungekaa tukasema vibarabara vyetu vya 1964 tungekuwa wapi? Kwa hiyo, MKUZA, Mwenyekiti wa *PAC* nathubutu kusema kwamba umefanyakazi kubwa sana ya kututoa tulikokuwa hadi hapa tulipo hii leo.

Mhe. Spika, katika suala ambalo Waheshimiwa wengi kama nilivyosema walizungumza ni suala la kukuwa kwa uchumi, watu wengi waliuliza naomba niseme tu kwamba katika uchumi mkuu, maana mbili za ukuwaji wa uchumi na maendeleo ya uchumi hushabihiana sana hasa katika kupambanua umuhimu wa ukuwaji wa uchumi na ongezeko la kipato na upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Spika, haya mambo naomba tuyazingatie hasa ukuwaji wa uchumi, kwenye ukuwaji wa uchumi maana yake ni kuongezeka kwa thamani ya uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa upana zaidi katika sekta mbali mbali nchini na hupimwa kwa ongezeko la thamani ya uzalishaji wa ndani wa bidhaa na huduma, yaani *JDP*. Kwa maana sahihi ukuwaji wa uchumi wa Zanzibar kwa wastani asilimia 7.4 kwa mwaka 2013 kumaanisha ukuwaji wa thamani ya uzalishaji wa ndani wa bidhaa na huduma kwa asilimia kama hizo.

Mhe. Spika, sasa nini maendeleo ya kiuchumi? Kwa maendeleo ya kiuchumi, maana yake ni kuimarika kwa hali ya maisha kwa wananchi na uhuru wa kuchagua kutokana na bidhaa na huduma mbali mbali nchini. Ni sahihi kwamba ukuwaji wa uchumi hupelekea maendeleo ya uchumi pindipo kasi ya ukuwaji wa uchumi kwa zaidi ya miaka 10, itakuwa marudufu ya kasi ya ukuwaji wa idadi ya watu tegemezi ndani ya nchi.

Mhe. Spika, kasi ya ukuwaji wa uchumi kwa Zanzibar bado haiwiani na kasi ya ongezeko la idadi ya watu, nafikiri nimesema zile *Population Trend* zilivyokwenda na idadi ya watu tegemezi nchini. Hali hii hupelekea kasi ndogo la uongezeko la kipato kwa wananchi na usambazaji wa huduma bora kwa maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba tangu miaka ya 70 kwa *Capital in come* kwa Zanzibar baina ya Zanzibar na Mauritius ilikuwa inalingana, lakini kwa miaka ya karibuni Mauritius imekuwa na pato la mtu binafsi kuwa kubwa kuliko Zanzibar na hii inatokana na sababu zifuatazo:-

Mhe. Spika, kwa vile pato la kila mwananchi hupatikana kwa kugawanya baina ya idadi ya watu nchini na jumla ya thamani ya uzalishaji inatokana na uzalishaji wa bidhaa na huduma. Kuna tofauti kubwa baina ya muundo wa idadi ya watu ambayo kwa Mauritius, idadi ya nguvu kazi ni 60 kwa sensa yao ya mwaka 2011 ikilinganishwa na Zanzibar.

Mhe.Spika, kwanza asilimia idadi ya watu tegemezi ni 62.8, kwa sensa ya mwaka 2012, tafauti hii hupelekea kupunguza kiwango cha kipato kwa kila mwananchi, yaani *Capital in come* ambacho hugawanya na idadi ndogo ya thamani ya uzalishaji unaotokana na nguvu kazi iliyopo.

Mhe.Spika, pili, kuhusu kuelimishwa wananchi juu ya maana ya ukuwaji wa uchumi na viashiria vyake ni kwamba Tume ya Mipango ikishirikiana na idadi ya mawasiliano Ikulu imeendelea kuelimisha wananchi juu ya juhudi ya serikali zilizopelekea ukuwaji wa uchumi kwa kusambaza nakala za vitabu, majarida vipeperushi mbali mbali, sambamba na kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo vya Habari na Magazeti.

Mhe.Spika, aidha zaidi ya nakala 1000 zinazoelekezea ukuwaji wa uchumi na maendeleo zilitolewa kupitia maonesho ya maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika *Bet-el Ras* na Tume ya Mipango imejipanga kuendelea na utoaji wa elimu hiyo kwa kila kipindi cha nusu mwaka.

Mhe. Spika, Waheshimiwa wengi walitaka kujua pia suala la miradi kwa ujumla na nini hasa mradi haishi, mbona mingi kumekuwa na utitiri. Sasa naomba tujiulize kwanza huu mradi hasa nini maana ya mradi? Tunajua tunaujua,

lakini twende. Nini maana ya mradi? Maana ya mradi ni kazi maalum iliyopangwa kufikia lengo mahasusi kwa muda uliopangwa, vigezo vya kuchagua miradi, kwanza mradi lazima uwe umekwenda sambamba na mikakati ya nchi ambayo ni dira ya maendeleo ya 2020 MKUZA II, Ilani ya Chama Tawala cha CCM na Sera ya Kimataifa. Pia, kunazingatia gharama za mradi.

Mhe. Spika, tatu kuwa miongoni mwa vipaumbele vya Taifa, mfano programu zilivyoibuka kwenye maabara.

Mhe. Spika, nne, miradi yenye tija nzuri kwa jamii kama kuongeza ajira kupunguza maradhi katika jamii kuongeza upatikanaji wa huduma za kijamii na mwisho miradi yote inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa sababu kule tuna uhakika pesa, zipo japo nao kidogo hali imekuwa si nzuri, nao wameonekana kutufikiria upya kutusaidia, lakini alau ukiwa na *External* Kampuni, basi *Automatically* unaipa tiketi kwamba huo mradi utatusaidia.

Mhe. Spika,vile vile, Waheshimiwa walituuliza huku kuchelewa Chelewa kwa miradi kunatokana na nini?

Mhe. Spika, hii inatokana na uhaba wa rasilimali zikiwemo fedha na rasilimali watu, lakini vile vile, mabadiliko ya miongo mfano miradi barabara kutotekelezwa wakati wa mvua, huwezi kujenga barabara wakati wa mvua, lakini hata ile misingi ya umwagiliaji aliyozungumza Mhe. Mtumwa Kheri huwezi kuijenga wakati wa mvua. Kwa hiyo, msimu nao ule wa utelezaji una- *affect* sana.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la sekta la viwanda, kwa mujibu wa *International Standard for Industrial Classification,* viwanda vimegawika katika maeneo makuu yafuatayo:-

Uchimbaji mchanga, madini na mawe, sio kama hii tunaweka sisi kwa mujibu wa Kimataifa *Classification* ya viwanda, lakini vile vile, bekari nazo ni jamii ya viwanda, utengenezaji matofali na viwanda vidogo vidogo vya uzalishaji.

Mhe. Spika, kulikuwa na masuala vile vile yaliulizwa juu ya takwimu za utalii, naona bora nilimalize kabisa, takwimu za idadi ya watalii wanaongia Zanzibar kweli zina matatizo tunakiri, lakini hii imetokana na takwimu zilizokuwa zimekusanywa ni za watalii wanaoshukia moja kwa moja Zanzibar na wanaoshukia Tanzania Bara hawakuwa wakirikodiwa hiyo ni *observation* yetu ya nyuma.

Mhe. Spika, kutokana na tatizo hilo, serikali imeanda mikakati mbali mbali kuondoa matatizo hayo ikiwemo majadiliano ya pamoja kwa sekta zote zinazohusina na masuala ya utalii, ni kuwa na takwimu moja. Sasa tumekaa *Institution* zote , watu wa *Airport* watu wa Utalii wenyewe, watu wa Bandari, nani anakuja pale? Wewe ni mtalii, basi tunarikodi hesabu yake tafauti na nyuma. Sekta hizo tumekubaliana kuweka Maafisa viwanja vya ndege na bandarini ili kuhakikisha kwamba wageni wote wanaoingia wanarikodiwa wakiingia nchini.

Mhe. Spika, vile vile, kulikuwa na suala zima la mashirikiano kati ya Sekta za Umma na binafsi, yaani *PPP*. *PPP* ni ile miradi ambayo serikali huwashirikisha watu binafsi katika utekelezaji wake, mara nyingi miradi hii hujikita katika maeneo ya ujenzi usimamizi na uendeshaji wa mradi na utoaji wa huduma. Matatizo yaliyojitokeza kwa kweli kwa kwetu tumegundua kwamba sheria imepitwa na wakati. Pia, hakuna hasa hiyo sera ya *PPP*. Vile vile, uwezo mdogo wa kitaaluma kwa watendaji sasa tumefanya nini?

Mhe. Spika, hapo tumeona ipo haja ya kuandaa Rasimu ya sera au sera ya *PPP*. Sasa Rasimu imeshaandaliwa na tunaifanyia kazi. Hatua itakayofuata baadae ni Sheria ya *PPP* nayo kufanyiwa mapitio na mshauri elekezo kutoa miongozo ya utekelezaji wa *PPP* na taaluma ya utendani wa *PPP* ameshawasili nchini na tayari ameshaanza kazi. Kwa hiyo, tuna muelekeo mzuri sana katika suala hili la *PPP*.

Mhe. Spika, nakumbuka Mhe. Asha Bakari alitaka kujua miradi mipya, nitataja kwenye sekta tu kwa sababu ni mingi kwenye programu mjumuisho ya kuendeleza utalii kwenye Programu ya mazingira bora ya biashara, kwenye Programu ya upatikanaji wa rasilimali fedha pia mradi wa kuijengea uwezo mamlaka ya maji awamu ya pili, uimarishaji wa miundo mbinu ya maji na michirizi Zanzibar, halafu *Bair Food Location Training in Centre in Zanzibar*, *Filteration of Zanzibar Archive* na kujenga uwezo wa kitengo cha utafiti na Ujenzi wa Chelezo cha uokozi.

Mhe. Spika, vile vile, kuna miradi katika kukamilika mwaka 2013/14, kwa mwaka huu serikali inategemea kukamilisha utekelezaji wa Programu moja na miradi mitatu kama ifuatavyo:-

(1) Kwa Wizara ya Kilimo Programu ya ujenzi wa barabara ya *Millennium Challenge Account* ;

(2) Wizara ya Kilimo na Maliasili, kuimarisha huduma za kilimo; na

(3) Kuangamiza adui kunguru na Wizara ya Afya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Mhe. Spika, aidha serikali imeamua kutenga shilingi bilioni 8.176, fedha ambazo zinagharamia Programu na miradi ambayo utekelezaji wake unaweza kukamilika kwa kipindi kifupi kijacho ili kupunguza idadi ya miradi kwa mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Elimu vile vile na *SUZA* awamu ya kwanza, halafu kuna kuimarisha huduma za Maktaba na kwa upande wa Wizara ya Fedha kuna ujenzi wa Wizara ya Katiba na Sheria. Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati usambazaji maji safi na Mazingira na Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais kuimarisha kiwanda cha uchapaji, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Ujenzi wa Studio na pia uimarishaji wa uwanja wa michezo. Hii ni miradi mbali mbali ambayo tunaendelea nayo.

Mhe. Spika, kwa upande wa fedha zilizotengwa ili ku-*support* ile *point* kwamba hiyo miradi sio kama utitiri tu au tunaipanga tu, lakini kwa kweli nataka nitoe fedha huko nyuma miaka mitano iliyopita tulikuwa wapi kwa upande wa miradi. Jumla ya fedha zilizopangwa kwa Programu ya miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha miaka saba 2008/2009.

Mhe. Spika, ilikuwa fedha zilizotengwa shilingi mia moja tisini na mbili elfu mbili sabini na tatu, nane tatu tano milioni, halafu 2009/2010, mia mbili thalathini tisa nukta tisa moja, mbili milioni, 2010/11 shilingi mia moja na tisini mbili milioni laki mbili na ishirini na saba elfu mia tatu thamanini na tatu, 2011/12 shilingi mia tatu sabini na nane elfu mia tisa na moja nukta tatu mbili tisa milioni, 2012/13 mia tatu arubaini na moja, moja, nne, sita, yaani *Trend* mpaka 2014/2015 tumetoka mia moja tisini na mbili mpaka mia tatu thalathini na moja bilioni. Sasa inaonesha *Trend* ya pesa ambazo tunazitenga kwenye miradi na kama nilivyosema inaomesha *criteria* za vipi tunaichagua hiyo miradi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Waheshimiwa wengi walizungumza au walitaka kujua ni suala la *Diaspora*. Kwa upande wa *Diaspora* nilitaka kusema tu kwamba sera ya *Diaspora* imefikia hatua ya kuridhisha na tumefanya hii kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimatiafa ya Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Uratibu wa Wazanzibari wanaishi nchi za nje pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya *Inter African Caribbean Pacific, Migration Facility,* pia, *International Organization for migration* katika utayarishaji wa sera hiyo.

Mhe. Spika, Rasimu ya awali ya sera tayari imeshajadiliwa katika kikoa cha wadau na watu na hatua inayofuata ni kuwasilisha Rasimu hiyo katika kikao cha Makatibu Wakuu. Sera itaanza kutumika *Inshaallah* katika mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, upande wa tovuti nayo Diaspora Zanzibar imekamilika na inapatikana kupitia *www. Zanzibar Diaspora. Co. TZ.*

Mhe. Spika, katika hatua za kuwatafuta, kuwatambua na kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kupitia Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na uratibu wa Wazanzibari wanaoshi nchi za nje kwa mashirikiano ya wadau mbali mbali wakiwemo Benki ya Watu Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi wa Jamii, Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi *ZIPA*, Shirika la Bima na Tume ya Mipango iliandaa safari maalum katika nchi mbali mbali zikiwemo Oman, *UK*, Dubai na Denmark ili kuona na kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na Wazanzibari wanaoshi katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, Wazanzibari hao wanaoneshwa kuguswa na nchi yao na baadhi yao tayari wameanza kuitikia wito wa kutoa michango yao katika Sekta za Elimu na Afya kwa kisiwa cha Unguja na Pemba. Katika maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora imetayarisha kipindi maalum kupitia *ZBC*

Television kinachoitwa Diaspora kwa Maendeleo ya Zanzibar. Waliobahatika kukiona watakuwa na kumbukumbu nzuri.

Mhe. Spika, vile vile, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora imeendelea kuelimisha umma juu ya dhana ya Diaspora kupitia vipindi vya redio katika Maelezo Baada ya Habari na *Television.*

Mhe. Spika, kulikuwa pia kuna michango mingi iliyogusa katika suala zima la karafuu. Upande wa karafuu Mhe. Mwakilishi alitaka kujua vipi mkulima amesaidiwa na anafaidika vipi?

Mhe. Spika, naomba kuthubutu kusema kwamba hii leo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kumfanya mkulima aweke mwenyewe au a-*retain* abaki na mauzo ya asilimia 80 ya *World price* au ya bei ya karafuu inayouzwa ulimwenguni.

Mhe. Spika, natoa mfano kama kule inauzwa tani moja dola elfu moja, basi mwananchi anabaki na dola 800, dola 200 tu au asilimia 20 tu, hizo ndio zinabaki serikalini. Sasa matumaini yetu kwamba pesa hizi mwananchi huyu azitie kwenye maendeleo ya nchi na maendeleo yake mwenyewe zizunguke zisibaki mifukoni hiyo, ndio mtizamo wetu na imani yangu mwenyewe Mhe. Waziri wakati wa bajeti atakuja kueleza haya, lakini kwa kweli faida kubwa sana tumeipata katika zao letu la karafuu baada ya mabadiliko ya bei.

Mhe. Spika, alizungumza kidogo tu MKUZA umefeli, Mhe. Omar nafikiri sitaki kulirejea mafanikio makubwa kama alivyosema yamepatikana kwa kweli katika sekta zote kama; kilimo, afya, elimu, maji, nyumba na masoko na lile suala la uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi, watu wengi waliona kama dhihaka kwamba kweli ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 26. Ninachosema hii imepigwa hesabu kwa mujibu wa idadi ya walimu na wanafunzi waliopo na ni kweli wapo hawa.

Mhe. Spika, lakini sasa *in reality* wangapi wapo wanaofundisha darasani hilo ni suala jengine? Lakini kwa hesabu zetu wale waliopo walimu na wanafunzi kwa hesabu zao wengine wanakwenda *martenity* na unajua walimu wengi sana wanaweza kufika 250 kwa wakati mmoja, wengi wanaumwa, wengine wamekwenda kusoma, wanaweza kufika walimu 1,000. Kwa hiyo, pengine utaona *ratio* hii *in practical* haipatikani, lakini hasa *theoretically* kwa mahesabu yetu hii ndio ilivyo. Sasa utakuta kidogo ina-*mislead,* nafikiri tutachukua *home-work* kukaa chini kuona hasa ukweli uko wapi na vipi tuweze kurekebisha.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la *PPP* Bandari ya Mpigaduri. Ninachotaka kusema nakumbuka Mhe. Rufai Said Rufai na wengine walizungumza sana, imekuwa nyimbo tu Mpigaduri weee, Mpigaduri, ile dhana ya Bandari ya Mpigaduri ilikuwepo siku nyingi sana, kwa sababu kwanza ule uzuri wa pale mahala, kina cha maji na ile kujificha kwake, wanasema ni *very visible,* yaani panavutia mno, pamekaa kibandari bandari hasa.

Mhe. Spika, sasa ule wakati tu ulikuwa haujafika. Sasa nataka kusema tu kwamba *Alhamdulillah, Feasibility Study* tayari imeshatayarishwa na kupelekwa kwa wafadhili wetu ambao ni *Exim Bank* ya China na hata Kampuni imeshapatikana na tunaambiwa kwamba makisio tu ni kiasi cha dola 230 milioni. Kwa hiyo, kwa sasa niseme mipango yetu mizuri ya bandari hii na *Inshaallah,* ule msongamano wa bandari hii hapa ya Malindi na lengo letu kwamba kule sasa ndio kwende mizigo, hapa tubaki na abiria wetu.

Mhe. Spika, lakini hatuishii hapo hata kama kuna wazo, kama mfano nasema tu itatokea wazo la bandari nyengine kwengine, basi tunalikaribisha ni maendeleo hayo katika nchi moja, lakini kwa sasa tunabaki na wazo hilo la Mpigaduri. *Airport* ya Pemba nayo iliulizwa, mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha analijua vizuri na atakuja kulitolea ufafanuzi, lakini kuna habari nzuri sana kwa wawekezaji kutoka Uturuki.

Mhe. Spika, kulikuwa na matatizo kidogo ya takwimu mapato ya ndani kati ya Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango. Rafiki yangu Mhe. Hija Hassan Hija ni kweli tukiri kwamba hiyo imetokezea na tofauti ile hasa kwamba ilitokezea sisi Tume ya Mipango tulichukua *data* ambazo baadae wenzetu wa Wizara ya Fedha walizifanyia *Adjustment,* walipofanya *Adjustment,* sisi tukawa hatuna habari, lakini kwenye lile halina taathira yoyote ni ndogo sana ile *margin* yenyewe na hiyo tutaweka sawa. Naomba nikiri Mhe. Hija *observation* yako ni sahihi kabisa.

Mhe. Spika, namalizia kulikuwa na suala la mradi wa uhakika wa chakula na lishe, nakumbuka Mhe. Bikame Yussuf Hamad aliuliza upo huo au tunatania tu. Naomba Mhe. Bikame ufungue kitabu cha pili ukurasa wa 15-16

umeeleza kwa ufasaha kabisa kwamba mradi ule upo na programu hii inaitwa Programu ya Kusaidia Kilimo na Uhakika wa Chakula na imeelezwa mpaka zile harakati na kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Programu imepangiwa shilingi milioni 50 za Serikali na shilingi milioni 570.5 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa hiyo, ukisoma kwenye ukurasa wa 15-16 mradi huu Mhe. Bikame utauona.

Mhe. Spika, lakini vile vile, kwa upande wa maeneo huru nao Waheshimiwa wengi walitaka kujua na Mnadhimu wangu. Naomba ukiangalia ukurasa wa 57 na 58 kuna maelezo mazuri sana ya kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2014/2015, kwa upande wa kuimarisha maeneo huru na mradi wenyewe unaitwa Mradi wa Utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Maeneo Huru Fumba. Kulikuwa na matatizo ya kutiwa pesa, lakini mwaka huu tayari pesa zimetengwa nzuri tu kwa kukamilisha kazi hiyo, umepangiwa shilingi milioni 150 kutoka serikalini.

Mhe. Spika, mwaka jana katika kitabu cha Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa, ukikiangalia tulitoa maelezo ya kina hasa kwa kila *component* ya mradi wa *ZUSP* sijui kama mnavyo, lakini utaona hasa jina la ule mradi na sehemu ya utekelezaji wake, baadae nitampa Mhe. Waziri Haji Omar Kheir aweze ku-*update* kuona pale mwaka huu walipo.

Mhe. Spika, kama nitakuwa nimesahau kwa *component* moja au nyengine, naomba radhi si lengo langu, lakini kwa kweli kama nilivyosema ni nia yetu sisi kwamba yale yote ambayo mmetuelekeza, mmetushauri, mmetwambia tutayachukua, labda nimalizie tu kulikuwa na matatizo kwamba na yalikuwa *very strong* tumeambiwa kwamba uchumi wetu hatuujui tunakwenda tu.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema si kweli, kama nilivyosema kupanga ni kuchagua, tulianza na uchumi wa *monoculture* uchumi wa karafuu tu, zikiyumba kukawa na programu nyengine au na sera nyengine ya *diversification* kutafuta mbadala mwengine wa zao gani ambalo la fedha litatusaidia. Tukafikiria labda mambo ya bei ya mwani wakati wa Mzee Aboud Jumbe, halafu wakati wa Komandoo Dkt. Salmin Amour Juma tukaja na *trade liberalization,* huu ndio tulipo-*open up,* sasa kwa sekta ya biashara, hapo *Alhamdulillah* tukaanza kuona macho.

Mhe. Spika, ulipokuja utalii tena ndio ukaweka sawa zaidi. Kwa hiyo, hii yote ni kupanga na unapanga kwa mujibu wa wakati.Sasa ikiwa wewe wakati umegeuka wewe bado umeng'ang'ania vile vile, hapo ndio utakapokwama. Kwa hiyo, sasa tunatizama vipi tutakwenda kwenye *industrialization* tuone tutafaidika vipi na viwanda. Hivi viliopo tuvifufue tuongeze vyengine tuweke hali nzuri ya kuwavutia wenzetu, tumetoka kwenye *monoculture economy* na MKUZA, huyo MKUZA ndio aliyetufunua macho akatuelekeza tunapanga, tunatathmini, tunakwenda, hiyo ndio *economic transformation* na mpaka hii leo tupo hapa tulipo.
Mhe. Spika, nafikiri kwa haya machache na kama nilivyosema mwenzangu Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja kwa sababu ameshakaa kwenye hii sekta kwa muda mrefu na ujuzi wake na utaalamu wake, naamini atasawazisha yale ambayo nimeyasahau na mengine amalizie kabisa.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunisikiliza na naomba nitoe hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majumuisho hayo uliyoyafanya. Hoja imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe sasa hoja hiyo tuiamue. Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na kuupitisha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi pamoja na Mpango wa Maendeleo mwaka 2014/2015, wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana. Mhe. Waziri wa Fedha alinambia kwamba na yeye yupo tayari sina hakika kama anaweza akamudu kuna muda kama nusu saa hivi. Nilikuwa najaribu kumuangalia kama anaweza kumudu kwa muda huo na dalili inaonekana kwamba na kwa ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe kwamba haitawezekana na ni kweli baada ya michango mingi sana iliyotoka inafaa Mhe. Waziri wa Fedha ajitanafasi ili aweze kufafanua mambo mbali mbali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyahoji na kuyauliza na mengine kutoa maelekezo yao.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda hautoshi ili Mhe. Waziri wa Fedha afanye majumuisho, naomba basi tusitishe shughuli zetu hizi ili tuje kesho asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali, basi kazi hii nayo iweze kumalizika. Tunasitisha shughuli zetu hadi kesho tarehe 21 Mei, 2014 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:15 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/05/2014 saa 3:00 asubuhi)